# CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

## Taasisi ya Elimu Endelezi

# OFP 008

# KISWAHILI

Kimetolewa na:
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Barabara ya Kawawa,
S.L.P 23409,
Dar es Salaam,
TANZANIA.
www.out.ac.tz

Toleo la Kwanza, 2008
Toleo la Pili, 2018

**ISBN : 987 9987 00 248 1**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigiza, kunakili au kukitoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Haki za mwandishi wa kitabu hiki zinalindwa na mkataba baina yake na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# Yaliyomo

**DIBAJI** .......... **5**

**UTANGULIZI WA KOZI** .......... **5**

**SEHEMU 1:**

**LUGHA, NADHARIA YA UKUAJI WA LUGHA, HISTORIA NA KUENEA KWA LUGHA YA KISWAHILI**

**Muhadhara 1: Lugha ni Nini?** .......... **6**

1.1 Utangulizi .......... 6
1.2 Asili ya Lugha .......... 7
1.3 Maana ya Lugha .......... 7
1.4 Aina za Lugha .......... 9
1.5 Mitazamo Mbalimbali Juu ya Fasili ya Dhana ya Lugha .......... 10
1.6 Tabia za Lugha .......... 11
1.7 Sifa za Lugha .......... 12
1.8 Hitimisho .......... 15

**Muhadhara 2 : Nadharia ya Ukuaji wa Lugha** .......... **17**

2.1 Utangulizi .......... 17
2.2 Njia za Uundaji wa Msamiati .......... 19
2.3 Vigezo Vitumikavyo Kupima Ukuaji wa Lugha .......... 24

**Muhadhara 3: Historia Fupi ya Kiswahili** .......... **26**

3.1 Utangulizi .......... 26
3.2 Nadharia Mbalimbali Kuhusu Historia ya Kiswahili .......... 27
3.3 Hitimisho .......... 43

**Muhadhara 4: Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili Nchini Tanzania** .......... **45**

4.1 Utangulizi .......... 45
4.2 Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili Kabla ya Ukoloni .......... 45
4.3 Tanzania Wakati wa Ukoloni .......... 46
4.4 Hitimisho .......... 51

**SEHEMU 2:**

**FONETIKI, FONOLOJIA, NA MOFOLOJIA**

**Muhadhara 5: Fonetiki** .......... **52**

5.1 Utangulizi ........ 52
5.2 Maana Ya Fonetiki ........ 52
5.3 Matawi ya Fonetiki ........ 53
5.4 Uainishaji wa Sauti ........ 56

**Muhadhara 6 : Fonolojia ya Kiswahili ........ 66**
6.1 Utangulizi ........ 66
6.2 Dhana ya Fonolojia ........ 66
6.3 Tofauti kati ya Fonetiki na Fonolojia ........ 67
6.4 Dhana ya Fonimu ........ 68
6.5 Silabi ........ 72

**Muhadhara 7: Mofolojia ya Kiswahili kwa Ujumla ........ 78**
7.1 Utangulizi ........ 78
7.2 Maana ya Mofolojia ........ 78
7.3 Alomofu ........ 89
7.4 Mofimu ........ 95
7.5 Neno ni Nini? ........ 97

**Muhadhara 8: Uambishaji na Mnyambuliko wa Maneno ........ 99**
8.1 Utangulizi ........ 99
8.2 Uambishaji ........ 100
8.3 Mnyambuliko ........ 101
8.4 Aina za Viambishi ........ 103
8.5 Dhima ya Viambishi Katika Neno ........ 104
8.6 Hitimisho ........ 105

**SEHEMU 3:**
**MAWANDA YA SINTAKSIA**

**Muhadhara 9: Mawanda ya Sintaksia ........ 108**
9 .1 Utangulizi ........ 108
9.2 Fasili ya Sintaksia ........ 108
9.3 Malengo ya Ufafanuzi wa Kisintaksia ........ 110

**Muhadhara 10: Kategoria za Kisintaksia na Ushahidi wa Kuwepo Kwazo ........ 112**
10.1 Utangulizi ........ 112
10.2 Dhana ya Kategoria ........ 112
10.3 Ushahidi wa Kuwapo kwa Kategoria za Kileksika ........ 114
10.4 Hitimisho ........ 117

**Muhadhara 11: Kategoria za Virai ........ 118**
11.1 Utangulizi ........ 118

11.2 Dhana ya Kirai ........................................ 119
11.3 Muundo wa Kirai ........................................ 120
11.4 Aina za Virai ........................................ 121

**Muhadhara 12: Uainishaji wa Sentensi ........................................ 125**
12.1 Utangulizi ........................................ 125
12.2 Dhana ya Sentensi ........................................ 125
12.3 Aina za Sentensi ........................................ 126
12.4 Hitimisho ........................................ 130

**Muhadhara 13: Kategoria za Kidhima ........................................ 132**
13.1 Utangulizi ........................................ 132
13.2 Kategoria za Kidhima ........................................ 132
13.3 Hitimisho ........................................ 139

**SEHEMU 4:**
**UCHAMBUZI WA SENTENSI NA SEMANTIKI**

**Muhadhara 14 : Uchambuzi/Uchanganuzi wa Sentensi ........................................ 141**
14.2 Mifano ya Uchambuzi/Uchanganuzi wa Sentensi kwa Njia ya Maelezo ........................................ 141
14.3 Kwa Njia ya Mishale ........................................ 143
14.4 Kwa Njia ya Matawi ........................................ 145

**Muhadhara 15: Semantiki ........................................ 149**
15.1 Utangulizi ........................................ 149
15.2 Maana ........................................ 149
15.3 Aina za Maana ........................................ 150
15.4 Uhusiano wa Maana ........................................ 151
15.5 Viwango vya Maana ........................................ 153

**SEHEMU 5:**
**FASIHI**

**Muhadhara 16: Fasihi kwa Ujumla ........................................ 159**
16.1 Utangulizi ........................................ 159
16.2 Maana ya Fasihi ........................................ 159
16.3 Chimbuko la Fasihi ........................................ 160

**Muhadhara 17: Fasihi ya Kiswahili ........................................ 165**
17.2 Fasihi ya Kiswahili ni ipi? ........................................ 165
17.3 Fasihi ya Waswahili ........................................ 166
17.4 Fasihi ya Kiswahili ........................................ 167
17.5 Uhusiano wa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ........................................ 170

17.6 Tofauti za Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ......171
17.7 Hitimisho ......173

**SEHEMU 6:**
**FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI, UHAKIKI NA UTUNGAJI**

**Muhadhara 18: Fani na Maudhui katika Fasihi ......175**
18.1 Utangulizi ......175
18.2 Fani na Maudhui ......175
18.3 Vipengele muhimu vya fani na maudhui vijengavyo kazi ya fasihi andishi ......177
18.4 Wahusika katika Fasihi ya Kiswahili ......179

**Muhadhara 19: Uhakiki wa Kazi za Fasihi ......183**
19.1 Utangulizi ......183
19.2 Mhakiki Ni Nani? ......183
19.3 Sifa za Mhakiki ......183
19.4 Dhima za Mhakiki ......185
19.5 Uhakiki wa Fasihi ......187

**Muhadhara 20: Utungaji ......193**
20.1 Utangulizi ......193
20.2 Insha/Utungaji ......193
20.3 Aina za Insha ......193
20.4 Sehemu za Insha ......194
20.5 Jinsi ya Kuandika Insha ......195
20.6 Miundo Mbali Mbali ya Insha ......196
20.7 Malengo ya Insha/Utungaji ......197

# DIBAJI

Kozi hii ni miongoni mwa kozi kumi na tano (15) za mwaka mmoja katika mfululizo wa Programu ya Maandalizi (Foundation Programme). Kozi hii pia ni mojawapo ya kozi kwa wanafunzi wa Stashahada ya Ualimu wa Shule za Msingi (Diploma in Primary Teacher Education).

# Utangulizi wa Kozi

Kozi hii ni ya Somo la Kiswahili. Walimu wako katika Taasisi wameziteua mada ambazo wanafikiri ni za msingi kuzifahamu kabla hujajiandikisha katika masomo ya shahada ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kila mada ina sura yake. Kwa jumla ziko sura ishirini. Baadhi ya mada zinaweza kuwa ni za kukukumbusha tu kwani huenda ulizisoma ukiwa katika Shule ya Sekondari. Vinginevyo, sehemu kubwa ya mada zilizoelezwa katika sura zinazounda kozi hii ni maarifa mapya kwako ambayo ukiyasoma kwa makini na kutafakari, bila shaka utafanikiwa katika Kozi hii muhimu.

# Madhumuni ya Kozi

Utakapomaliza kusoma kozi hii, utaweza:

1. Kueleza maana ya lugha na chimbuko la lugha ya Kiswahili.
2. Kuunda tungo mbalimbali.
3. Kuelezea muundo wa maneno ya Kiswahili.
4. Kutambua kategoria za kisintaksia na ushahidi wa kuwepo kwazo
5. Kuainisha sentensi za Kiswahili na kuzichanganua kwa njia mbalimbali
6. Kutathmini fasihi ya Kiswahili kwa jumla

Tunatumai utaisoma Kozi hii kwa ari, nguvu na kasi mpya nasi tunakutakia mafanikio mazuri.

# MUHADHARA 1

# Lugha ni Nini?

## 1.1 Utangulizi

Ukitaka kuelewa lugha ni nini uwe unawasikiliza watu wanapozungumza lugha ambayo huielewi huku jambo lililozungumzwa linakuhusu moja kwa moja .Katika hali kama hiyo wewe mwenyewe mazungumzo hayo yataonekana ni mwingiliano wa sauti tu ambazo zinakuletea kelele tu.Lakini wahusika yamkini utawaona wakicheka,wakikutazama ,wakihuzunika ,wakioneshana ishara na kuonesha hisia zao.Wewe yamkini utaambulia kuona ishara na kupata hisia kutokana na uzoefu wa jamii utokayo.kimsingi wao huelewana kwa lugha waitumiayo hali hii ndio hujumuiswa na kutoa jibu la kwamba lugha ni chombo cha mawasiliano.

Swali la kujiuliza :ni kwa namna gani kelele zinazosikika zikitamkwa mara kadhaa na kwa namna fulani tofauti tofauti ,zinawezesha kuelewana ,kupeana maelekezo ,kuwasilisha ujumbe na kupeana habari kwa kila muhusika wa kelele hizo.Yamkini wazo unaloweza kupata kwa haraka linaweza kuwa lazima kelele zitolewazo na wahusika zina maana fulani ijulikanayo kwa wasemaji /watamkaji wa kelele hizo.Kwa hakika kelele za namna hiyo zikifikia kiwango cha kuweza kufikisha mawasiliano juu ya masuala yanayojitokeza katika jamii fulani ndipo kelele hizo huitwa **lugha** ya jamii husika.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu utaweza:

- Kueleza asili ya lugha
- Kueleza maana /dhana ya lugha
- Kujadili aina za lugha
- Kujadili mitazamo mbalimbali ya fasili ya dhana ya lugha
- Kujadili tabia za lugha.
- Kufafanua sifa za lugha.

## 1.2 Asili ya Lugha

Ni dhahiri kuwa kila jamii ina hadithi zake kuhusu jinsi lugha yake ilivyozaliwa/kuanza.Lakini katika historia kuna hadithi nyingi zinazohusu asili/chimbiko la lugha zote za binadamu.Mojawapo ya hadithi hizo ile inayosimuliwa katika kitabu maarufu kama Biblia inayohusu chanzo cha watu kunena lugha mbalimbali wakati wa ujenzi wa mnara wa Babeli.Ambapo inasemekana kwamba kulitokea kutoelewana kwa kila mmoja kuzungumza lugha yake na huo ukawa mwanzo wa lugha mbalimbali Duniani.Hadithi hii yaelekea kuwa na ukweli kiimani zaidi kwani watu wa imani hii huamini kuwa ni kweli lakini kitaalumu hakuna kigenzo chochote ambacho kinaweza kidhibitisha ukweli huo.

### 1.2.1 Mtazamo wa kiisimu

Kiisimu asili ya lugha huweza kutazamwa kwa namna mbili .namna ya kwanza ni ile inayoangalia hali za mabadiliko ya binadamu toka kale hadi kupata lugha asili ambazo zote ni kamili kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya jamii fulani. Katika mtazamo huu inaelezwa kwamba lugha huweza kuzuka kukua na kufa.Namna ya pili ya mtazamo juu ya asili ya lugha ni ule unaozingatia namna motto anavyoipata lugha.Kimsingi ni dhahiri kwamba hakuna motto anayezaliwa akiwa na lugha au uwezo wa kuzungumza lugha fulani . Badala yake kila motto huzaliwa katika hali ya kawaida bila lugha lakini huwa na uwezo wa kupata lugha yeyote ya jamii inayomlea au jamii inayomzunguka.ukiangalia namna hii utagundua kuwa ili mtoto aweze kupata lugha ni lazima awe miongoni mwa jamii ya watu.mpaka sasa wataalamu hawajasema lolote iwapo mtoto ataachwa mahali bila kuwa na mwingiliano na watu /jamii yeyote atakuwa na lugha au atakuwa na athari gani kilugha kutokana na upweke huo.

Katika ujumla wake umejifunza kwamba chimbuko la lugha linafungamana sana na maumbile pamoja na mazingira ya mtu binafsi na jamii yake kwa mda mrefu.katika kipengele cha muda haijajulikana vema muda kamili ni upi na hivyo kupelekea kuwepo na simulizi kuhusu chimbuko la binadamu na lugha yake.

## 1.3 Maana ya Lugha

Fasili ya lugha kwa mujibu wa wa crystal (1992) anasema :"lugha ni mfumo wa sauti nasibu, ishara au maandishi kwa ajili ya mawasiliano na kujieleza katika jamii ya watu"

Katika fasili yake ametaja mambo makuu matano ambayo ni mfumo,*sauti za nasibu, sautialama na ishara,jamii ya wanadamu, mawasiliano na kujieleza/kujitambulisha*.
Ili kupata dhana nzima ya fasili hii ni muhimu tuangalia kila kipengele katika fasili yake:

### 1.3.1 Mfumo

Kila lugha ina muundo wake ambao huwa ni fofauti na lugha nyingine.kwa maana hii kila lugha ni kijisehemu cha miundo iliyopo katika kundi zima la miundo ya lugha duniani.miundo hiyo yaweza kuwa jinsi maneno yalivyoundwa jinsi maneno yalivyofuatana.hivyo kila lugha ina ruwaza maalumu.

### 1.3.2 Sauti Nasibu

Hapa ina maana kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya neno na kile kinachowakilishwa katika lugha.Hivyo maana inayowakilishwa huwa ni ya kinasibu tu au inatokana na makubaliano ya wanajamii/watumiaji wa lugha fulani katika mazungumzo yao ambayo huwa yanatofautiana kutoka rika moja hadi jingine.

**Mfano**: Neno MEZA halina maana ya moja kwa moja na umbo linalowakilishwa.

### 1.3.3 Sauti, Alama na Ishara

Kimsingi kila lugha huteua sauti ,alama au ishara zianazowakilisha wazo au ujumbe.lugha nyingi hutumia sauti katika mazungumzo wakati baadhi ya lugha hutumia ishara za maandishi katika mawasiliano na lugha nyingine hutumia alama katika kukamilisha mawasiliano.

### 1.3.4 Jamii ya Wanadamu

Kimsingi ni wanadamu pekee ndio watumiao lugha na ni jamii zao pekee zinazoteua maneno na kuyapa maana waitakayo katika jamii hiyo sambamba na jinsi gani miundo ya lugha zao wanataka ziwe.Viumbe wengine wana njia za mawasiliano ambazo zinatofautiana kabisa na njia za mawasiliano ya wanadamu.Hivyo lugha huwa ni kwa wanadamu tuu.

### 1.3.5 Mawasiliano

Katika kueleza dhana nzima ya lugha inafaa kugusa dhima ya lugha hiyo kwa wale waitumiayo.Lugha hutumika kama njia kuu ya mawasiliano.Kwa kupitia lugha watu huweza kutoa na kupokea ujumbe

pamoja na kutolea hisia zao.Kwa kutumia lugha tunasema tukitakacho ili kukidhi mahitaji yetu.Mawasiliano katika lugha kunaajumuisha kuzungumza ,kuandika,kusoma na hata kutumia mifumo mingine ya ishara.njia zote hizi ni njia za mawasiliano kwa kutumia lugha.

Katika ufafanuzi wa dhana ya lugha ni muhimu kuzingatia vipengele vilivyojadiliwa hapo juu ilio kutoa dhana ya lugha kwa upana wake.

## 1.4 Aina za Lugha

Kwa kutumia msingi wa kutazama hali halisi na mifumo ya sauti na ishara anayoitumia binadamu kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake ya lugha katika jamii,wataalamu wa lugha wameafikiana kutenga lugha katika aina kuu mbili ambazo ni lugha asili na lugha unde.

### 1.4.1 Lugha za Asili

Lugha asili ni ile lugha inayohusisha mfumo wa sauti zinazotolewa kwa kutumia ala katika chemba ya mdomo wa binadamu Lugha asili ina sifa za kuwa na viwango tofauti katika muundo wake,na huwa na uwezo wa kuzalisha tungo zisizo na ukomo/kikomo.kwa mujibu wa mwanaisimu John Lyons,lugha asili ina viwango viwili muhimu vya muundo ambavyo ni :

(i) Kiwango cha msingi kinachohusisha vipashio kamili vyenye maana kama vile maneno
(ii) Kiwango kisicho msingi kinachihusisha vipashio ambavyo vyenyewe havina maana lakini hutumika katika kuunda vipashio vipashio vya msingi.vipashio hivi huwa ni sauti katika lugha (Lyons 1970:11-13)

Sifa hii ya uwezo wa kuzalisha tungo zisizo na ukomo kimsingi inahusu hasa uwezo wa binadamu wa kuunda na kuelewa idadi isiyo kikomo ya maumbo ya maneno na sentensi katika lugha yake.hii hufanyika kiasili bila mhusika kukusudia kutumia kanuni fulani za kisarufi katika lugha yake.Katika uzalishaji huu mtumiaji wa lugha hutumia sauti fulani ili kupata maneno ya aina fulani.Kwa mfano kwa kutumia sauti i,m,l na a katika mipangilio mbalimbali ,katika Kiswahili tunaweza kupata maneno kama imla, lima, lami.

Pia kwa kutumia muundo wa aina moja kuweza kuzalisha sentensi nyingi mbalimbali.kwa mfano kwa kutumia muundo wa wenye KIIMA, KITENZI NA YAMBWA ianwezekana kupata sentensi kama:

Tembo amemla mtu

Mtu amemla tembo

Mwalimu anasoma gazeti

Mama anapika ugali

Mkulima analima karanga.n.k.

### 1.4.2 Lugha Unde

Lugha unde ni ile inayohusu mfumo wa ishara ambazo binadamu amezibuni na huzitoa kwa kutumia viungo vyake vya mwili kama mikono,vidole kope za macho n,k maandishi pia huingia kwenye kundi la hili kwani ni nyenzo mojawapo anazoziunda mwanadamu ili kikidhi mahitaji yake ya mawasiliano.katika hali ya kawaida lugha hii huwa na maana tofautitofauti kutokana na rika la watu uhusiano wao,mahali, tukio napengine mahitaji yake.

Hadi leo haijajulikana kama wanyama wana aina gani ya lugha kati ya hizi.chakujiuliza ni je wanyama wana lugha ?na kama wanayo ipo katika kundi gani?aidha sifa zilizobainishwa zinaelezea kitu kinachoitwa lugha na kudokeza kwamba si kila njia ya mawasiliano ni lugha katika maana ileile ya lugha.

## 1.5 Mitazamo Mbalimbali Juu ya Fasili ya Dhana ya Lugha

Wataalamu wengi wameileza dhana ya lugha tangu miaka ya 1920 na 1930 hususan wanaisimu wa skuli ya isimu-miundo ambao ni Leonard Bloomfield na Edward Sapir.mawazo yao kuhusu ni lugha ni kwamba (i)lugha ni ishara (ii)ishara hizo huzihusisha moja kwa moja na ala za sauti zilizomo katika bomba la sauti,(iii)sauti hizo zimo katika mfumo maalumu,(iv)mfumo huo wa sauti ni wanasibu(V)kwa kutumia mfumo huo wa nasibu, jamii inayoitumia lugha husika huwasiliana.zipo fafanuzi nyingine za lugha ambazo zimejikita katika misingi ya Nyanja totauti ya kitaaluma kama ifuatavyo:

Kwa wanafalsafa wanaona lugha ni chombo cha fikra. Wao huona kwamba mtu hawuzi kufkiri bila kuwa na lugha hivyo lugha ni chombo cha fikra.

Kwa wanazuoni /wanaelimu jamii wanaona kwamba lugha ni namna fulani ya tabia.wao huhusiana namna mtu anavyotumia /anavyoongea na tabia yake kama mtu anaongea maneno yote kwa ukali hiyo ndio tabia yake na tofauti yake ni sahihi.

Kwa wanasaikolojia wanaona lugha ni mlango wa kutambua akili za binadamu wao wanaamini kwamba bila lugha huwezi kutambua akili za watu.

Ama kwa hakika wapo wataalamu wengine ambao huenda wamefafanua zaidi juu ya dhana nzima ya neno lugha ni jukumu,lako kutafua zaidi juu ya dhana hii.

## 1.6 Tabia za Lugha

Ama kwa hakika zipo tabia ambazo zinajitokeza kwa kila lugha ,tabia hizo zinaihalalisha lugha fulani kuwa lugha kwa maana halisi ya lugha.

### 1.6.1 Tabia ya kukua

Lugha ina tabia ya kukua,lugha inavyozidi kutumika katika jamii huongeza maneno kulingana na mahitaji, kitendo hicho hupelekea lugha kuwa na tabia ya kukua.Katika mchakato huu maneno ya zamani hubadilika na maneno mapya hujitokeza,mabadiliko haya hujitokeza kutokana na maendeleo ya kijamii,maendeleo ya sayansi na teknolojia.mabadiliko haya huwa yanajikita katika nyanja zote za kimaisha yaani kisiasa kiuchumi na kiutamaduni,kwa mfano kipindi cha maendeleo ya vyama vingi ndipo tulipopata misamiati ya ngangari ngunguri n.k pia kuna misamiati kama kasheshe,kilimo kwanza,kompyuta n.k.

### 1.6.2 Tabia ya kuathiri na kuathiriwa

Lugha ina tabia ya kuathiri lugha na kuathiriwa na lugha nyingine.kwa kawaida lugha inavyochua maneno fulani kutoka lugha nyingine huwa inaathiri lugha inakochukua maneno wakati lugha inayopokea maneno yale huwa inakuwa inaathiriwa na lugha ile.ni dhahiri kwamba Kiswahili kimeathiriwa na lugha ya kiarabu,kibantu,na kiingereza,wakati huohuo Kiswahili kimeathiri lugha hizo.

### 1.6.3 Tabia ya ubora

Lugha ina tabia ya ubora .Tabia hii ina maana kwamba kila lugha ni bora kwa wale wanaoitumia .Hakuna lugha iliyobora kuliko nyingine kwani kwa wale wanaoitumia inawafaa.Ijapokuwa upo uwezekano wa kuwa na bora lugha, bora lugha hujitokeza sana kwenye rejesta ambazo huzingatia mawasiliano ya kundi fulani na hivyo kuwa na bora lugha badala ya lugha bora.

### 1.6.4 Tabia ya kujitosheleza

Lugha ina tabia ya kujitosheleza kulingana na mahitaji ya jamii ambayo inaitumia.Tabia hii hujipambanua wazi kutokana na kujitosheleza kimsamiati kulingana na mahitaji ya jamii husika.

## 1.7 Sifa za Lugha

**Lugha huhalalishwa kuwa lugha kutokana na sifa zifuatazo:**

***(i) Lugha ni lazima imuhusu Mwanadamu***

Ama kwa hakika hakuna kiumbe kisichokuwa mwanadamu (mtu)kinachoweza kuzungumza lugha kwa maana halisi ya lugha.Lugha ni chombo maalumu wanachotumia wanadamu kwa lengo kuu la mawasliano.Kwa mantiki hiyo basi sifa kuu ya chombo hiki ni lazima kiwe kinamhusu mwanadamu na si vinginevyo.

***(ii) Sauti***

lugha ambayo inamhusu mwanadamu,huambatana na sauti za binadamu zinazotoka kinywani mwake.Katika jambo hili ni lazima mwanadamu atamke jambo kinyani mwakekwa sauti.Ijapokuwa mwanadamu anaweza kutumia njia nyingine ya maandisha na akawa amefikia lengo lake la mawasiliano.

***(iii) Lugha ni lazima iwe na utaratibu maalumu***

Kama ilivoelezwa kwenye fasili ya lugha kuwa lugha ni sauti zenye utaratibu maalumu.ambao hupangwa kwa kufuata utaratibu fulani unaokubalika kwa jamii hiyo ya watu.Kwa maana hiyo basi si kila sauti itokayo kinywani mwa mwanadamu ni lugha,itakuwa lugha iwapo itakuwa imefuata taratibu zinazokubalika katika jamii husika.mfano mtoto anapolia anatoa sauti lakini hatuwezi kusema kulia ni

lugha kwa sababu ni sauti inayotoka kinywani la hasha.Utaratibu wa sauti hizo kwa neon moja hitwa Sarufi.

Mfano:

(a) Hatusemi.

(i) Juma wimbo anaimba.

(ii) Kitabu changu mimi nimekipoteza.

(b) Jamii imepatana kusema kwa utaratibu ufuatao:

(i) Juma anaimba Wimbo.

(ii) Mimi nimekipoteza kitabu changu.

***(iv) Lugha huwa na misingi ya Fonimu.***

Lugha hufuata misingi ya fonimu ,ambapo lugha ina vitakwa au vipashio ambayo huitwa fonimu.wanaisimu wanakubaliana kwa ujumla kwamba fonomu ni sauti yenye uwezo wa kuleta tofauti katika maana ikipachikwa katika neno la lugha husika.Baadhi ya fonomu za lugha ya Kiswahili:

1./a/,/e/,/i/,/o/,/u/.

Katika neno {tata} tunaweza kupachika fonimu nyingine na tukapata maana tofauti tofauti kama ifuatavyo:

{tata}={teta}={tita}={tota}={tuta}

Pia katika neno {taa} tunaweza kuzalisha maneno yafuatayo:

{taa}={tea}={tia}=[toa}={tua}

2./p/,/b/,/t/,/d/,/f/,/k/,/g/,/s/,/z/n.k

Tunaweza kupata maneno kama pawa,bawa,tawa,dawa,chawa,jawa,gawa sawa zawa na maneno mengi mengineyo.

***(v) Lugha hufuata mpangilio wa vipashio unaoleta maana***

Lugha ni lazima iwe na mpangilio wa vipashio mpangilio huo huwa unafahamika na watumiaji wa lugha husika. Katika mpangilio huo ndipo unapotokea muundo wa sentensi kwa maana kwamba ili sentensi iwe na maana ni lazima vijenzi vya sentensi hiyo view kwenye mpangilio unaokubalika.katika lugha ya kiwsahili mpangilio huo huanza na fonomu,neno,kirai,kshazi na hatimaye sentensi.

**(vi) Lugha Husharabu**

Lugha husharabu /hushabihiana hii ina maana kwamba lugha huchukua baadhi ya maneno kutoka

Lugha nyingine ili kujiongezea msamiati wake. Tabia hii inazisaidia sana lugha zinazokua.Katika tabia hii lugha ikishachukua neno kutoka lugha nyingine hulifanya neno lile liendae na maneno mengine ya lugha husika.Kimsingi vitu viwili vinaweza kutokea katika tabia hii,kwanza lugha inaweza kuchua neno kutoka lugha fulani na kulitumia kama lilivyo,pili lugha inaweza kuchukua neno kutoka lugha nyingine na kulirekebisha ili liendane na mfumo mzima wa lugha husika.Vitu vyote hivi kwa neno moja huitwa kusharabu.

***(vii) Lugha Inajizalisha***

Lugha ina sifa ya kutumia vipashio vyake kujiongezea misamiati/maneno mapya.Kujizalisha kwa lugha huweza kutokea kwa njia ya kunyambulishaji na mara nyingine lugha hujipatia misamiati kutokana na urudufishaji.

Unyambulishaji hufanyika pale vipashio vinapopachikwa kwenye mzizi wa neno ili kuzalisha maneno mengine.

***UNYAMBULISHAJI***

***UAMBISHAJI*** ***UNYAMBUAJI***

***MZIZI***

***KIELELEZO***

Unyambulishaji unahusu kitendo cha kuongeza vipashio mbele na nyuma ya mzizi. Uambishaji katika Kiswahili hutokea kabla ya mzizi wakati unyambuaji hutokea baada ya mzizi.

Katika mzizi{-lim-} inawezekana kufanya unyambulishaji na kupata maneno kama:

(a) Yeye Analima

(b) Wewe Unalima

(c) Mimi Ninalima

(d) Wao wanalima

Kutokana na mfano wa hapo juu utaona kwamba uambishaji unaopofanyika unaendana sambamba na upatanishi wa kisarufi kama inavyoonekana katika mfano hapo juu a-d

Hata hivyo katika unyambuaji Kiswahili hujiongezea msamiati kwa kuzalisha maneno mapya,angalia mifano ifuatayo:

(a) pig=>ku-pig-a=>ku-m-pig-a=>tu-li-m-pig-a

(b) pig-i-a=>pig-ish-a=>pig-ish-an-a=>pig-ik-a

(c) pig-ik-a

## 1.8 Hitimisho

Lugha ni lazima iwe sauti za kusemwa na binadamu. Sauti hizo za binadamu lazima ziwe na utaratibu maalumu wa kuwasiliana, na kama hakuna utaratibu maalumu hiyo siyo lugha. Sauti na milio iko mingi duniani, milio ile inayoweza kuwafanya binadamu wawasiliane ndiyo tunayoiita lugha.

Lugha lazima iwe na sifa zinazoambatana na tabia za binadamu katika utamaduni wake. Vinginevyo lugha husika itakuwa si asilia

### Zoezi

1. Lugha ni nini ?
2. Jadili sifa za lugha ukitoa mifano muafaka
3. Jadili tabia ya lugha
4. Fafanua dhana zinazokusudiwa na Wana-Isimu wanaodai kwamba :
    (a) Lugha husharabu
    (b) Lugha ni mfumo wa sauti nasibu
    (c) Lugha ni sauti, alama, ishara
    (d) Lugha ni mawasiliano
    (e) Lugha hutambulisha msemaji
5. Jadili jinsi lugha na watumiaji wake wanavyoshirikiana kitabia katika jamii husika

## Marejeo


1. Grimes, B. (2000), *Ethnologue*, 14th ed. Dallas: SIL.
2. Nkwera, Fr. F. V. (2003), *Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo.* Creative Prints Ltd: Dar es Salaam.
3. Habwe, J na Karanja, P. (2004), *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.*
4. Bussman, H. (1996) *Routedge Dictionary of language and linguistics.*

# MUHADHARA 2

# Nadharia ya Ukuaji wa Lugha

## 2.1 Utangulizi

Kuna mambo mbalimbali yanayofanya lugha yoyote ikue. Mambo hayo ni kama vile matumizi ya lugha katika shughuli mbalimbali kama vile:

- Shughuli za utawala na kampeni za kisiasa.
- Shughuli za kibiashara ndani na nje ya nchi.
- Maswala ya Elimu.
- Mikutano ya nchi (kitaifa) na kimataifa.
- Shughuli mbalimbali za kiutamaduni, muziki, sherehe, nk.
- Matumizi ya lugha katika vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni, nk.
- Urahisi wa lugha yenyewe katika kueleweka na kuweza kuchukua maneno ya kigeni au maneno ya utamaduni wa mataifa mengine bila mgogoro.

Urahisi huo wa lugha waweza kuwa katika:

(i) Matamshi yake

(ii) Msamiati

(iii) Miundo

(iv) Maana-:mfano neno moja kuwa na maana zaidi ya moja, nk.

(v) Mwingiliano wa tamaduni mbalimbali na uhamiaji wa kigeni.

(vi) Vita. Husababisha kuchangamana kwa watu wengi pamoja na hivyo huweza kusababisha lugha ya utamaduni fulani kuenea na kukua haraka ukilinganisha na lugha za tamaduni nyingine.

(vii) Usanifishaji. Husababisha lugha fulani iteuliwe kutumika katika nyanja fulani kama elimu, utawala, biashara, nk. Na hivyo lugha hiyo hukua. Kutokana na usanifishaji ndipo tunapata lugha rasmi na lugha ya taifa.

Hivyo kukua kwa lugha ni hali ya kuongezeka kwa msamiati. Msamiati ni jumla ya maneno yanayotumiwa katika lugha fulani. Ili lugha yoyote ikue lazima msamiati wake ukuzwe.

Sababu za uundaji wa msamiati/maneno ni kama zifuatazo:

(a) Kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo huchukua

sura mpya kila siku.

(b) Kwa ajili ya kuweza kutafsiri mengi kutoka lugha yako kwenda lugha ya kigeni au kutoka lugha ya kigeni kuingia katika lugha yako.

(c) Ili kupata msamiati unaokubalika na shughuli mahsusi kama vile benki, forodhani, Jeshini, nk.

(d) Kwa ajili ya matumizi ya utamaduni wa watu wa taifa hili

au hata taifa jingine. Jambo la muhimu ni kuona msamiati wa Kiswahili unaendelezwa ili kukidhi haja ya watumiaji wa Kiswahili katika kupokea maingiliano ya fani mpya za utamaduni wa kigeni.

(e) Ili kukidhi msamiati wa masomo yote katika lugha yako, ambayo hapa ni Kiswahili.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu utaweza:

- Kuielewa dhana ya uundaji wa msamiati
- Kujua njia mbalimbali za uundaji wa msamiati

## 2.2 Njia za Uundaji wa Msamiati

Njia zinazojitokeza katika uundaji wa msamiati ni kama ifuatavyo:

**Njia ya kutumia mpangilio tofauti wa fonimu au vitamkwa:**

Kila lugha ina fonimu au sauti za msingi ambazo hutumika kujenga silabi ambazo nazo hujenga maneno yote ya lugha husika. Maneno mengi katika lugha huweza kupatikana kwa kubadili mpangilio wa vitamkwa/sauti-fonimu za lugha husika.

Kwa mfano:

Sauti-fonimu /a/, /o/, /n/ zikibadilishiwa mpangilio kwa namna mbalimbali zinaweza kuzalisha maneno kama vile:

(i) o-n-a => ona (ii) => noa (iii) => oana.

(ii) Sauti- fonimu /i/m/l/a/tunaweza kupata (i)=> lima (ii)=>imla (iii)=> lami

**Njia ya miambatano yaani kuunganisha maneno:**

Hapa maneno mawili yanaunganishwa na kuwa neno moja. Kuna aina mbalimbali za miambatano:

(i) Miambatano kati ya jina huru na jina huru.

*mwana + hewa* ⇨ *mwanahewa*

*mwana + nchi* ⇨ *mwananchi*

*Afisa + misitu* ⇨ *Afisamisitu*

(ii) Miambatano kati ya Nomino na Kivumishi.

*Mla + mbivu* ⇨ *Mlambivu*

*Mwana + kwetu* ⇨ *Mwanakwetu.*

(iii) Miambatano kati ya jina tegemezi na jina huru. Jina tegemezi linatokana na kitenzi.

*Mpiga + maji* ⇨ *Mpigamaji.*

*Mpiga + mbizi* ⇨ *Mpigambizi*

(iv) Miambatano kati ya kitenzi na jina.

*Piga + mbizi* ⇒ *pigambizi*

*Pima + maji* ⇒ *pimamaji*

**Kutohoa maneno:**

Kila lugha ina uwezo wa kuchukua maneno kutoka kwenye lugha nyingine ili kukidhi haja ya mawasiliano kulingana na maendeleo ya jamii. Kiswahili nacho kimechukua maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni na lugha za Kibantu na kuyatohoa ili kusadifu misingi ya sarufi yake.

Mfano:

(a) Kiingereza:

(i) tractror => trekta => trekita => terekita

(ii) plaugh => plau => pulau

(iii) shirt => sheti => shati

(iv) geography => jiografia => jografia

(v) machine => mashine

(b) Kiarabu:

(i) laki => pokea

(ii) ahadi => milele

(iii) dhaifu => nyonge

(iv) ila => isipokuwa

(c) Kireno:

(i) bibo => bibo

(ii) roda => roda

(ii) mesa => meza

(iii) copa => kopa

(d) Kiajemi:

(i) bandar => bandari

(ii) dirisha => dirisha

(iii) kod => kodi

(iv) pilao => pilau.

(e) Kihindi:

(i) achari => achari

(ii) biyme => bima

(iii) ghati => gati

(iv) lakh => laki

(f) Kijerumani:

(i) schule => shule

(ii) hella => hela

(g) Kutoka Lugha za Kibantu

(i) faculty => kitivo <kipare/kisambaa.

(ii) composite => kivung <kipare

(iii) state house => ikulu <kigogo/kisukuma

(iv) national assembly => bunge<kigogo/kisambaa

(v) fluid => ugiligili <kinyakyusa

**Njia ya urudufishaji:**

Hii ni njia ya kurudia neno, likawa neon moja.

Mfano:

(i) kimbele => kimbele mbele

(ii) pole => pole pole

(iii) kinyume => kinyume nyume

(iv) kimya => kimya kimya

(v) kizungu => kizungu zungu

**Kwa njia ya kufupisha maneno:**

Njia ya kufupisha maneno inachukua ama herufu ama silabi ya kwanza ya kila neno lililojitokeza katika jina zima la mahali au kitu funi.

Mfano:

(i) **T**aasisi ya **U**chunguzi wa **Ki**swahili => **TUKI**

(ii) **Ba**raza la **Ki**swahili **Ta**nzania => **BAKITA**

(iii) **C**hama **C**ha **M**apinduzi => **C.C.M**

(iv) **Ba**raza la **Mi**tihani la **Ta**ifa => **BAMITA**

**Njia ya kutumia mnyambuliko na uambishaji:**

Neno jipya huundwa kwa kuunganisha viambishi kwenye mzizi au shina la neno. Njia hii hukuza lugha bila taabu kwani maneno ya lugha nyingi yanaweza kunyumbuliwa na kuambishwa, kama ifuatavyo:

(a) Mnyambuliko wa Majina:

(i) taifa => taifisha => taifishwa => taifishiwa. nk.

(ii) soma => somea => somesha => someshea => someshwa => someshewa => somesheka => , nk.

(b) Mnyambuliko wa Vitenzi:

(i) piga => pigana => pigisha => pigishwa => pigishia => pigia => pigiana, pigika, nk.

(ii) cheza => chezana => chezesha => chezeshwa => chezeshea => chezeana => chezwa => chezeka, nk.

(c) Mnyambuliko wa Vivumishi:

(i) fupi => fupisha => fupishia => fupishwa => fupishiwa => => fupishana => fupishika, nk.

(ii) safi => safisha => safishana => safishia => safishiana => safishika, nk.

(d) Mnyambuliko wa Vielezi:

(i) haraka => harakisha => harakishana => harakishika => harakishia => harakishiana, nk.

**Njia ya Kutumia Uambishaji**

(i) taifa => utaifa, mataifa, utaifishaji, nk.

(ii) piga => kupigana, anapiga, nk.

(iii) safi => msafi, wasafi, nk.

(iv) haraka => kuharakisha, nk.

**Njia ya kufananisha sauti/umbo:**

Baadhi ya maneno ya Kiswahili yametokana na mwigo wa sauti au dhana ya kitu fulani.

Mfano:

(i) *Piki-piki- piki-piki* => pikipiki,

Neno ambalo limetokana na mwigo wa sauti (mlio) wa chombo husika.

(ii) *tu-tu-tu* => mtutu (wa bunduki)

neno ambalo limetokana na mwigo wa sauti ya risasi inapotoka kwenye bunduki baada ya kufyatuliwa.

(iii) *kifaru*

Hii ni zana ya kivita ambayo imepewa jina hilo kutokana na umbo lake lililofanana na mnyama aitwaye kifaru.

**Njia ya vijenzi/viundaji**:

Mara nyingi *vijenzi* huunda neno ambalo huwa *nomino*. Vijenzi hupachikwa mwishoni mwa kitenzi ili kiwe nomino. Maneno yanayojitokeza huwa na maana na ngeli tafauti tafauti.

Vijenzi vitumikavyo ni kama ifuatavyo:

| **Kijenzi** | **Kitenzi** | **Nomino** |
|---|---|---|
| **{i}** | jenga | mjenz**i** |
| | linda | mlinz**i** |
| | soma | msom**i** |
| | panda | mpanz**i** |
| **{ji}** | winda | mwinda**ji** |
| | soma | msoma**ji** |
| | sema | msema**ji** |
| | cheza | mcheza**ji** |
| | linda | mlinda**ji** |
| **{o}** | soma | som**o**/masom**o** |
| | sema | msem**o**/misem**o** |
| | cheza | mchez**o** |

| | | |
|---|---|---|
| **{u}** | kua | uku**u** |
| | tulia | utulivu /mtulivu |
| | tukuka | utukufu/mtukufu |
| | choka | uchovu |
| **{e}** | teua | mteule |
| | tuma | mtume |
| | kata | mkate |
| | umba | kiumbe |

**Njia ya kukopa maneno kutoka lugha nyingine**

## 2.3 Vigezo Vitumikavyo Kupima Ukuaji wa Lugha

Ukuaji wa lugha ni tabia mojawapo ya lugha**.**Vigezo vitumikavyo kupima ukuaji wa lugha ni kama ifuatavyo:

(i) Matumizi katika nyanja mbalimbali kama vile elimu, dini, utawala, biashara, nk.

(ii) Kupanuka kwa msamiati wenyewe.

(iii) Kupanuka kwa miundo katika lugha.

(iv) Kupanuka katika maana na maneno.

**Zoezi**

(a) Kila lugha hukuza msamiati wake.
Eleza sababu za hoja hii.

(b) Kwa kutumia mifano ya lugha ya Kiswahili, fafanua
njia zinazoweza kutumiwa katika kukuza msamiati wa Kiswahili.

(c) Jadili mbinu zitumikazo katika kukuza msamiati wa lugha.

## Marejeo


1. Massamba, D. P. B na Wenzake (2001) Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo. (Chapa ya pili) DSM: TUKI.
2. Habwe, H na Karanja P (2006) Darubini ya Kiswahili: Marudio Kamili ya KCSE. Nairobi: Phoenix Publishers

# MUHADHARA 3

# Historia Fupi ya Kiswahili

## 3.1 Utangulizi

Katika mihadhara iliyotangulia tumefafanua dhana ya lugha, lakini pia dhana ya fasihi ambayo inatumia Kiswahili kama lugha ya kuumulika utamaduni wa jamii inayotumia Kiswahili katika mawasiliano kuhusu shughuli zao za kila siku hususan, Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Aidha, tumefafanua matawi ya sarufi inayoijenga lugha ya Kiswahili, hususan fonolojia, mofolojia, na sintaksia. Mihadhara iliyotangulia zinahitimishwa na muhadhara unaozungumzia baadhi ya mada zinazotumika katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule hususan za Tanzania na Afrika Mashariki kwa jumla, yaani: kusoma, imla, ufahamu, muhtasari na utungaji.

Baada ya kufahamishwa taswira ya lugha ya Kiswahili, sasa ni wakati muafaka wa kuelezea kwa kifupi juu ya asili ya lugha ya Kiswahili. Tunapozungumzia historia ya kitu fulani, tunakufahamisha asili au chimbuko la kitu hicho. Neno asili lina maana ya jinsi kitu au jambo lilivyotokea au lilivyoanza. Kwa hiyo tunapoangalia asili ya Kiswahili tunaangalia jinsi Kiswahili kilivyotokea au kilivyoanza.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu unatarajiwa kuweza:

(i) Kueleza dhana mbalimbalikuhusu historia ya Kiswahili.

(ii) Kueleza kwamba Historia ya Kiswahili inatokana na Historia ya Kibantu kwa ushahidi wa ki-Historia na wa ki-Isimu

(iii) Kujadili Chimbuko la Lugha ya Kiswahili.

(iv) Kufafanua vyombo vinavyohusika katika kukikuza, kukisanifisha na kukieneza Kiswahili.

## 3.2 Nadharia Mbalimbali Kuhusu Historia ya Kiswahili

Pamekuwa na nadharia kadha wa kadha kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili. Katika kozi hii, tutazitaja baadhi tu ya nadharia muhimu zinazodaiwa.

### 3.2.1 Kiswahili Asili Yake ni Kongo

Baadhi ya wataalamu hudai kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni huko Kongo ambayo baadaye iliitwa Zaire na sasa inaitwa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Dai hili linaimarishwa na wazo lingine linalodai kwamba katika vipindi kongwe vilivyopata kuwako, sehemu za Pwani ya Afrika mashariki hazikuwa zimekaliwa na watu. Kutokana na hali ya vita, uchungaji na biashara, inadaiwa kuwa Wabantu walitoka sehemu za Kongo walisambaa na kuja pwani ya Afrika mashariki kupitia Kigoma. Baadhi ya wabantu hawa walipitia sehemu za Uganda. Wakati wa kusambaa kwao, walieneza pia lugha zao ikiwemo hii ya Kiswahili.

Udhaifu wa nadharia hii ni kwamba, madai ya kuwa asili ya Kiswahili ni Kongo hayana msingi kwani mpaka sasa wataalamu wanaodai hivi hawajaweza kueleza na kuthibitisha kisayansi ama Kihistoria juu ya lini hasa watu walianza kuishi pwani ya Afrika mashariki.

### 3.2.2 Kiswahili ni Ki-Pijini au ni Ki-Krioli

#### *(i) Kiswahili ni Ki-Pijini*

Baadhi ya wataalamu hudai kuwa Kiswahili ni Ki-Pijini. Wataalamu hawa hudai kwamba Ki-Pijini ni lugha ambayo huzaliwa kutokana na kukutanika kwa makundi mawili (A) na (B) yanayotumia lugha mbili tofauti. Ili makundi haya yaweze kuwasiliana kunaundwa lugha ambayo kitabia ni tofauti na zile zinazozungumzwa na makundi yanayohusika. Lugha hii inaweza kuwa na msamiati mwingi kutoka lugha kati ya zile mbili, au inaweza kuwa na msamiati wenye uzito sawa. Lugha hiyo ndiyo inayoitwa Ki-Pijini. Mazingira yanayosababisha kuwepo Ki-Pijini ni kama vile biashara, utumwa, ukoloni, nk.

Kwa mantiki ya nadharia hii, wataalamu hawa hukiona Kiswahili kuwa kilianza kama Ki-Pijini kwani ni tokeo la mwingiliano baina ya wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki na wageni wa kutoka

Mashariki ya Kati, hususan Waarabu. Aidha, husisitiza kuwa lugha ya Kiswahili haikuwepo kabla ya hapo.

**Zingatia**

Wataalamu wa nadharia hii hudai kwamba Kiswahili ni lugha ya kati iliyozuka ili kurahisisha/kufanikisha mawasiliano katika shughuli ya biashara ya mwanzo kwa sababu hapakuwa na mfanya-biashara mmoja wao (A) aliyeijua lugha ya mfanya-biashara mwenzake (B). Lugha inayozushwa na makundi haya mawili (A) na (B) huitwa Ki-Pijini.

***(ii) Kiswahili ni Ki-Krioli***

Wataalamu hawa wanadai kwamba watu wanaozungumza Ki- Pijini wanaweza kuishi pamoja kwa muda wa karne nyingi na kwa hiyo wakaweza kuzoeana na hata kufikia hatua ya kuoana. Wakioana watoto wao huikuta lugha ya ki-Pijini ama lugha yao ya kwanza. Inapofikia hatua ya aina hii kwa watoto wanaozungumza lugha hiyo, wao husemekana sasa wanazungumza lugha ya Ki-Krioli, lugha ambayo ni hatua ya juu ya Ki-Pijini, yaani Ki-Pijini kilichokomaa.

Nadharia hii hutumia kigezo cha msamiati wa Kiswahili kuonesha uhusiano uliopo kati ya Kiswahili na Kiarabu. Wanadai kuwa, msamiati mwingi wa Kiswahili unatokana na Kiarabu. Hivyo huhitimisha kuwa hapana shaka Kiarabu kimehusika katika kuizalisha na kuikomaza lugha ya Kiswahili.

Udhaifu wa nadharia hii ni kwamba hutumia kigezo cha msamiati tu bila kuzingatia vipengele vingine vya lugha kama vile matamshi, maumbo ya maneno au muundo wa sentensi za Kiswahili. Aidha, wataalamu hawa hawakuhoji suala la kufanana kwa Kiswahili na lugha jirani katika hayo yaliyotajwa hapo juu na katika eneo la Kijografia ambamo Kiswahili na lugha hizo nyingine hujikuta zikizungumzwa. Vigezo hivi ni ushahidi tosha unaoonesha kuwa Kiswahili SI Ki-Pijini wala SI Ki-Krioli, bali ni lugha kama zilivyo hizo lugha jirani.

**Zingatia**

**Kiswahili *si* pijini wala -krioli**

**Zoezi**

Je, pana ushahidi wo wote wa ki-hitoria kuhusu madai haya?

### 3.2.3 Kiswahili ni Lugha ya Jamii ya Vizalia

Kundi la kwanza la wataalamu wa nadharia hii, Bishop Edward Steera, Bwana Taylor, Dkt. R. Reusch, (Katika Maganga, 1997) hudai kwamba:

- Waarabu na Waajemi waliohamia pwani ya Afrika ya Mashariki waliwaoa wanawake wa ki-Afrika.
- Watoto wao walijifunza maneno ya Kiarabu na ki-Ajemi kutoka kwa baba zao.
- Aidha, watoto hao wakajifunza maneno ya ki-Bantu kutoka kwa mama zao.
- Katika jitihada zao, watoto hao walijirekebisha kutokana na tamaduni za wazazi wao ambazo ni tafauti: utamaduni wa Kiarabu na utamaduni wa kiBantu.
- Vizalia hawa wakaanza kutumia lugha mpya ya mseto wa Kiarabu, Kiajemi na lahaja mbalimbali za ki-Bantu.
- Kwa kiasi kikubwa, lugha mpya ya mseto ilikuwa ni upotoshaji wa lugha ya Kiarabu na Kiajemi.
- Mwarabu au Mu-Ajemi alikuwa muumini wa dini ya Uislamu.
- Umo humo, vizalia hawa wakayaingiza maneno ya Kiarabu, Kishirazi na Kihindi katika hii lugha mpya.
- Pamoja na kuyaingiza maneno ya kigeni, lugha-mpya yao hii (Kiswahili), ilikithiri vionjo vingi vya lugha mbali mbali za ki-Bantu.
- Ndipo baadaye, lughampya yao hii ikajulikana au kuitwa Kiswahili.

- Kwa maoni ya wataalamu hawa, sehemu mbili kati ya tano (2/5)ya maneno yanayotumika katika lugha hii mpya ni ya ki-Bantu.
- Sarufi ya lugha mpya hii ni mseto wa ki-Bantu (chenye utata na kisicho na mpangilio maalumu) pamoja na Kiarabu (chenye mantiki na kilichokomaa).

Kundi la pili la wataalamu wa nadharia hii, B. Krumm na F. Johnson lina mawazo yanayodai kwamba:

- Kiswahili kilitokana na visiwa vya Lamu, Kilamu/Kiamu.
- Wageni kutoka Ghuba ya Ushirazi/Uajemi na Arabia ya Kusini walikuja katika Pwani ya Afrika ya Mashariki na lugha tofauti.
- Lakini kutokana na kuoana kwao na wenyeji, wageni hawa wakaichukua lugha ya hapo walipofikia, wakaikuza kwa maneno kadhaa na sentensi kadhaa kutoka lugha zao za asili, yaani Kiarabu, Kiajemi na Kihindi hususan katika masuala ya biashara, ubaharia, vyombo vya kazi zao na nguo.
- Aidha, utumwa na tabia ya kuoa wake wengi ilisaidia kutoa kundi kubwa la masuria. Hali hii ikaondosha hisia za ugeni katika lugha zao; na maneno yote yakabatizwa kuwa ya ki-Bantu, na hata kupoteza kabisa sura ya ugeni.

**Zingatia**

Japokuwa mtazamo wa nadharia hii ni kwamba Kiswahili ni lugha ya vizalia wa Waarabu na Waajemi, kwa upande mmoja, na Wabantu kwa upande mwingine, nadharia hii imeshindwa kuthibitisha ki-historia na ki-isimu kuwepo kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki na visiwa vya jirani ambazo zinahusiana katika matamshi, msamiati na mofolojia kwa ujumla.

### 3.2.4 Kiswahili ni Kiarabu

Kuna hoja kuu tatu ambazo baadhi ya wananadharia hii huzitumia kutetea nadharia hii kuwa Kiswahili asili yake ni Kiarabu.

(i) Inadaiwa kuwa maneno yenye asili ya Kiarabu yaliyomo katika Kiswahili ni ishara tosha kwamba lugha hii ilianza kama Pijini ya Kiarabu.

(ii) Inahusu neno lenyewe Kiswahili ambalo asili yake ni Kiarabu. Neno Kiswahili linatokana na neno "sahili" (umoja) na "swahil" (wingi) lina maana ya pwani.

(iii) Inadaiwa kwamba kwa kuwa Kiswahili kilianza pwani, kwa kuwa idadi kubwa sana ya wenyeji wa pwani ni waislamu, na kwa kuwa uisilamu uliletwa na Waarabu, basi Kiswahili nacho kililetwa na Waarabu.

### 3.2.5 Kiswahili si Kiarabu

Madai kwamba Kiswahili **si** Kiarabu yanathibitishwa na hoja kinzani zifuatazo:

- Tukianza na dai la kwanza 'kwamba maneno yenye asili ya Kiarabu yaliyomo katika Kiswahili ni ishara tosha kwamba lugha hii ilianza kama pijini ya Kiarabu' tunaona wazi kwamba madai haya hayana mashiko. Lugha ya Kiswahili imetokea kuwa na maneno ya mkopo yenye asili ya Kiarabu (na kwa hakika yapo yenye asili ya Kiajemi, Kireno, Kihindi, Kijerumani, Kiingereza nk.) kutokana na ukweli kwamba kulikuwa na mawasiliano ya karne na karne baina ya wenyeji wa pwani na wafanyabiashara wa Kiarabu. Wasemaji wa lugha mbili tofauti wanapokutana hawaachi kuathiriana kilugha. Kwa hiyo lugha kuwa na maneno mengi ya mkopo kutoka lugha nyingine, haifanyi lugha hiyo isemekane kuwa imetokana na hiyo lugha nyingine.

- Pili wataalamu hawa wanadai kwamba neno lenyewe *Kiswahili* lina maana ya Kiarabu. Kwani linatokana na neno "sahili" (umoja) na "swahil" (wingi) lina maana ya pwani. Hapa ingetupasa tuelewe kwamba kila mtu binafsi au jamii binafsi aghalabu hajiiti mwenyewe jina lake, yeye huitwa kwa hilo jina alilopewa na wengine: Jamii yake au wageni waliomtembelea kwake. Na hivi ndivyo ilivyojitokeza kwa upande wa jamii ya watu wa pwani ya Afrika mashariki, yaani Waswahili, walipotembelewa na Waarabu na kuitwa As-Sahilyy au AsSawahiliyy, na nchi yao kuitwa sahil (wingi wake Sawahil), yaani pwani (upwa), ufuo. Kwa mantiki hii, dai hili halina mashiko !

Kigezo cha dini nacho hakikubaliki lugha haiwi lugha kwa sababu ya imani. Hata hivyo lugha ya Kiarabu yenyewe ilikuwepo karne nyingi kabla ya kufunuliwa dini ya Uislamu. Hali kadhalika, lugha nyingine za Kimagharibi zilikuwepo karne nyingi kabla ya kufunuliwa imani ya ukristo. Kama ilivyo

kwamba Kiingereza au Kijerumani si ukristo, basi ndivyo vivi hivyo ilivyo kwamba Kiswahili hakiwezi kuwa dini ya uislamu, aslan! Wala Kiarabu nacho si uislamu. Tunachoweza kufanya ni kuitumia lugha kuifasili dini, lakini hatuwezi kuitumia dini kuifasili lugha.

**Zingatia**

Kiswahili si ki-Pijini wala Krioli wala si ki-Arabu wala ki-Ajemi

**Zoezi**

Thibitisha kwamba Kiswahili **si** ki-Pijini wala **si**-Krioli wala **si** KiArabu wala **si** kiAjemi

### 3.2.6 Kiswahili ni Kibantu

Vipengele vinavyotumika katika kuihalalisha nadharia inayodai kwamba Kiswahili ni Kibantu ni ushahidi wa ki-Isimu, ushahidi wa ki-Historia na kuichunguza lugha ya Kiswahili katika mfumo mzima wa historia ya mgawanyiko wa kusambaa kwa lugha za ki-Bantu. Wataalamu wa nadharia hii wanahitimisha kwa kudai kwamba Kiswahili ni mojawapo kati ya lugha katika jamii kubwa ya lugha za ki-Bantu.

Baadhi ya wataalamu muhimu wanaoiunga mkono nadharia hii ni Prof. Malcon Guthrie, Dkt. C. Meinholf na Dkt. C. Rohl na Prof. Clement Maganga.

Profesa Malcom Guthrie ni mtaalamu (mwanaisimu) mashuhuri kutoka Chuo Kikuu cha London, Uingereza. Alitumia miaka 20 kuchunguza uhusiano uliopo baina ya lugha za Kibantu zilizoko katika eneo lote ambalo hukaliwa na wabantu. Sehemu hii ni ile ambayo inajulikana kama Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alifanya uchunguzi wa mashina/mizizi (viini) ya maneno 22,000 kutoka lugha 200 za Kibantu. Katika uchunguzi wake alikuta mizizi (mashina) 2,300 imezagaa katika lugha mbalimbali za Kibantu na Kiswahili kikiwemo. Mashina/mizizi 500 yalilingana katika lugha zote 200. Mashina haya yalipatikana katika lugha zote za Kibantu. Mashina haya yalikuwa ya asili moja. Baadhi ya lugha hizo 200 zilizofanyiwa uchunguzi Kiswahili kilionesha kuitikia ulinganifu sawa na Kikongo kwa asilimia arubaini na nne (44%).

Katika kuchunguza ni asilimia ngapi za mashina hayo 500 yaliyomo katika kila lugha, mgawo uliojitokeza ulikuwa kama ifuatavyo:
Kiwemba kizungumzwacho Zambia - 54% Kiluba kizungumzwacho Katanga - 51%
**Kikongo kizungumzwacho Zaire - 44%**
**Kiswahili kizungumzwacho Afrika Mashariki 44%**

| | |
|---|---|
| Kisukuma kizungumzwacho Tanzania | 41% |
| Kiyao kizungumzwacho Tanzania/Msumbiji - | 35% |
| Sotho kizungumzwacho Botswana - | 20% |
| *Kirundi kizungumzwacho Burundi - | 43%* |
| Kinyoro kizungumzwacho Uganda - | 37% |
| Kizulu kizungumzwacho Afrika Kusini - | 29% |

Baada ya kupata matokeo haya, Profesa Malcom Guthrie anaiunga mkono nadharia hii ya kwambaKiswahili ni ki-Bantukwa kudai kwamba: (i) Kiswahili kilikuwepo kabla ya ujio wa wageni;

(ii) Anaonyesha kwamba Kiswahili kina uhusiano mkubwa na lugha za Kibantu;

(iii) Mwisho anasema Kiswahili kilianzia Pwani ya Afrika Mashariki.

### *(i) Ushahidi wa Kiisimu*

*(a) Msamiati*

Matokeo ya utafiti alioufanya kuhusu msamiati wa Kiswahili ulibaini kwamba 60% ya maneno yote yanayoweza kuandikwa na kutamkika katika lugha ya Kiswahili asili yake ni lugha za Kibantu, 30% ni

lugha ya Kiarabu na 10% ni lugha nyingine za kigeni kama vile Kiingereza, Kireno, Kijerumani, Kihindi, Kiajemi, Kifaransa, nk. Kinyume chake ni kwamba msamiati wa Kiswahili na ule wa Kibantu hautofautiani.

**Mfano:**

| **Kiswahili** | **Kindali** | **Kizigua** | **Kijita** | **Kikurya** | **Kindendeule** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mtu | Umundu | Mntu | Omun | Omontu | Mundu |
| Maji | Amashi | Manzi | Amanji | Amanche | Maache |
| Moto | Umulilo | Moto | Omulilo | Omoro | Mwoto |

*(b) Tungo (Sentesi) za Kiswahili*

Miundo ya tungo (sentesi) za maneno ya Kiswahili zinafanana sana na miundo ya tungo za maneno ya ki-Bantu. Sentesi za Kiswahili na za lugha za ki-Bantu zina kiima na kiarifu.

**Mfano:**

| **Lugha za Kibantu** | **Kiima** | **kiarifu** |
|---|---|---|
| Kiswahili | Juma | anakula ugali. |
| Kizigua | Juma | adya ugali. |
| Kisukuma | Juma | alelya bugali |
| Kindali | Juma | akulya ubbugali. |
| Kijita | Juma | kalya ubusima. |
| Kindendeule | Juma | ilye ughale. |

*(c) Ngeli za Majina*

Wanataalamu wanakubaliana kuhusu ngeli za majina kwa mujibu wa:
maumbo ya nomino (umoja na wingi wa majina) pamoja; na upatanisho
wa kisarufi katika sentesi.

Kigezo cha maumbo ya majina:Kigezo hiki hufuata maumbo ya umoja na uwingi katika kuyaainisha majina. Majina yaliyo mengi katika lugha ya Kiswahili na lugha za ki-Bantu hufuata mkondo wa umoja na uwingi. Majina ya lugha ya Kiswahili na lugha za ki-Bantu yaliyo mengi yana maumbo dhahiri ya umoja na uwingi.

**Mfano:**

| Lugha za Kibantu | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | mtu | - | watu |
| | mtoto | - | watoto |
| Kikurya | omanto | - | banto (abanto) |
| | omona | - | bana (abana) |
| Kizigua | mntu | - | bhantu |
| | mwana | - | bhana |
| Kindali | mundu | - | bhandu |
| | mwana | - | bhana |
| Kindendeule | mundu | - | βhandu |
| | mwana | - | βhana |

Kigezo cha upatanisho wa kisarufi katika sentesi: Katika kigezo hiki tunaangalia uhusiano uliopo kati ya kiima (jina na viambishi awali vya nafsi) na vivumishi katika vitenzi vya Kiswahili na ki-Bantu. Vivumishi, majina pamoja na viambishi hivyo vya vitenzi hubadilika kutokana na maumbo ya umoja na uwingi.

**Mfano:**

| Lugha za Kibantu | Umoja | - | Wingi |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | Baba analima | - | Baba wanalima |
| Kindali | Utata akulima | - | Abbatata bbakulima |
| Kikurya | Tata ararema | - | Batata(Tata)bararema |
| Kijita | Tata kalima | - | Batata abalima |
| Kindendeule | Tate ilima | - | Akatate βhilima |

*(d) Vitenzi vya Kiswahili na Kibantu*

Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya vitenzi vya Kiswahili na vile vya lugha zingine za ki-Bantu. Vipengele vinavyothibitisha uhusiano huu ni: Viambishi, mnyumbuliko, pamoja na mwanzo au mwisho wa vitenzi, kama ifuatavyo:

Viambishi:vitenzi vya lugha ya Kiswahili na vya lugha zingine za ki-Bantu hujengwa na mzizi (kiini) pamoja na viambishi vyake vya awali na vya tamati.

**Mfano:**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | - | analima | = | a – na – lim - a |
| Kiikuyu | - | arerema | = | a – re – rem–a |
| Kindali | - | akulima | = | a - ku – lim – a |
| | | | | 1 - 2 - 3 - 4 |

**Sherehe:**

1 - Kiambishi awali kipatanishi cha nafsi.

2 - Kiambishi awali cha njeo (wakati uliopo).

3 - Mzizi/Kiini.

4 - Kiambishi tamati.

Mnyambuliko wa vitenzi:Mnyumbuliko wa vitenzi vya Kiswahili hufanana na ule wa vitenzi vya lugha za ki-Bantu.

**Mfano:**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | - | kucheka | - | kuchekesha | - | kuchekelea. |
| Kindali | - | kuseka | - | kusekasha | - | kusekelela. |
| Kibena | - | kuheka | - | kuhekesha | - | kuhekelea. |
| Kinyamwezi | - | kuseka | - | kusekasha | - | kusekelela. |
| Kikagulu | - | kuseka | - | kusekesha | - | kusekelela |

Mwanzo wa vitenzi:Vitenzi vyote vya Kiswahili na vile vya lugha za ki-Bantu huanza na viambishi ambavyo ni viwakilishi vya nafsi, kama ifuatavyo:

**Mfano:**

| | | |
|---|---|---|
| Kiswahili | - | **N**i-nakwenda |
| Kihaya | - | **N**i-ngenda |
| Kiyao | - | **N-**gwenda |
| Kindendeule | - | **Ni-**yenda |

Mwishilizo wa vitenzi: Vitenzi vya lugha za ki-Bantu na Kiswahili huishia na irabu –a.

**Mfano:**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | kukimbi-a | - | kuwind-a | - | kushuk-a |
| Kindali | kukind-a | - | kubhing-a | - | kukol-a |
| Kisukuma | kupil-a | - | kuhwim-a | - | Kutend-a |
| Kisunza | kwihuk-a | - | kuhig-a | - | kising-a |
| Kindendeule | kuβhutuk-a | - | kuhwim-a | - | kuhuk-a |

Utafiti wa Prof. Maganga kuhusu ushahidi wa ki-Isimu wa kuthibitisha kama Kiswahili ni ki-Bantu au la ungeweza kuelezwa kimuhtasari kwa mifano mingine ifuatayo:

Mfano wa 1:

| **Lugha** | **Sentesi** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | Jongo | anafuga | mbuzi | kuku | na | ng'ombe |
| Kipare | Jongo | erisha | mbuji | nkuku | na | ng'ombe |
| Kindamba | Jongo | kafugha | mene | nguku | na | senga. |
| Kichaga | Jongo | nao he | mburu | nguku | na n' | umbe |
| Kihaya | Jongo | n'afuga | embuzi | enkoko | na | ente |
| Kikaguru | Jongo | kachima | m'ehe | ngu'ku | na | nn'ombe |
| Kindendeule | Jongo | ifuga | mbuhi | nguku | | ng'ombe |

Katika mfano huu inaonekana kwamba mpangilio wa maneno katika sentesi una ufanano kwa sababu katika kila sentesi kuna kiima na kiarifu. Katika kiima kuna nomino, yaani jina la mtenda (Jongo) na katika kiarifu kuna kitendo kinachofanyika na nomino mtendwa. Pia nafasi ya viunganishi ni ile ile kwa lugha zote zilizoonyeshwa katika mfano huu.

Kuna mfano mwingine wa ufanano wa mpangilio huu.

**Mfano wa 2:**

| Lugha | Sentesi |
|---|---|
| Kiswahili | Sitamkuta kesho |
| Kihaya | Timushangemu nyenkya |
| Kisukuma | Natusanga intondo |
| Kinyaturu | Tumuhanga fadyu |
| Kipare | Nesikemkiche yavo |
| Kizigua | Sirambila luvi |

Katika sentensi hizo mpangilio wa maneno una ufanano kwa sababu kila sentensi ina kiima na kiarifu chenye kitenzi na kielezi. Pia kiambishi cha nafsi cha nomino ya mtenda kinajitokeza mwanzoni mwa neno la kwanza la kila sentesi.

**Si**tamkuta; **Ti**mushangemu; **Na**tusanga; **Tu**muhanga; **Ne**sikamkiche; **Si**tambila.

Viambishi hivyo vya nafsi ya mtenda pia vinaonyesha hali ya ukanushi katka kila sentesi na nafasi yake ni ile ile kwa kila sentesi.

Viambishi vya urejeshi navyo vinajitokeza katika kitenzi cha kila sentesi.

Viambishi {m}, {m}, {ti}, {tu} sita**m**kuta, **ti**mushangemu, na**tu**sanga, tumuhanga, nesika**m**kiche, na sita**m**bwila ni vya urejeshi; vinawakilisha nomino mtendwa.

Kwa hivyo, hali hii inadhihirisha kwamba miundo ya sentensi hizi inafanana na vitenzi vyake vina tabia mbalimbali, kama vile:

(i) kubeba viambishi vya nafsi, mtenda na mtendwa,

(ii) kuonyeshga hali ya ukanushi njeo za wakati na kitendo kinachofanyika.

## Mfano wa 3:

| Lugha | Sentesi |
|---|---|
| Kiswahili | Akija mwambie anifuate Akeza |
| Kizigua | umugambe anitimile. |
| Kihaya | Kalaija omugambile ampondele |
| Kisukuma | Ulu nahali anikubije Newaja |
| Kinyaturu | mwele ang'onge. |
| Kipare | Ekiza umti aniratere Anda |
| Kindendeule | ahikite n'nongerera |
| | angobhekeraye |

Katika sentesi hizo inaonekana kwamba sentesi zote zinafanana kimpangilio. Pia maneno yake yanakubali uambishaji, kwa mfano:

(i) Katika maneno ya mwanzo:

akija, akeza. kalaija, akuja, newaja, ekiza, herufi zilizopigiwa vistari ni viambishi vya nafsi vinawakilisha dhana ya mtenda.

(ii) Vivyo hivyo katika maneno:

anifuate, ampondele, anitimile, ang'nge, aniratere, angobhekeraye, viambishi vilivyoko katika viarifu vya sentesi hizo vinawakilisha nafsi za watenda.

(iii) Pia vitenzi vya sentesi hizo vina tabia ya kubeba virejeshi vya nafsi kama ilivyo katika, **m**wa**m**bie, o**mu**gambile, na**ha**li, **m**b**we**le na u**m**ti, vinaonyesha njeo na hali ya uyakinifu- hali inayoonyesha ufanano wa maumbo ya maneno.

(iv) Licha ya kuwa na mpangilio unaofanana na wa lugha nyingine za kibantu, kwa mfano, katika mifano tuliyoiona hapo juu, baadhi ya maneno yanafanana: tazama maneno: kafugha (Kindamba); nafuga (Kihaya); nifuga (Kindendeule); anafuga (Kiswahili).

Pia maneno:

nkuku (Kipare);

nguku (Kindamba);

| | |
|---|---|
| nguku | (Kichaga); |
| enkoko | (Kihaya); |
| ng'uku | (Kikaguru); |
| nguku | (Kindendeule); |
| nguku | (Kindendeule) |

Katika mfano wa 3, maneno yafuatayo yana ufanano:

| | |
|---|---|
| Akeza | (Kizigua); |
| kalaija | (Kihaya); |
| alize | (Kisukuma), |
| newaja | (Kinyaturu); |
| ekiza | (Kipare); |
| anda ahikite, | (Kindendeule); |
| akija, | (Kiswahili.) |

Pia maneno;

| | |
|---|---|
| umugambe | (Kizigua); |
| omugambile | (Kihaya); |
| unongeraye | (Kindendeule); |
| na mwambie | (Kiswahili). |

Ufanano huu wa msamiati, maumbo ya maneno pamoja na wa mpangilio wa maneno katika sentesi, vyote vinathibistisha kwamba lugha ya Kiswahili ni ya kibantu kama zilivyo nyingi nyinginezo.

## Zingatia

Ufanano huu tuliouona wa msamiati, maumbo ya maneno pamoja na wa mpangilio wa maneno katika sentesi, vyote vinathibistisha kwamba lugha ya Kiswahili ni ya ki-Bantu kama zilivyo nyingi nyinginezo.

Kiswahili SI ki-pijini wala SI ki-krioli wala SI ki-Arabu bali NI lugha mojawapo ya Kibantu.

***(ii) Ushahidi wa Kihistoria Kwamba Kiswahili ni Kibantu***

Baada ya kuangalia ushahidi wa kiisimu kuhusu asili ya Kiswahili, katika sehemu hii Maganga (1997) aliendelea kuchambua ushahidi wa Kihistoria unaothibitisha kuwa lugha ya Kiswahili ilizungumzwa katika upwa wa Afrika Mashariki hata kabla ya ujio wa wageni kama vile Waarabu na Wazungu. Ushahidi huu ulitolewa na wageni mbalimbali waliofika hapa Afrika Mashariki. Wote wanathibitisha kuwa lugha ya Kiswahili ilizungumzwa hapa Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wageni.

*(a)* ***Ugunduzi wa Ali-Idris (1100-1166)***

Ugunduzi huu yasemekana ulifanywa huko Sicily yapata mwaka 1100-1166. Kwenye mahakama ya mfalme Roger II. Licha ya kufahamika kuwa Kiswahili, kilipata kuandikwa kabla ya 10BK. Ali-Idris alikuwa wa kwanza kugundua jina la zamani la Zanzibar kuwa ni Unguja. Katika maelezo yake anaandika pia majina kama vile *kikombe, mkono wa tembo, muriani, na kisukari,* ambayo ni ya ndizi mbalimbali zilizokuwa zikipatikana huko.

*(b)* ***Ushahidi wa Marco Polo***

Huyu ni mzungu ambaye alijishughulisha sana na masuala mbalimbali ya kijiografia na alisafiri sehemu nyingi duniani. Marco Polo aliandika hivi:

"Zanzibari ni kisiwa kizuri ambacho kina ukubwa wa mzunguko wa maili 200. Watu wote wanaabudu (Mungu), wana Mfalme na wanatumia lugha yao, na hawalipi kodi (ushuru) kwa mtu." *Safari za Marco Polo* 1958:301

Marco Polo anasemekana aliandika pia kitabu cha jiografia ambacho hakikupata kuchapishwa lakini sehemu zake zimepata kufasiriwa kwa Kirusi na Kifaransa. Mfano mmojawapo ni huu unaofuata:

"Katika visiwa vya Sjawaga vilivyoshughulikiwa katika sura hii, ni kile kisiwa cha Andjaba ambacho mji wake mkuu unaitwa katika lugha ya kwao. Zanguabar/Ungudya, na wakazi wake, japokuwa ni mchanganyiko, kwa sasa wengi wao ni Waislam…chakula chao kikuu kikiwa ndizi. Kuna aina tano ambazo zinajulikana kama kundi, fili, ambazo uzito wake waweza kuwa wakia
12, Omani, Marijani, Sukari...."

Maelezo haya ya Marco Polo yanathibitisha mambo ya msingi kuhusu wakazi wa Pwani ya Afrika ya Mashariki na lugha yao; mintarafu ya dini, chakula na utamaduni wao kwa ujumla.

### *(c) Ushahidi wa Al-Masudi (915 BK)*

Katika moja ya maandiko yake, Al-Masudi anazungumzia juu ya wakazi wa mwambao ambao walijulikana kwa jina la "wazanji". Kwa dhana hii, neno Zanzibar linatokana na Zenzibar yaani "Pwani ya Zenji". Katika maelezo yake Al-Masudi anaonyesha kwamba Wazenji walikuwa "Watawala Wakilimi" ambao waliaminiwa kuwa walitawala kwa nguvu za Mungu. Kuna maelezo kuwa huenda neno "wakilimi" lina maana ya "wafalme". Al-Masudi alisisitiza katika maelezo yake kuwa Wazenji walisema lugha kwa ufasaha na walikuwa na viongozi waliowahutubia kwa lugha yao. Kutokana na neno "zenji" kuna uwezekano kuwa kabla ya majilio ya Waarabu, Kiswahili kiliitwa "Kiazania" au "Kizanji" na wageni waliofika pwani.

### *(d) Ushahidi wa Ki- Historia wa Mji wa Kilwa*

Kimsingi habari zinazoeleza historia ya mji wa Kilwa katika karne ya 10-16BK zinataja majina ya utani kama vile: *mkoma watu, nguo nyingi*, nk. ambayo walipewa Masultani wa kwanza wa Kilwa Ali Ibn Hussein na mwanae Mohamedi Ibn Ali. Kutokana na habari hizi huenda lugha ya Kiswahili ilishaanza kusemwa mnamo karne ya 10 au ya 11 BK. Maelezo ya kihistoria yanaeleza juu ya Sultani aliyeitwa Talt Ibin Al Husaini ambaye alipewa jina la utani "*Hasha Hazifiki"*.

### *(e) Utenzi wa Fumo Liyongo (13 BK) kama Ushahidi*

Shairi la zamani kabisa lililopata kuandikwa la Kiswahili, linalojulikana ni lile la *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Utenzi huu inasemekana uliandikwa karne ya 13BK. Kuweko kwa shairi hili kunadhihirisha kuwako kwa lugha ya Kiswahili kabla ya karne hiyo, na kwa hivyo, huenda Kiswahili kilianza kutumika kabla ya karne ya 10BK. Baadhi ya beti za utenzi wa Fumo Liyongo ni hizi zifuatazo:

Ubeti 6:
Liyongo Kitamkali,
Akabalighi vijali
Akawa mtu wa kweli
Na hiba huongeya.

Ubeti 7:
Kilimo kama mtukufu

Mpana sana mrefu
Majimboni yu maarufu
Watu huja kwangaliya.


Ubeti 10: Sultani pate Bwana
Papo nae akanena
Wagala mumemwona
Liyongo kiwatokeya.

(Kutoka E.A. Swahili Committee 1973)

Lugha hii ndio mfano wa lugha iliyokuwa ikitumika kunako karne ya 13BK. Ni wazi kuwa lugha hiyo ilianza kusemwa mapema kabla ya muda huo. Hoja za kihistoria inaelezea historia ya lugha ya Kiswahili toka karne ya 10BK hadi karne ya 18BK. Kutokana na ushahidi huu ni dhahiri kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni Wabantu wa Afrika ya Mashariki.

## 3.3 Hitimisho

Ama kuhusu suala la mahali hasa ambapo ndipo chimbuko la lugha ya Kiswahili, wataalamu wanahitilafiana. Wengine wanadai kuwa lugha ya Kiswahili inatokana na Kingozi, lugha ya Kaskazini Mashariki mwa Kenya, na wengine wamesema kuwa Kiswahili chimbuko lake ni Kishomvi kilichozungumzwa na watu wa Bagamoyo Mzizima eneo linalojulikana kwa jina la Dar es Salaam hadi Kilwa. Lakini hapana hata mmoja aliyewahi kusema kwamba asili ya Kiswahili ni Moroko ambako neno "Sahil/Sawahil" lipo likiwa na maana ya "pwani/upwa".Kwa mantiki hii, madai kwamba Kiswahili chimbuko lake ni Pwani ya Afrika Mashariki yana mashiko muafaka na yanaweza kuwekwa katika kielelezo kama ifuatavyo:




(Pamoja na ushahidi huu, utafiti zaidi unahitajika kufanywa na wataalam wa mawanda haya)

## Zoezi

1. 'Kiswahili si Kiarabu wala Ki-Pijini'. Jadili hoja hii kwa kutumia ushahidi wa kiisimu
2. "Kiswahili ni lugha kwa dhati yake na wala si Ki-Pijini au KiKrioli". Jadili hoja hii ukithibitisha hoja zako kwa kutumia ushahidi wa kiisimu na kihistoria.
3. "Kiswahili ni Kibantu". Jadili hoja hii ukithibitisha hoja zako kwa hoja za Kiisimu tu.
4. Idadi kubwa ya maneno ya Kiarabu katika Kiswahili ni ushahidi wa kutosha kwamba Kiswahili ni Kiarabu" Jadili hoja hii.
5. "Kiswahili ni Kiarabu kwa jina lake, lakini ni Kibantu kwa tabia yake." Jadili hoja hii

## Marejeo


1. Maganga (1997), OSW 102: *Historia ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
2. Masebo, J. A. Nyangwine, N. (2002), *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili, Kidato cha 5 na 6*. Aroplus Industries Ltd: Dar es Salaam.
3. Nkwera, Fr. F. V. (2003), *Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo*. Creative Prints Ltd: Dar es Salaam.

# MUHADHARA 4

# Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili Nchini Tanzania

## 4.1 Utangulizi

Lugha kusikika imeenea kama kuna ongezeko la watu wanaoitumia lugha yenyewe ndani ya nchi husika. Ongezeko hilo linakomaa kiasi cha kuvuka mipaka ya awali. Leo hii, Kiswahili kinazungumzwa si nchini Tanzania tu, bali pia nje ya mipaka yake: Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi na Msumbiji.

## 4.2 Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili Kabla ya Ukoloni

Kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania kabla ya ukoloni kulikuwa wakati wa biashara ya waafrika wenyewe kwa wenyewe. Biashara hii, ilikuwa imeshamiri sana, si nchini Tanzania tu, bali pia katika upwa wote wa Afrika Mashariki.

Wenyeji wa pwani na wenyeji wa bara, hususan Tanzania, walikuwa na mawasiliano ya muda mrefu kabla ya kufika wageni wa Kiarabu na Kizungu. Kulikuwa na safari za kibiashara baina ya Pwani na Bara zilizokuwa zikifanywa na Waafrika wenyewe. Katika safari hizo, watu wa Bara walikitumia Kiswahili cha pwani na kukieneza sehemu za Bara, sio tu wakati waliporejea makwao kuwataka hali ndugu na majirani zao waliowaacha kwa miaka kadhaa, bali pia wafanyabiashara hao walipokuwa wakifanya biashara zao na Waarabu. Kwa mantiki hiyo, ndio walioanza, bila kukusudia, kuieneza lugha ya Kiswahili kutoka Pwani hadi sehemu za Bara za Tanzania.

### Zingatia

Kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania kabla ya ukoloni kulikuwa wakati biashara ya Waafrika wenyewe kwa wenyewe katika eneo la upwa mzima wa Afrika Mashariki.

## 4.3 Tanzania Wakati wa Ukoloni

Wageni waliohusika walioshirikiana na Wenyeji katika kueneza Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni walikuwa Waarabu, Waajemi, Wareno, Wajerumani na Waingereza. Sababu zilizowafanya waje Afrika Mashariki, husasani Tanzania, ni pamoja na kufanya biashara, kueneza dini na kutawala.

### 4.3.1 Kutokana na Biashara

***(i) Waarabu***

Kwa mujibu wa maelezo ya Nkwera (2003:119) Waarabu walifika Pwani ya Afrika Mashariki karne ya kumi. Walipofika hapa waliwakuta wenyeji wanazungumza Kiswahili, na kutokana na nia ya kueneza biashara yao, Waarabu wanajulikana sana kwa biashara, hususan biashara ya watumwa. Walishirikiana sana na watumwa katika dini, biashara na kuoana.Waarabu hao waliitumia lugha ya Kiswahili kila walipopita kufanya biashara yao. Lugha ilikuwa muhimu sana kwa mawasiliano kwa kila jambo walilofanya kati yao na wenyeji wao, hususan kwa kuwatumia watumwa wao.

Kwa kufanya hivyo, walijikuta wameeneza lugha ya Kiswahili.

Katika kuhakikisha kuwa lugha hii inafundishwa vyema na biashara inaendelea bila tatizo, Waarabu walianzisha vituo maalum kwa ajili ya biashara na wakati huo huo kufundisha dini ya Kiislamu. Vituo vya kibiashara kama vile Tabora na Ujiji vilikuwa na umuhimu mkubwa sana katika kueneza dini ya Kiislamu na Kiswahili hapa nchini.

***(ii) Wajerumani***

Wajerumani walianzisha mashamba makubwa ya mazao ya biashara na wakalazimisha Watanganyika kutoka Bara na Pwani kufanya kazi ya kulima katika mashamba hayo, hususan mashamba ya Mkonge (katani). Kwa kuwa walikuwa watu wa makabila mbalimbali, Kiswahili kilitumika sana katika mawasiliano baina yao. Na wale waliobahatika kurejea nyumbani, walisaidia kukieneza Kiswahili huko kwao.

### 4.3.2 Kutokana na Dini

#### ***(i) Waarabu na Dini ya Ki-Islamu***

Walipofika karne ya 10 waliwakuta wenyeji wakizungumza lugha zao za Kibantu kikiwemo Kiswahili. Waarabu walipofika na dini ya Kiislamu walijikuta wakishirikiana na wenyeji wa upwa huu katika mambo makuu matatu; Dini, biashara na kuoana.

Ili waweze kueneza dini yao vyema, Waarabu walijifunza kwa dhati lugha ya Kiswahili. Kwa vile walijishughulisha pia na biashara, Waarabu waliweza kujumuisha mambo mengi kwa mara moja.

#### ***(ii) Wamishenari na Dini ya Ki-Kristo***

Hawa walifika pwani ya Afrika Mashariki kabla ya utawala wa Wakoloni. Mashirika mbalimbali ya kidini yaliingia Afrika Mashariki katika nyakati tofauti tofauti. Mashirika haya ni "*Roho Mtakatifu*" toka Ufaransa mwaka 1868, *White Fathers* toka Ufaransa mwaka 1878, *Church Missionary Society*

*(CMS)* ambalo liliongozwa na J.C. Krapf kutoka Ujerumani. Shirika hili mwaka 1876 liliandika sarufi ya kwanza ya Kiswahili cha Kimvita katika kitabu kilichoitwa *Outlines of the Elements of Kiswahili Language with Specific Reference to the Kinika Dialect*.

Pia mwaka 1845, Krapf alimpelekea katibu wa CMS orodha pana ya maneno (muhtasari) wa sarufi pamoja na tafsiri ya Injili ya Luka na Yohana ili kuwasaidia Wamishenari wengine ambao walikuwa wakiletwa Afrika ya Mashariki. Mwaka 1905 Misioni ya Magila walitoa kijitabu juu ya historia ya Wasambaa kilichoitwa *Habari za Wakilindi*. Makao makuu ya shirika hili yalikuwa Mombasa.

Shirika la *Universities Mision to Central Afrika* (U.M.C.A) (Uingereza) liliingia mwaka 1875 nchini, UMCA ilijishughulisha sana na kukiweka Kiunguja katika maandishi waka 1870 Askofu Edward Steere alichapisha toleo la kwanza la sarufi ya Kiswahili cha Kiunguja lililoitwa "*A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar*". Pia walichapisha vitabu vya nyimbo na kamusi za Kiswahili na Kiingereza-Kiswahili kazi ya awali ya kuziandaa kamusi hizo ni ya Edward Steere, lakini ilikamilishwa na A. Madan na baadaye kurudiwa na F. Johnson aliyeandaa kamusi mbili *A Standard English-Swahili Dictionary* na *Swahili English Dictionary* ambazo zilitolewa mwaka 1939. UMCA walichapisha pia magazeti ya *Msimulizi* (1888), *Habari za Mwezi* (1876), *Pwani na Bara* (1910).

Kwa ujumla wamisheni walijishughulisha sana na Kiswahili kwa sababu walikihitaji katika shughuli zao za kidini kwa kufanya hivyo walijikuta wanaikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa kufuatana na uongezekaji wa vituo vyao nchini. Baadhi ya vituo hivyo ni Bagamoyo (1868), Magila (1864), Mpwapwa (1876), Ujiji (1877), Masasi (1876), Zanzibar (1860) na Ziwa Nyasa (1881).

### 4.3.3 Kutokana na Utawala

#### *(i) Kutokana na Utawala wa Wajerumani*

Tunafahamishwa na Nkwera (2003:120) kwamba Wajerumani wameitawala Tanganyika kwa miaka thelethini (30) yaani (1885 – 1916) kwa jina la Deutsch Ost Afrika (Afrika ya Mashariki ya Mjerumani).

Wajerumani walipoingia Tanganyika walikuta tayari kuna misingi mizuri ya lugha ya Kiswahili, Wamisheni walikuwa tayari wameandaa mfumo wa elimu na dini uliokuwa unatumia lugha ya Kiswahili. Kutokana na misingi hiyo utawala wa Kijerumani ulipoanzishwa nchini Kiswahili tayari kilikuwa kimeimarika.

Kwa hiyo, Wajerumani walikiona Kiswahili kuwa ni chombo muhimu sana kwa kuwasiliana na wananchi katika mawanda yafuatayo:

(a) Kiswahili kilitumiwa na wamisionari kueneza Injili.

(b) Katika Shule za watoto wadogo (Chekechea), Shule za Misingi na Shule za Kati (Middle Schools), Wamisionari walitumia Kiswahili kufundishia kuandika, kusoma, kuhesabu na kazi mbali mbali za ufundi, k.v.

useremala, uashi na ufyatuaji mataofali.

(c) Kwa upande wa Seriali, Kiswahili kilitumika kuelezea na kuenezea siasa ya Kijerumani na mipango ya Serikali kwa wananchi, na pia kuendeshea shughuli za utawala.

Kwa mantiki hii, Wajerumani walisisitiza sana kwamba Kiswahili kifundishwe mashuleni kote, na Kijerumani kifundishwe katika madarasa ya Elimu ya Watu Wazima. Walilazimisha kila Akida afahamu Kiswahili barabara ili aweze kutumwa na kufanya kazi mahali popote, siyo tu katika sehemu aliyozaliwa na kukulia.

(d) Wajerumani walijenga shule Tabora, Ujiji, Kilimatinde, Kasangu mwaka 1905 na hatimaye Bukoba, Mpwapwa, Iringa, Mwanza, Kilosa, Tukuyu na Moshi. Vyuo vya kufundishia Walimu vilianzishwa huko Tabora na Bukoba.

Kutokana na Wajerumani kusisitiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli za utawala, shule, kortini (mahakama) na hata katika kuwasiliana na wananchi, walisaidia sana kukieneza Kiswahili sehemu mbalimbali za Tanganyika.

***(ii) Kutokana na Utawala wa Waingereza***

Baada ya ujio wa Waingereza Tanganyika, juhudi mbalimbali zilifanywa katika kueneza Kiswahili nchini. Kwanza ilikuwa ni kuteua aina moja tu ya Kiswahili ambayo ingetumika katika nchi zote nne za Afrika Mashariki. Pia uwepo mtindo mmoja wa kukiandika. Hivyo mwaka 1928 mkutano ulifanyika Mombasa na walikubaliana kuwa nchi zote nne zitumie lugha ya aina moja yaani Kiunguja.

Mwaka 1929 Katibu wa halimashauri ya magavana wa Afrika Mashariki aliziandikia serikali nne kuhusu suala la kuanzishwa kamati ya lugha ya serikali zote nne na tarehe 1-1-1930 kukaanzishwa kamati iliyoitwa *InterTerritorial Language (Swahili) Committee* ili ihusike na kusanifisha Kiswahili.

Madhumuni ya kamati hiyo ya lugha ilikuwa kama ifuatayo:

(a) Kuendeleza lugha moja kwa kupata maafikiano kamili katika mamlaka ya Afrika Mashariki.

(b) Kuleta ulinganifu kama itakavyoonekana, wa matumizi ya maneno yaliyoko na maneno mapya kwa kusimamia uchapaji wa makamusi ya mashule na mengineyo.

(c) Kuleta ulinganifu wa sarufi kwa kuchapisha vitabu vya sarufi vilivyoafikiwa.

(d) Kuwatia moyo na kuwasaidia waandishi ambao ni wenyeji wa lugha ya Kiswahili.

(e) Kuandaa vitabu vya Kiswahili vya kiada na vya ziada.

(f) Kusahihisha lugha ya vitabu vya shule na vinginevyo ambavyo vimechapishwa mara masahihisho yanapohitajika.

(g) Kutafsiri kwa Kiswahili vile vitabu vilivyochaguliwa kwa ajili ya kutumiwa shuleni au kwa kusoma kwa ziada au kuvitunga moja kwa moja vitabu hivyo.

(h) Kusoma na kuhakiki vitabu vya Kiswahili vinavyoshughulikiwa na kamati.

(i) Kuwapa waandishi wa vitabu maelezo ya taratibu za kufundishia za wakati uliopo katika nyanja mbalimbali.

(j) Kujibu maswali yoyote kuhusu lugha ya Kiswahili na fasihi yake.

Kamati hii ilitoa makamusi ya *Standard Swahili-English-Swahili Dictionary*. Mwaka 1935 kulianzishwa mashindano ya kuandika insha kwa Kiswahili katika shule za Kiafrika. Mwaka 1939 kukawa na mashindano ya waandishi wa vitabu. Vile vile kamati ilitoa kijarida kilichojulikana kwa jina la *Bulletin of the Inter-Territorial Language (Swahili) Committee*.

***(iii) Kutokana na Vyombo Mbalimbali***

Wakati wa utawala wa Mwingereza vyombo vilivyosaidia sana kueneza Kiswahili ni:

(a) Elimu

Wakati wa Mwingereza Kiswahili kilitumika kufundishia shule za msingi, darasa la kwanza hadi la nne, na kilikuwa somo mojawapo hadi darasa la 12 katika shule za Waafrika.

(b) Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vilivyojishughulisha sana na kukuza na kueneza Kiswahili ni magazeti, radio, nk.

- Magazeti yaliyojishughulisha sana ni *Masimulizi* (1888), *Habari za Mwezi* (1894), *Pwani na Bara* (1910), *Rafiki Yangu* (1890), *Habari za Leo* (1954), *Mwangaza* (1923), *Sauti ya Pwani* (1940), *Kiongozi* (1950), *Mamboleo*, nk.
- Chombo kingine cha habari ni radio Tanganyika ilianza matangazo kwa lugha ya Kiswahili mwaka 1950. Kwanza kama Sauti ya D.S.M. halafu baadaye kama Sauti ya Tanganyika.

(c) Wakati wa Manamba

Utaratibu wa serikali za kikoloni ulikuwa ni kuzitenga sehemu fulani kwa ajili ya vibarua wa kufanya kazi katika mashamba hayo, mawasiliano yote yalifanywa kwa Kiswahili, na kwa njia hii kulikuwa na kukua na kuenea kwa Kiswahili kwa urahisi zaidi hapa nchini.

(d) Suala la Jeshi (KAR)

Wanajeshi waliopigana katika vita mbalimbali walikuwa na nafasi ya kusafiri sehemu mbalimbali na kwa kuwa lugha yao ya mawasiliano ilikuwa ni Kiswahili, lugha hiyo iliweza kuenea kwa urahisi nchini.

(e) Kampeni za Kisiasa

Baada ya vita ya pili ya dunia, mataifa mengi yaliyokuwa yanatawaliwa yalianza kudai uhuru wao, Afrika Mashariki nayo haikuwa nyuma.

Ingawa kulikuwa na makabila mengi yenye lugha tofauti, jambo lililowauganisha ilikuwa ni lugha ya Kiswahili, ambayo iliweza kueleweka na watu wengi. Lugha ya Kiswahili iliweza kuunganisha watu wa makabila tofauti katika mikutano mbalimbali iliyokuwa ikifanywa na vyama vya siasa nchini wakati huo.

## 4.4 Hitimisho

Lugha ya Kiswahili ilisaidia sana katika kueneza siasa za TANU. Kiswahili ambacho leo ni lugha ya Taifa, kinatokana na lugha za kibantu. Kiswahili kinazungumzwa karibu na jamii zote katika Tanzania. Hivyo ilikuwa ni rahisi kuenea kwa TANU kwa watu wengi pasipo haja ya mkalimani. Hivyo mikutano mbalimbali ya kampeni za kisiasa ilisaidia sana kueneza Kiswahili nchini kwani mikutano mingi iliendeshwa kwa Kiswahili.

### Zoezi

Eleza njia zilizotumika kueneza lugha ya Kiswahili Tanzania Bara kati ya karne ya 10 AD. Na kabla ya mwaka 1900.

### Marejeo

1. Masebo, J. A. Nyangwine, N. (2002), *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili, Kidato cha 5 na 6*. Aroplus Industries Ltd: Dar es Salaam.

# MUHADHARA 5

# Fonetiki

## 5.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu tutafafanua dhana ya fonetiki. Tutayapitia na kuyahakiki maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana hiyo na tutatoa maana ya jumla ya fonetiki.

## 5.2 Maana Ya Fonetiki

Hyman (1975) kama alivyonukuliwa na Method (2009) anaeleza kuwa fonetiki ni taaluma ambayo hususani huchunguza sauti ambazo hutumiwa na wanadamu wakati wanapowasiliana kwa kutumia lugha. Anaendelea kueleza kuwa uchunguzi wa kifonetiki huwa hauhusishwi na lugha yoyote maalumu na kutokana na hali hiyo kipashio cha msingi cha fonetiki ni foni. Hyman anaendelea kwa kueleza kuwa foni ni kipande kidogo kabisa cha sauti kisichohusishwa na lugha yoyote.

Naye Massamba na wenzake (2004) wanaeleza kuwa fonetiki ni tawi ambalo hujishughulisha na uchambuzi wa taratibu zote zinazohusiana na utoaji, utamkaji, usafirishaji, usikiaji na ufasili wa sauti za lugha za binadamu kwa ujumla. Kinachozingatiwa hapa ni kuchunguza maumbo mbalimbali ya sauti zinazoweza kutolewa na ala sauti, namna ambavyo maumbo hayo yanavyoweza kutolewa, yanavyoweza kumfikia msikilizaji (yaani yanavyosikika) na yanavyofasiliwa na ubongo; bila kujali sauti hizo zinatumika katika lugha gani.

Kwa kusikiliza sauti wanafonetiki wanaweza kuzipanga sauti hizo katika makundi na kuzitolea sifa zinazotofautisha sauti moja na nyingine.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma huhadhara huu utaweza:

- Kueleza kwa ufasaha maana ya fonetiki.
- Kufafanua matawi ya fonetiki
- Kueleza makundi makuu ya sauti za lugha yaani: irabu na konsonanti.
- Kufafanua kwa ufasaha sifa bainifu za irabu na konsonanti.

## 5.3 Matawi ya Fonetiki

Fonetiki ina matawi kadhaa kama ifuatavyo:

i Fonetiki Matamshi

ii FonetikiAkustika

iii Fonetiki Masikilizi/Masikizi

iv Fonetiki Tiba matamshi.

Fonetiki Matamshi. Massamba na wenzake (2004) wanaeleza fonetiki matamshi kuwa ni tawi linalojishughulisha na jinsi sauti mbalimbali zinavyotamkwa kwa kutumia zile ala sauti. Kinachoangaliwa hapa ni jinsi ya utamkaji wa sauti hizo (kama sauti ni kikwamizi), mahali pa matamshi (kama sauti hizo ni midomo) na hali ya mkondo hewa (kama ni ghuna au si ghuna).

Fonetiki Akustika. Tawi hili la fonetiki huchunguza jinsi mawimbi sauti yanavyosafiri kutoka katika kinywa cha msemaji hadi kufikia sikio la msikilizaji.

Fonetiki Masikizi. Ni tawi la fonetiki linaloshughulikia jinsi mawimbi sauti yanavyoingia katika sikio la msikilizaji na kutafsiriwa na ubongo wake hata kupata maana. Method (2009).

Fonetiki Tiba matamshi. Tawi hili kama linavyoitwa na Massamba (2004) pia linaitwa na Mgullu (1999) kuwa ni fonetiki majaribio na linajishughulisha na matatizo yanayoambatana na usemaji na jinsi ya kuyatatua. Tawi hili ni jipya zaidi na limeibuka hivi karibuni.

Kwa minajili ya kozi hii tutajikita zaidi kwenye fonetiki matamshi.

Fonetiki Matamshi

Fonetiki matamshi kama ilivyoelezewa hapo awali kuwa ni tawi linaloshughulikia jinsi sauti zinavyotolewa na ala sauti. Swali la msingi ala sauti ni nini? Na ni zipi?

Ala sauti ni viungo vya mwili wa binadamu vinavyotumika kumwezesha binadamu kutoa sauti. Viungo hivi pia vina kazi nyingine za kibiolojia. Kwa mfano:

- Mapafu – hupeleka hewa kwenye damu katika koromeo
- Nyuzi sauti –hufunga koo wakati wa kula hivyo huzuia chakula kisipite kwenye viribahewa.
- Ulimi – kuonja
- Meno – kutafuna

Viungo vifuatavyo ni ala za sauti zinazoshiriki utoaji wa sauti: meno, ufizi, kaa kaa gumu, kaa kaa laini, kidaka tonge/uvula, pua, ncha ya ulimi, pembeni, nyuma, shina la ulimi, koromeo, chemba cha pua, chemba cha kinywa, nyuzi sauti.

Makundi ya ala sauti.

i Ala Sogezi. Hizi ni vile viungo vya binadamu ambavyo hujisogezasogeza wakati wa utamkaji wa sauti. Ala hizi ni pamoja na midomo, ulimi n.k

ii Ala Tuli. Ala hizi huwa hazisogei wakati wa utamkaji. Zipo kinyume na ala sogezi. Mfano wa ala tuli ni kaa kaa gumu, kaa kaa laini n.k

**Meno**. Ni ala tuli ambayo hutumika kutamka sauti kadhaa za lugha. Hewa huweza kuzuiwa kati ya meno na kuachiwa na hivyo kutoa sauti Fulani. Kwa mfano: f, v, /s/, /z/ n.k

**Midomo.** Kwa kawaida binadamu ana midomo miwili. Mdomo wa juu na mdomo wa chini, na midomo hii ni ala sogezi. Ina jukumu kubwa katika utamkaji. Baadhi ya sauti za midomo ni /b/, /p/, /m/ n.k

**Ufizi.** Ala tuli.Hizi ni ala ambazo zinashikilia meno ya juu nay a chini. Baadhi ya sauti za ufizi ni /n/, /t/, /d/, /s/ n.k

**Kaa kaa gumu.** Ala sauti hii hupakana na ufizi. Mfano wa sauti za kaa kaa gumu ni: ch, y n.k

**Kaa kaa laini.** Sehemu hii huanza mara baada ya kaa kaa gumu. Mfano wa sauti za kaa kaa laini ni:k, g, ny, kh, ng' n.k

**Ulimi.** Ni ala sauti muhimu sana kwani husaidia utamkwaji wa sauti nyingi sana. Irabu zote hutegemea ala hii katika utamkaji wake. Mfano wa irabu ni: a, e, i, o, u. ulimi umegawanyika katika sehemu kuu tatu.

a. Ncha ya ulimi. Hutamka vitamkwa mbalimbali kama vile n, t, d.
b. Sehemu ya kati. Hutamka vitamkwa kama ch, j.
c. Sehemu ya nyuma. Huenda juu au chini, mbele au nyuma katika kutamka sauti mbalimbali. Kusogea huko kwa sehemu ya nyuma ya ulimi huathiri umbo la chemba cha kinywa.

**Nyuzi sauti.**Ni misuli miwili yenye uwezo wa kunyambulishwa ambayo huwepo kwenye koromeo. Nyuzi sauti zina mchango mkubwa sana katika katika utoaji wa sauti. Nyuzi sauti zinapotikiswa hutoa mghuno na hivyo hutoa sauti ziitwazo ghuna, kwa mfano b, g, d n.k. Nyuzi sauti zisipotikiswa hazitoi mghuno hivyo hutoa sauti ziitwazo si ghuna. Mfano: p, k, t n.k

**Chemba ya pua.** Hii hutoa sauti ziitwazo nazali. Wakati wa utamkaji wa sauti hizo hewa hupitia katika chemba ya pua. Mfano wa nazali m, n, ny n.k

**Glota.** Ni uwazi uliopo kati ya nyuzi sauti. Uwazi huu hubadilikabadilika kutegemeana na kinachotamkwa. Sauti ya glota ni h.

## 5.4 Uainishaji wa Sauti

Makundi makuu ya sauti za lugha ni: irabu na konsonanti.

### 5.4.1 Irabu


Ni sauti za lugha ambazo wakati wa kutamkwa hewa haizuiwi wala kuzibwa mahali popote, hewa hupita kwa urahisi bila kizuizi chochote.

Tofauti kati ya irabu na konsonanti ipo katika utamkaji.

Irabu huainishwa kwa kutumia vigezo vitatu: mahali pa kutamkia, mwinuko wa ulimi na hali ya mdomo.

**Mahali pa kutamkia**

Irabu huweza kutamkwa katika sehemu tatu za ulimi: sehemu ya mbele ya ulimi, sehemu ya kati ya ulimi na sehemu ya nyuma ya ulimi.



Mfano:

- [i],[e]- Hutamkiwa sehemu ya mbele ya ulimi hivyo huitwa - **Irabu za mbele**
- [u],[o]- Hutamkiwa  sehemu ya nyuma ya ulimi hivyo huitwa – **Irabu za nyuma**
- **[a] –** Hutamkiwa sehemu ya kati ya ulimi hivyo huitwa –**Irabu ya kati**

**Mwinuko wa ulimi**


Wakati wa utamkaji wa irabu ulimi huwa juu, kati au chini. Ulimi huwa umenyanyuka au umeshuka.

Irabu zimegawiwa katika makundi matatu (3). Nayo ni haya yafuatayo :

i [i] na [u]- Ulimi umenyanyuka juu.

ii [e] na [o]- Ulimi umeinuka mpaka katikati.

iii [a]- Ulimi ukiwa chini kabisa.




**Hali ya mdomo**

Wakati wa utamkaji mdomo unaweza kuwa umeviringwa au haukuviringwa. Tunapata irabu viringo na irabu si viringo. Irabu viringo ni [o] na [u]. irabu si viringo ni [i], [e] na [a].

Uainishaji wa Irabu

[i] - irabu ya mbele, juu, si viringo.

[e] – irabu ya mbele kati, si viringo.

[a] – irabu ya kati, chini, si viringo.

[u] – irabu ya nyuma, juu, viringo

[o] – irabu ya nyuma, kati, viringo.

### 5.4.2 Konsonanti

Konsonanti ni aina ya sauti katika lugha ambazo wakati wa utamkaji wake mkondo wa hewa huzuiwa katika sehemu mbalimbali kinywani. Wakati mwingine hewa huzuiwa kabisa, wakati mwingine hewa huzuiwa kiasi mahali fulani baada ya kupita kongomeo. Mfano wa konsonanti ni [p], [g], [b] na [h].
Ili uweze kuzitambua konsonanti ni lazima ufahamu sifa bainifu za konsonanti. Zifuatazo ni sifa maalumu za utambuzi wa konsonanti :

- i Namna ya utamkaji
- ii Mahali pa kutamkia
- iii Ghuna au si ghuna

**Namna ya Utamkaji**

Kigezo cha kwanza cha kuainishia konsonanti ni namna ya utamkaji. Katika namna ya utamkaji tunarejelea jinsi ambavyo mkondo hewa unavyozuiwa katika sehemu mbalimbali za bomba la sauti wakati wa kutoa sauti za lugha.

Kama tulivyotaja hapo awali mkondohewa unaotoka mapafuni huweza kuzuiwa na vizingiti vya ala sauti kwa namna tatu kimsingi :

a) Mkondohewa unaweza kuzuiwa kabisa.

b) Mkondohewa unaweza kuruhusiwa upite katika mwanya mdogo kwa shida.

c) Mkondohewa unaweza kuruhusiwa upite bila kuzuiwa.

Kwa kutumia hali hizi za mkondohewa, konsonanti huainishwa katika makundi yafuatayo :

i. Vipasuo/ Vizuiwa

ii. Vipasuo – kwamiza

iii. Vikwamizi/Vikwamizwa

iv. Nazali

v. Vitambaza

vi. Vimadende

vii.

**I. Vipasuo/Vizuiwa**

Ni konsonanti ambazo wakati wa utamkaji wake mkondohewa kutoka mapafuni hubanwa kabisa wakati wa kutamkiwa kisha huachiwa ghafla.

Sauti hizi zimeitwa vipasuo kutokana na kuachiwa ghafla kwa mkondohewa. Sauti zitokeazo zina mlio wa kupasua. Ifuatayo ni mifano ya vipasuo :

- Vipasuo vya midomoni: [ p ], [ b ], [ m ]
- Vipasuo vya midomo-meno: [ɱ] (Hii si fonimu ya Kiswahili; hudhihirika kimatamshi tu.)
- Vipasuo vya ufizi: [ t ], [ d ], [ n ]
- Vipasuo vya kaakaa gumu: [ ɟ ], [ ɲ ]
- Vipasuo vya kaakaa laini: [ k ], [ g ], [ŋ]

**Habwe J na Karanja P (2004 )**

**II. Vipasuo – kwamiza**

Ni konsonanti ambazo wakati wa utamkaji wake ala sauti huwa zimefungwa kabisa na kasha kuachiliwa hewa ipite ghafla kwa mlipuko lakini ala sauti haziachani kabisa; huacha mwanya mdogo na kuruhusu mkondo hewa kupita kwa shida kati yao na kusababisha sauti inayotoka kuwa mkwaruzo. Mifano ya vipasuo- kwamiza ni:

- Vipasuo-kwaruzo vya ufizi: [ts], [dz]
- Vipasuo-kwaruzo vya kaakaa gumu: [ tʃ ], [ dʒ ]

**Habwe J na Karanja P (2004 )**

**III. Vikwamizi**

Sauti hizi hutamkwa wakati ala sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo. Sauti za vikwamizi zaweza kutamkwa mahali popote kwenye bomba la sauti.

- Vikwaruzo vya midomoni: [β ], [ Φ ]
- Vikwaruzo vya midomo-meno: [ f ], [ v ]
- Vikwaruzo vya menoni: [ θ ], [ð]
- Vikwaruzo vya ufizi: [ s ], [ z ]
- Vikwaruzo vya kaakaa gumu: [ ʃ ], [ ʒ ]
- Vikwaruzo vya kaakaa laini: [ x ], [ ɣ ]
- Vikwaruzo vya kilimi: [ʁ]
- Vikwaruzo vya koo: [ħ]
- Vikwaruzo vya kongomeoni: [ h ]

**Habwe J na Karanja P (2004 )**

**IV. Nazali**

Ni sauti ambazo hutamkwa kwa kuruhusu mkondo hewa kupitia kwenye chemba cha pua. Mifano ya sauti nazali ni:

- Nazali yam domo: [m].
- Nazali ya ufizi: [n].

**V. Vitambaza**

Ni sauti ambazo wakati wa kutamka ulimi hutandazwa na kuruhusu hewa ipite pembeni ya ulimi bila mkwaruzo mkubwa sana. Mfano wa kitambaza ni [l].

### VI. Vimadende

Ni sauti ambayo wakati wa utamkaji wa sauti ncha ya ulimi inakuwa imegusa ufizi lakini kutokana na nguvu ya mkondo hewa inayopita kati ya ulimi na ufizi, ncha ya ulimi hupigapiga kwa haraka haraka kwenye ufizi. Mfano wa kimadende ni [r].

### Mahali pa kutamkia

Kigezo cha pili cha kuainisha konsonanti ni mahali pa kutamkia. Wakati wa utamkaji ala sogezi na ala tuli hukaribiana na kugusana. Mara nyingi huwa kuna ala sogezi ambayo husogea kuelekea kwa ala tuli ingawa kuna hali ambayo ala sogezi mbili huhusika. Kwa mfano mdomo wa juu unahusiana na wa chini katika kutoa sauti.

Konsonanti hugawanywa katika makundi makuu saba.

i. Midomo
ii. Midomo na meno
iii. Meno
iv. Ufizi
v. Kaakaa gumu
vi. Kaakaa laini
vii. Koromeo

### Midomo

Konsonanti zinazotamkwa kwenye midomo huhusisha utatizwaji wa hewa katika midomo yote miwili. Mdomo wa chini huelekeana na ule wa juu. Hapa midomo yote miwili huwa ni ala sogezi. Sauti zitolewazo kwenye midomo ni [m], [p] na [b].

### Midomo na Meno

Sauti zitamkiwazo hapa huhusisha mdomo wa chini na meno ya juu. Hapa mdomo wa chini huwa ala sogezi na husogea kuelekea meno ya ju ambayo ni ala tuli. Mfano wa sauti hizo ni [f], [v].

**Meno**

Sauti za meno hutamkwa kwa ncha ya ulimi ikiwekwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Mfano wa sauti hizo ni:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| [ θ ] | [θawabu] | thawabu | Kiswahili | Malipo mema kutoka kwaMungu |
| [ð] | [ðahabu ] | dhahabu | Kiswahili | Aina ya madini yenye thamani kubwa |

**Habwe J na Karanja P (2004 )**

**Ufizi**

Sauti za ufizi huhusisha bapa la ulimi kama ala sogezi na mwinuko wa ufizi ulio nyum`a ya meno ya juu ukiwa ndio ala tuli. Mifano ya sauti za ufizi ni: [t], [d], [n], [r], [l], [s] na [z].

**Kaakaa gumu**

Sauti za hapa hutamkwa kwa kuhusisha bapa la ulimi na kaakaa gumu. Mfano wa sauti hizo ni :

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| [ ʃ ] | [ʃɛmɛɟi] | <shemeji> | Kiswahili | Ndugu ya mume au mke |
| [ ʒ ] | [meʒə] | <measure> | Kiingereza | Pima |
| [ dʒ ] | [ dʒin ] | <gin> | Kiingereza | Mvinyo |
| [ tʃ ] | [tʃakula] | <chakula> | Kiswahili | Kitu cha kula |
| [ ɟ ] | [ɟaɱvi] | <jamvi> | Kiswahili | Aina ya mkeka |
| [ j ] | [ jakini ] | <yakini> | Kiswahili | Hakika |
| [ ɲ ] | [ ɲaɲa ] | <nyanya> | Kiswahili | Mama mzaa baba au mama |

**Habwe J na Karanja P (2004 )**

**Kaakaa Laini**

Sauti za hapa hutamkwa kwa kutumia sehemu ya nyuma ya ulimi ambayo hugusana au kukaribiana na kaakaa laini. Mfano wa sauti hizo ni :

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| [ ŋ ] | [ŋɔmbɛ] | ng'ombe | Kiswahili | Aina ya mnyama afugwaye |
| [ x ] | [iŋgɔxɔ] | ingokho | Kiluhya | Kuku . |
| [ ɣ ] | [ɣala] | ghala | Kiswahili | Jengo la kuhifadhia bidhaa |
| [w] | [wɛka] | weka | Kiswahili | Tia kitu juu ya mahali |

*Fahamu:* **[w]**, kama tulivyosema awali, hutamkiwa mahala pawili: katika midomo na kaakaa laini.

**Habwe J na Karanja P (2004 )**

**Koromeo**

Sauti ya koromeo hutamkiwa kwenye tundu la glota. Mfano wa sauti hiyo ni [h].

# Muhimu

Kuna sauti ambazo siyo konsonanti wa irabu huitwa viyeyusho/ nusu irabu. Mfano [w] na [y].

**[w]**

- Mahali pa kutamkia ni kwenye mdomo
- Namna ya utamkaji mdomo huvirigwa wakati wa utamkaji wake.

**[y]**

- Mahali pa kutamkia ni kwenye kaakaa gumu
- Namna ya utamkaji, kutandaza midomo na sehemu ya kati ya ulimi hukaribiana na kaakaa gumu.

**Jedwali la namna ya utamkaji na mahali pa kutumika**

**Jedwali la IPA la Konsonanti**
**(kutoka IPA 1989)***

| | Midomo | Midomo-meno | Meno | Ufizi | Kaakaa-gumu | Kaakaa laini | Kilimi | Koo | Kongomeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipasuo | p b | | | t d | ɟ | k g | | | |
| Nasali | m | ɱ | | n | ɲ | ŋ | | | |
| Kikwaruzo | β | f v | θ ð | s z | ʃ ʒ | ʁ | ħ | | h |
| Kipasuo -kwaruzo | | | | ts dz | tʃ dʒ | | | | |
| Kimadende | | | | r | | | | | |
| Kitambaza | | l | | | | | | | |
| Nusuvokali | w | | | | j | w | | | |

*Sauti ya kulia katika kila kisanduku ni ya kandamsepetuko ilhali ya kushoto ni ya kandatuli.
*Sauti zilizoorodheshwa hapa ni zile zilizorejelewa katika kazi hii.

**Ghuna au si ghuna**

Sauti ghuna ni sauti ambazo wakati wa utamkaji wake nyuzi sauti hurindima au kutetema. Sauti ghuna pia huitwa sauti za *kandamsepetuko*.

Sauti ambazo si ghuna hazina mrindimo wa nyuzi sauti wakati wa utamkaji wake. Sauti si ghuna pia huitwa *sauti za kandatuli au sauti hafifu*. Mifano ya sauti ghuna ni : [ b, d, g, v, dh, z] na nazali. Mfano wa sauti si ghuna : [p, t, k, f, s]

## Zoezi

1. Zitaje alasogezi (articulators) zilizomo katika bomba la sauti la mwanadamu.
2. Eleza tofauti kati ya matamshi ya irabu [i] na irabu [u] na nusu-irabu [w].
3. Eleza mahali pa kutamkia, namna ya kutamka na ughuna wa sauti zifuatazo:
    a) [p] na [b]
    b) [m] na [n]
    c) [w] na [y]
    d) [v] na [s]
4. Eleza tofauti baina ya irabu na konsonanti.
5. Kutokana na neno tusihangaishwe, zibainishe:
    a) irabu zilizotumika katika kuliunda neno hili.
    b) Konsonanti zilizotumika katika kuliunda neno hili.

## Marejeo


1. Batibo, H. (1981), *Tuutazameje Mfungamano: King'ong'o-Konsonanti Katika Kiswahil.* TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
2. Habwe J na Karanja P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers : Nairobi.
3. Maganga, C., (1979), *Jinsi ya Kufundisha Matamshi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wageni.* TAKILUKI: Zanzibar.
4. Ibid (1992), *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu, Idara ya Kiswahili.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
5. Mdee, J. S. (1986), *Kiswahili: Muundo Na MatumiziYake*, Intercontinental Publishers: Nairobi.
6. Mgullu, Richard, S. (1999), *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia Na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers: Nairrobi.
7. TUKI (1990), *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

# MUHADHARA 6
# Fonolojia ya Kiswahili

## 6.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu tutajadili fonolojia ya Kiswahili. Vile vile tutachambua kwa kina tofauti na uhusiano uliopo baina ya fonetiki na fonolojia. Vile vile tutaelezea fonimu, sifa za fonimu, alofoni na miundo ya silabi za Kiswahili.

## Madhumuni ya Muhadhara

Ukimaliza kusoma muhadhara huu utaweza :

- Kutofautisha kwa ufasaha fonetiki na fonolojia.
- Kueleza fonimu ni nini na sifa zake ni zipi
- Kujua mbinu za kutambua fonimu
- Kueleza miundo mbalimbali ya silabi za Kiswahili.

## 6.2 Dhana ya Fonolojia

Fonolojia ni taaluma inayotafiti ili kujua jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi katika lugha husika kama chombo cha mawasiliano katika jamii husika. Ili tujue jinsi sauti ya lugha inavyofanya kazi kuwasilisha ujumbe kwa wazungumzaji wa jamii husika, lazima tuzijue sifa bainifu za kifonetiki zinazojitokeza wakati sauti hizo za lugha husika zinapotamkwa katika lugha husika. Kwa maana nyingine, sifa-bainifu za kifonetiki ndizo zinasababisha kuwako kwa sifa bainifu za kifonolojia. Kipashio cha chini kabisa cha fonolojia huitwa fonimu. Alama ya fonimu huandikwa katikati ya mistari ya aina hii: / /.

Ingawa lugha mbili au zaidi zinaweza kutumia sauti zile zile, utaratibu wa kuzipanga sauti hizo katika kuumba maneno huweza kutofautiana. Maelezo haya  yana maana ya kwamba kila lugha ina utaratibu wake wa mpangilio wa sauti ambao unatumika katika kuunda  ama silabi, mofu, neno au sentensi itakayotamkwa; na kila *sauti* inayotamkwa huandikwa katikati ya mistari ya aina hii:**[ ].**

## 6.3 Tofauti kati ya Fonetiki na Fonolojia

Fonetiki na Fonolojia ni matawi mawili ya isimu yaliyo jirani sana na wakati wote matawi haya hutegemeana na kukamilishana.

Matawi haya mawili yanachunguza kitu kimoja ambacho ni **sauti za lugha.**

Hata hivyo ingawa taaluma hizi huchunguza sauti za lugha lakini fonetiki huchunguza sauti bila kuzingatia mfumo ambamo sauti hizo hutumika, huchunguza sauti kwa ujumla *lakini* fonolojia huchunguza sauti zilizo katika mfumo mmoja na lugha mahsusi.

Taaluma ya Fonetiki ni moja tu lakini fonolojia ni nyingi kama ilivyo idadi ya lugha duniani. Kuna fonolojia y alugha mbalimbali kama vile fonolojia ya Kiswahili, fonolojia ya Kiha,fonolojia ya Kiingereza. Ina maana kila lugha ina fonolojia yake ambayo ni tofauti na lugha nyingine.

Wanafonetiki wamekusanya sauti nyingi kutoka lugha mbalimbali duniani. Fonolojia ya lugha fulani hutumia sehemu ndogo tu ya lugha zilizokusanywa.

Fonetiki ni seti isiyo na kikomo lakini fonolojia ni seti yenye kikomo. Inaaminika kuwa lugha nyingi duniani hutumia wastani wa fonimu kati ya 20 na 40 tu. Kiswahili kina fonimu 30 tu.

Katika kiwango cha fonetiki sauti zote huorodheshwa na kutolewa ufafanuzi makini ambao huonesha tofauti zote za kifonetiki katika foni. Ufafanuzi wa kifonolojia huzionesha zile sifa bainifu katika lugha inayoshughulikiwa. Yaani sifa zile ambazo si bainifu si lazima zitumike kubainisha fonimu za lugha hiyo.

Kipashio cha ufafanuzi wa kifonetiki ni foni ambacho ni kipande kidogo kabisa cha sauti ambacho hakihusishwi na lugha yoyote. Katika ufafanuzi wa kifonolojia kipashio cha ufafanuzi ni fonimu.

Uchambuzi wa kifonetiki hauzingatii mfumo maalumu wa lugha lakini uchambuzi wa kifonolojia huzingatia mfumo maalumu wenye taratibu maalum.

Katika sifa za kiarudhi, fonetiki huzibainisha na kuzielezea sifa hizo kama zinavyotokea katika lugha mbalimbali. Wakati fonolojia hushughulikia sifa za kiarudhi ambazo ni bainifu katika lugha ile na kuziacha zile sifa ambazo si bainifu katika lugha inayochunguzwa.

**Fonetiki na fonolojia hutegemeana na kukamilishana.**

Uchambuzi wa kifonetiki husaidia uchambuzi wa kifonolojia na uchambuzi wa kifonolojia husaidia uchambuzi wa kifonetiki.

Fonetiki ni msingi imara ambao husaidia uchambuzi wa kifonolojia. Mtu asipokuwa na ujuzi wa fonetiki atapata shida kufanya uchambuzi wa kifonolojia.

Fonetiki huzipata foni zote kutoka lugha mbalimbali yaani fonolojia za lugha mbalimbali. Kama kusingekuwa na fonolojia za lugha mbalimbali wanafonetiki wasingepata cha kuchunguza.

Hivyo uchunguzi wa kifonolojia huwa nyenzo ya uchunguzi wa kifonetiki.

## 6.4 Dhana ya Fonimu

Kama tulivyoona kuwa jukumu mojawapo la fonolojia ni kutambua na kuorodhesha fonimu za lugha mahsusi. Njia kuu ya kutambulisha fonimu ni kutumia jozi mlinganuofinyu. Jozi mlinganuofinyu ni utaratibu unaohusu kulinganisha maneno mawili yenye idadi sawa ya sauti lakini yenye tofauti ya neno moja tu kwa mtazamo wa neno moja katika jozi inayohusika. Tuangalie mifano katika lugha ya Kiswahili

Ona basi, katika jozi hizi za mlinganuo finyu, eti kwa sababu tu ya kwamba kila mojawapo ya jozi hizi hutofautiana ki-matamshi kwa sauti moja tu, basi tunapata maneno yenye maana tafauti. Kwa sababu hii, sauti kama hii huitwa kipashio cha chini kabisa cha lugha ambacho kina uwezo wa kubadilisha maana ya neno, lakini chenyewe kikiwa peke yake hakileti maana. Na ndicho hichi hichi kipashio kiitwacho fonimu, (Nchimbi, 1979).

### 6.4.1 Sifa za Fonimu

Fonimu zina sifa za jumla zifuatazo:

1. Kila fonimu inayo sifa zake za kifonetiki zinazoweza kuelezwa ili kufafanua fonimu.
2. Kila fonimu ina sifa zake za kifonolojia ambazo huonesha uamilifu wa fonimu hiyo katika lugha mahsusi.
3. Watumiaji wa lugha Fulani huzielewa sifa zote za fonimu za lugha yao ikiwa ni sehemu ya umilisi wa lugha hiyo.
4. Kila fonimu hushiriki kujenga na kutofautisha maana katika maneno. Fonimu moja peke yake haina maana yaani si kiashiria cha kiashiriwa chochote. Ikisimama peke yake sio fonimu.ukibadili fonimu katika neon maana ya neon hilo litabadilika. Ukiongeza fonimu katika neno maana ya neno hilo itabadilika au itapotea. Ukipangua mpangilio wa fonimu katika neno maana ya neno hubadilika au hupotea kabisa.
5. Kila lugha ina fonimu zake na fonimu za lugha tofauti hazifanani katika uamilifu wake.

### 6.4.2 Alofoni: Dhana na Mifano ya Alofoni

Alofoni ni sauti mojawapo miongoni mwa sauti kadhaa zinazowakilisha fonimu moja.

Alofoni ni sura au maumbo mbalimbali ya fonimu moja yanayotokea katika mazingira tofauti. Fonimu za lugha moja huweza kupata sura tofauti tofauti kulingana na mazingira ambamo hutokea. Ina maana kuwa fonimu inaweza kubadilika na kuchukua umbo moja kutokana na kutokea kwake katika mazingira na pia inaweza kubadilika na kuchukua umbo jingine kutokana na kutokea kwake katika mazingira mengine tofauti.

Wataalamu wanatofautiana kutokana na uwepo wa alofoni katika Kiswahili. Wengine wanasema kuna alofoni mfano Massamba na wengine wanasema hakuna alofoni mfano Mgullu.

Mfano 1: Kiti kirefu

Kiti cheupe

Cheupe imetokana na Ki-eupe

Fonimu /k/ inapotanguliwa na irabu /i/ na ikiwa katika mpaka wa mofimu na kufuatiwa na irabu /e/ athari yake huleta ch /t § /. Hivyo /t §  / ni alofoni ya fonimu /k/.

2. Baibui

Buibui

Hii sio alofoni.

3. Ulimi mrefu

   Ndimi ndefu

   n + limi      n+refu

Fonimu /l/ inapotanguliwa na nazali /n/ hubadilika na kuwa fonimu /d/.

### 6.4.3 Mbinu za Kutambua Fonimu

Kuna njia mbalimbali zinazoweza kutumika kuzibainisha fonimu za lugha. Njia hizo ni :

1. Kufanana kifonetiki
2. Jozi za mlingauo finyu
3. Mgawanyo wa kiutoano
4. Mpishano huru

**Kufanana kifonetiki**

Sauti zinazofanana kifonetiki ni sauti zilizo na sifa bainifu zinazofanana. Irabu zina sifa bainifu zake na konsonanti zina sifa bainifu zake. Kila lugha huteua baadhi ya sifa bainifu zinazotumika kubainisha foni katika kiwango cha kifonetiki na kuzitumia kuzifafanua fonimu za lugha hiyo.

Sauti zinazoweza kufikiriwa kuwa ni fonimu moja lazima zifanane sana kifonetiki. Kwa mfano hatuwezi kufikiria /i/na /a/ ni fonimu moja kwa sababu zinatofautiana sana kifonetiki yaani sifa bainifu zao ni tofauti sana.

| [i] | [a] |
|---|---|
| Mbele | kati |
| Juu | chini |
| Si viringo | Si viringo |

**Jozi za Mlinganuo Finyu**

Mlinganuo finyu ni tofauti ndogo kabisa ya kifonolojia iliyopo baina ya maneno fulani. Maneno hayo mara nyingi huwa na idadi sawa. Fonimu zote huwa zimefanana isipokuwa moja na mpangilio wa fonimu ulio sawa au unaolingana.

Mfano : piga      pi<u>t</u>a

Kul<u>a</u>      Kul<u>i.</u>

Katika maneno haya fonimu /g/, /t/, /a/ na /i/ ndio zinazotofautisha maana za maneno baina ya neno moja na jingine

Mlinganuo finyu unapatikana kwa kulinganua maneno mawili yenye tofauti ndogo. Hivyo jozi ya mlinganuo finyu ni orodha ya maneno mawili ambayo tofauti zake ni ndogo. Kigezo hiki cha mlinganuo finyu ni cha kiuamilifu kwa sababu ingawa maneno hayo yana tofauti ndogo lakini baada ya kuweka fonimu zenye sifa tofauti za kifonetiki neno linalopatikana lazima liwe la lugha husika na pia liwe na maana tofauti na neno la awali.

**Mgawanyo wa Kiutoano**

Hii ni mbinu nyingine ya kutambua fonimu. Hutumiwa kuonesha uhusiano uliopo baina ya sauti mbili au zaidi za fonimu moja ambazo haziwezi kutokea katika mazingira yanayofanana. Sauti ina mazingira maalum ambayo hayawezi kukaliwa na sauti nyingine. Mbinu hii inatuwezesha kutofautisha fonimu na alofoni.

Mazingira hayo hayawezi kukaliwa na sauti nyingine zaidi ya hiyo.

Mfano, katika lugha ya Kiingereza kuna sauti /P / yenye mpumuo na sauti /P/ isiyo na mpumuo ambazo tunaelewa wazi kuwa [P ] hutokea mwanzoni mwa neno tu, kwa mfano, katika /pin/, /pen/, /put/, nk. Kwa upande mwingine /p/ isiyo na mpumuo hutokea sehemu yoyote ya neno isipokuwa mwanzoni. Hapa tunapata kigezo muhimu sana cha kutofautisha fonimu na alofoni.

**Mpishano huru**

Kwa mujibu wa Mgullu (1999) akimnukuu Martinent anaeleza kuwa dhana ya mpishano huru ni maneno mawili yanayoweza kuwa na tofauti ya fonimu moja tu lakini tunapozitazama fonimu hizo zilizotofauti, tunaona wazi kuwa kwanza fonimu hizo ni tofauti sana Kifonetiki au haziwezi kuwa alofoni za fonimu moja, pia tunaona kwamba fonimu hizo zilizotofauti kifonetiki hazipo katika ule uhusiano wa kimtoano, yaani zote zinaweza kutumika katika mazingira yaleyale kwenye neno lakini fonimu hizo ingawa ni tofauti hazisababishi tofauti za maneno katika maneno zinamotokea yaani kila moja inaweza kutumiwa badala ya nyingine (katika maneno maalumu) bila kubadili maana katika maneno hayo.

*Mifano:*

*Alimradi* *ilimradi* */a/ na /i/*

*Baibui* *buibui* */a/ na /u/*

*Amkia* *amkua* */i/ na /u/*

*Bawabu* *bawaba* */a/ na /u/*

*Wasia* *wosia* */a/ na /o/*

*Benua* *binua* */e/ na /i/*

*Heri* *kheri* */h/ na /kh/ au /x/.*

## 6.5 Silabi

Silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho kwa ukubwa kipo kati ya fonimu na neno. Silabi ni ndefu kuliko fonimu na fupi kuliko neno.

Ni kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi ambacho sauti za lugha hutamkwa mara moja kwa pamoja kama fungu moja la sauti.

Mfano jaribu kutamka neno "mama" utagundua kuwa utatamka 'ma' kama fungu moja na ' ma' kama fungu linguine. Hivyo neno 'mama' lina silabi mbili ambazo ni ma/ma

1 2

Ingawa maneno ya lugha hutamkwa kwa kufuata utaratibu wa silabi lakini kila lugha ina muundo wake wa silabi na namna ya utamkaji wake. Fonimu zinapokaapamoja hujenga silabi ambazo huweza kutamkwa kama kitu kimoja.

### 6.5.1 Aina za Silabi

Wanaisimu wamegundua aina mbili (2) za silabi katika lugha. Nazo ni silabi huru/wazi na silabi funge.

**Silabi huru/wazi**

Silabi huru ni silabi ambazo mara nyingi huishia na irabu. Sauti za silabi huru huwa na msikiko au mvumo wa juu. Kutokana na kuishia na irabu, silabi huru huwa zinakuwa na msikiko mkubwa zaidi. Kwa mfano; la, ma, kwa, mba, n.k.

**Silabi funge**

Silabi funge ni silabi ambazo huishia na konsonanti. Silabi funge kwa kawaida huwa na msikiko hafifu kutokana na kuishia na konsonanti msikiko wake huwa na mvumo hafifu.

Wanafonolojia wengi wanaamini silabi ina sehemu kuu tatu:

(a) Mwanzo wa silabi

(b) Kilele cha silabi

(c) Mwisho wa silabi

Sehemu ya mwanzo na mwisho wa silabi ni sehemu ambazo husaidia kuweka mipaka katika silabi zinazofuatana.

Sehemu ya kilele cha silabi mara nyingi huwa katikati ya silabi na husikika kwa nguvu zaidi kuliko sehemu ya mwanzo na sehemu ya mwisho. Katika lugha nyingi irabu hukaa katika kilele cha silabi. Mara nyingi kila silabi inakuwa na irabu kama kilele chake hata iwe silabi huru au funge.

Irabu ikiwa peke yake au miongoni mwa sauti nyingine zinazounda silabi, irabu husikika kuwa kilele cha silabi.

Kuna baadhi ya lugha hutumia baadhi ya konsonanti pekee kama silabi. Mfano /m/, /n/, /l/ n.k

Katika Kiswahili nazali /m/ na /n/ huweza kusimama peke yake kama silabi.

| | | |
|---|---|---|
| Kwa mfano: | neno | silabi |
| | Mtu | m/tu |
| | Nta | n/ta |
| | Mkate | m/ka/te |

## 6.5.2 Miundo ya Silabi za Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ina miundo kadhaa ya silabi, nayo ni:

(a) Silabi za Irabu

(b) Silabi za Konsonanti

(c) Silabi za K+I

(d) Silabi K+K+I

(e) Silabi za K+k+I

(f) Silabi za K+K+K+I

(g) Silabi za K+I+K

**Silabi za Irabu**

Kiswahili kina irabu tano nazo huwa silabi za maneno mbalimbali.

| Mfano: neno | silabi |
|---|---|
| Ua | **u-a** |
| Oa | **o-a** |
| Teua | te-**u-a** |

**Silabi za Konsonanti**

Lugha ya Kiswahili huruhusu baadhi ya konsonanti kuwa silabi katika maneno. Mfano /m/ na /n/ huwa silabi katika mazingira maalum. Mara nyingi huwa mwanzoni au mwishoni mwa neno.

| Mfano : neno | silabi |
|---|---|
| Mpaka | **m**-pa-ka |
| Mganga | **m**-ga-nga |
| Namna | na-**m**-na |
| Nne | **n**-ne |

**Silabi za K+I**

Muundo huu wa konsonanti irabu ndio ulioshamiri zaidi si katika Kiswahili pekee bali katika lugha nyingi duniani. Maneno huwa na silabi moja, mbili au zaidi.

| Mfano : neno | silabi |
|---|---|
| Kaka | **ka-ka** |
| Samaki | **sa-ma-ki** |
| Takataka | **ta-ka-ta-ka** |

**Silabi za K+K+I**

Katika Kiswahili konsonanti za mwanzo katika muundo huu wa silabi huwa ni vitamkwa vya nazali /m/ na /n/. vitamkwa hivi huwa vinafungamana na konsonanti inayofuata ili kuunda muundo huu.

| Mfano : neno | silabi |
|---|---|
| Penda | pe-**nda** |
| Njama | **nja**-ma |
| Mbali | **mba**-li |

Pamoja na muundo huu wa nazali kutangulia pia kuna baadhi ya silabi zenye kuanza na vitamkwa visivyo nazali. Konsonanti zinapokabiliana katika muundo huu wa silabi huwa hazikubaliani na muundo wa lugha za kibantu.

| Mfano : neno | silabi |
| --- | --- |
| Stoo | **sto**-o |
| Sekta | se-**kta** |
| Labda | la-**bda** |

**Silabi za K+k+I**

Kiswahili kina muundo mwingine wa silabi ambao ni **K+k+I.** Muundo huu huhusisha vitamkwa *w* na *y*. Kwa kawaida konsonanti huwa mwanzoni na kufuatiwa na kiyeyusho (w au y) na kumalizia na irabu.

| Mfano : neno | silabi |
| --- | --- |
| Mwanga | **mwa**-nga |
| Afya | a-**fya** |
| Mpya | m-**pya** |
| Kwani | **kwa**-ni |

**Silabi za K+K+K+I**

Muundo huu unatumika zaidi kwa maneno ambayo yamekopwa kutoka lugha nyingine.

| Mfano : neno | silabi |
| --- | --- |
| Skrubu | **skru**-bu |
| Springi | **spri**-ngi |

**Silabi za K+I+K**

Kiswahili kina silabi chache ambazo huishia na konsonanti na zinajulikana kama silabi funge. Silabi funge mara nyingi hupatikana katika maneno yasiyo ya kibantu au maneno ya kukopwa.kwa maneno hayo kumekuwa na utata wa kuweka mpaka wa silabi.

| Mfano : neno | silabi | silabi |
| --- | --- | --- |
| Labda | lab-da | la-bda |
| Alhamisi | alha-misi | |
| Teknolojia | tek-no-lo-ji-a | |

## Zingatia

Vitu vinavyounda lugha ni: sauti (irabu, nusu-irabu, konsonanti) => silabi => maneno => sentensi => aya => tungo.

**Maana/dhana ya:**

**Fonolojia** ni taaluma inayochunguza jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi; ni kazi ya sauti husika ya kuleta maana wakati wa harakati za kuwasiliana baina ya Wana-jamii. Kipashio cha chini kabisa cha fonolojia huitwa fonimu.

**Fonetiki** ni taaluma inayochunguza jinsi sauti inavyopatikana. Katika uwanja wa Isimu, taaluma hii inayohusu jinsi sauti ya lugha ya binadamu inavyopatikana wakati wa harakati za kuitamka katika Bomba la Sauti. Kipashio cha chini kabisa cha fonetiki ni foni au sauti.

**Fonimu** ni kipashio cha chini kabisa cha fonolojia ambacho kina uwezo wa kubadilisha maana ya neno. Sauti-konsoni-mang'ong'o za Kiswahili nazo pia zina sifa za ufonimu.

Alofoni ni ni sauti ambayo haina uwezo wa kubadilisha maana ya neno.Kila alfabeti/alama ya foni/sauti itaandikwa katikati ya mistari ya aina hii**: [ ].**

Kila alfabeti/alama ya fonimu itaandikwa katikati ya mistari ya aina hii**: / /.**

## Zoezi

1. Vitaje vigezo vinavyoijenga lugha.
2. Fafanua dhana ya fonimu na alofoni huku ukitoa mifano.
3. Je, iko tofauti kati ya sauti na fonimu? Toa mifano.
4. Kwa nini sauti zifuatazo ni fonimu za Kiswahili?:
   (a) [ a ], [ e ], [ i ], [ o ], [ u ],

(b) [p], [t], [c], [k], [f], [v] [r], [l], [ð]

5. Je, sauti zifuatazo za Kiswahili zina alofoni zake? Toa mifano ukitumia uzoefu wako wa kuyasikia matamshi ya wana-jamii mbalimbali wanapozung umza kwa Kiswahili.
   (a) [ a ],  [ e ],  i ],  [ o ], [ u ],
   (b) [p], [t], [c], [k], [f], [v] [r], [l], [ð], [θ], [ɣ],

6. Eleza maana/dhana ya silabi

7. Zibaininsh silabi zinazojitokeza katika maneno yafuatayo:
   (i) wameshindwa
   (ii) haambiliki
   (iii) waliooana
   (iv) ugonjwa wa bana Simba si mba
   (v) huko nje ya nyumba yetu kuna mbu, samba na nge wengi

# Marejeo

1. Batibo, H. (1981), *Tuutazameje Mfungamano: King'ong'o- Konsonanti Katika Kiswahil.* TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
2. Habwe J na Karanja P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers : Nairobi.
3. Maganga, C., (1979), *Jinsi ya Kufundisha Matamshi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wageni.* TAKILUKI: Zanzibar.
4. Massamba, D, P, B. na Wenzake (2004), *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA) Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Taasisi Ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
5. Mdee, J. S. (1986), *Kiswahili: Muundo Na MatumiziYake*, Intercontinental Publishers: Nairobi.
6. Mgullu, Richard, S. (1999), *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia Na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers: Nairrobi.

# MUHADHARA 7
# Mofolojia ya Kiswahili kwa Ujumla

## 7.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu, tunakusudia kuelezea maana ya mofolojia, mofu, alomofu na mofimu kama ifuatavyo:

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu unatarajiwa kuweza:

- Kufafanua dhana/maana hasa ya mofolojia, mofu, alomofu, mofimu, neno, uambishaji naunyambulishaji.
- Kutaja aina mbalimbali za mofu, alomofu na maneno.
- Kueleza maana ya uambishaji na unyambulishaji wa maneno.

## 7.2 Maana ya Mofolojia

Wanaisimu wengi wamekubali kuwa mofolojia kama taaluma inaweza kugawanyika katika matawi makuu mawili, yaani: (a) Fonolojia ya uundaji maneno *(Derivational Morphology)*
(b) Fonolojia ya minyambuliko ya maneno *(Inflectional Morphology);* Mgullu
(1999:96).

Madai ya Mgullu yana maana ya kwamba mofolojia ni taaluma inayoshughulikia si tu vipashio vya lugha vinavyoliunda neno la lugha hiyo, bali pia minyambuliko ya maneno yaliyoundwa kwa vipashio husika ambavyo wanaisimu huviita mofu.

TUKI (1990:40) nao wanadai kuwa mofolojia ni tawi la isimu ambalo huchunguza maneno na aina zake.

### 7.2.1 Dhana ya Mofu

Mofu ni vipashio vidogo kabisa ambavyo vina uwezo wa kusetiri maana ya neno ambalo kwavyo limeundwa. Katika lugha yoyote mofu ni nyingi sana lakini wingi wa mofu hizo unaweza kugawika katika makundi makubwa mawili tu:mofu zenye maana ya kisarufi, na mofu zenye maana ya kileksika/msamiati.

#### (i) Mofu Zenye Maana ya Kisarufi

Ni mofu zinazoambatanishwa ili kuliunda neno lenye maana kamili. Mzizi ni mojawapo kati ya mofu zinazoambatanishwa katika kuliunda neno husika. Kwa hiyo, mofu zenye maana ya kisarufi huhusu vipengele mbalimbali vya muundo wa lugha yenyewe.

Kwa mfano wa kwanza:

Idadi *(umoja au wingi)* katika *m* – toto (umoja), *wa* – toto (wingi).

Nafsi (ya kwanza: mimi {ni-}, sisi {tu-}.)

(ya pili: *wewe {u-}, nyinyi {m-}.)*

*(*ya tatu: *yeye {a-}, wao {wa-}).*

Njeo/wakati:(uliopo: {-na-}.)

(uliopita: {-li-}, {-ka-}, {-ngali-});na (ujao: {-ta-})

Hali:(timilifu: a-me-fika),

(ya kuendelea: a-na-lima),

(ya mazoea: hu-lima).

#### (ii) Mofu Zenye Maana ya Kileksia/Msamiati

Ni mofu zisizoambatanishwa na mofu nyingine yo yote; neno lenyewe huwa ndiyo mofu hiyo hiyo! Kwa mfano:

Baba, mama, kaka, dada, kuku, mimi. Wewe, yeye, chura, simba, njiwa, ng'ombe, na, sababu, nk.

Kwa mfano wa pili:

Katika neno *amemnywesha,* kuna vipashio kadhaa ambavyo vimehusika katika kulijenga neno hili la Kiswahili. Vipashio hivyo vimebeba maana kamili katika Kiswahili. Tukivitenganisha, vinajitokeza kama ifuatavyo na, maana ya kila kipashio kilichohusika katika kuliunda neno hili itaeleweka na kila Mswahili:

{a + me + m + nyw + esh + a}

1 2 3 4 5 6

Nafasi ya 1ambapo pametamkwa mofu {a} na, katika nafasi hiyo, panaweza kutamkwa mofu {wa}, {u}, [m}, {ni}, {tu}, {ik}, {vi}, {li}, nk. Mofu zote hizi zinashereshea maana ya mtenda jambo, yaani hii ni *mofutenda.*

Nafasi ya 2 ambapo pametamkwa mofu {me} na, katika nafasi hiyo, panaweza kutamkwa mofu {ta}, {takapo}, {li}, [na}, {nge}, {ngali}, {ka}, nk. Mofu zote hizi zinashereshea maana ya wakati/njeo au hali au masharti/ kutegemeana, yaani hii ni *mofu-wakati/njeo* au *mofu-hali* au *mofu-masharti.*

Nafasi ya 3 ambapo pametamkwa mofu {m} na, katika nafasi hiyo, panaweza kutamkwa mofu {wa}, {ku}, [li}, {ni}, {tu}, {ka}, {ji}, nk. Mofu zote hizi zinashereshea maana ya mtendwa jambo, yaani hii ni *mofu-tendwa.*

Nafasi ya 4 ambapo pametamkwa mofu {nyw} ambayo ni mzizi unaobeba maana ya neno zima, yaani hii ni *mofu-mzizi.*

Nafasi ya 5ambapo pametamkwa mofu {esh} ambayo inaleta maana ya kumfanya mtu atende jambo fulani, yaani hii ni *mofu-tendeshi.*

Nafasi ya 6 ambapo pametamkwa mofu {a} ambayo *inaishiliza neno,* lakini pia inaonesha kwamba jambo fulani latendeka. Wataalamu wengi huiita *mofu-yakinishi.* Kwa mujibu wa mfano wetu huu, jambo linalotendeka hapa ni la ku-*nywesha.*Tuangalie mifano ifutayo:

{a - me - m - nywesh-a}

{wa - ka - ni - nywesh-a}

{u - li - tu - nywesh-a}

{tu - takapo -ku - nywesh-a}

{li - nge - wa - nywesh-a}

Kwa mfano huu, vipashio vyote vyenye kuonesha mtenda, njeo, mtendwa, tendo, masharti/kutegemeana, hali ya kuyakinisha, nk. huitwa mofu.Kwa ufupi, mofuni kipashio kidogo kabisa chenye uwezo wa kusetiri maana kamili.

### 7.2.2 Aina za Mofu

Mofu huainishwa kwa kuzingatia vigezo viwili:

(i) Kigezo cha maana zinazowakilishwa na mofu;

(ii) Kigezo cha mofolojia ya mofu.

Tunapotumia kigezo cha maana zinazowakilishwa na mofu, tunapata aina tatu za mofu, yaani: (i) Mofu huru (ii) Mofu funge (iii) Mofu tata

Kwa upande mwingine tunapotumia kigezo cha mofolojia au maumbo ya mofu zenyewe tunapata aina mbili za mofu, yaani:

Mofu changamano

Mofu kapa

Kwa mantiki hii tunazo aina tano za mofu ambazo ni:

Mofu huru

Mofu funge

Mofu tata

Mofu-changamano

**(i) Mofu Huru**

Mofu huru ni zile mofu ambazo zinaweza kukaa peke yake kama maneno kamili yenye maana inayoweza kueleweka bila kusaidiwa na mofu nyingine. Aghalabu, mifano mingi ya mofu huru hupatikana kutoka kwenye vipashio vya lugha, kama ifuatavyo:

Nomino: {baba}, {kuku}, {sungura}, {ndege}, {dada}, {paka}, nk.

Vivumishi: {safi}, {baya}, {dhaifu}, {zuri}, {imara}, {hodari}, nk.

Viwakilishi: {mimi}, {sisi}, {wewe}, {ninyi}, {yeye), {wao}, nk.

Vielezi: {upesi}, {haraka}, {sana}, {leo}, {jana}, {juzi}, nk.

Vitenzi: {tafiti}, {samehe}, {arifu}, {sali}, {jibu}, {badili}, nk.

Vihusishi: {ya}, {juu}, {mbele}, {kwa}, nk.

Viunganishi: {na},{halafu}, {bado}, {ila}, {aidha},{pia}, nk.

Kwa mujibu wa mifano hii inadhihirika kwamba Kiswahili kinazo mofu huru nyingi ambazo zimo katika aina zote za vipashio vya lugha. Hivyo, mofu huru ni mofu ambazo zinaweza kukaa peke yake kama maneno kamili yanayoeleweka bila kusaidiwa na viambishi.

**(ii) Mofu funge au Mofu tegemezi**

Mofu funge au Mofu tegemezi ni mofu ambayo haiwezi kutumiwa peke yake kama neno lililo na maana yake kamili; aghalabu mofu funge hutumiwa kama kiambishi tu kinachoambatanishwa na mzizi au viambishi vingine ili kulikamilisha neno husika. Mofu funge ina sifa zake ambazo ni pamoja na:

Mofu funge haiwezi kukaa peke yake ikawa neno kamili.

Mofu funge ni lazima iambatanishwe na angalau mafu nyingine moja ndipo tupate neno kamili.

Kutokana na sifa hii ndiyo mdiyo maana wanaisimu wengine huziita mofu hizi kuwa ni *mofu tegemezi* ambayo ina maana sawa na *mofu funge*

**Mfano:**

Idadi ya Umoja

Idadi ya Uwingi m-toto (m) wa-toto (wa) ki-su (ki) vi-su (vi)

m-ti (m) mi-ti (mi)

Ukumbwa wa Nomino

Udogo wa Nomino ji-tu (ji) ki-ji-tu (ki)

ji-su (ji) ki-ji-su (ki)

Maana za mofu funge hutegemea sana muktadha wa mofu funge husika. Mofu funge ikiondolewa kwenye muktadha wake hukosa maana na ni vigumu kujua maana yake bila kuiweka katika muktadha wa neno. Mofu funge inaponing'inizwa peke yake haituwezeshi hata kidogo kujua maana yake.

Umbo moja linaweza kuwa na maana nyingi kwa mujibu wa miktadha ambamo imeambatanishwa katika mzizi wa neno. Aghalabu, mofu funge ni sawa na viambishi vya mizizi mbalimbali katika neno. Hii ina maana kwamba viambishi vilivyo vingi katika lugha huwa ni mofu funge. Tunasema viambishi vingi kwa sababu si viambishi vyote ambavyo huundwa kwa mofu funge. Vipo viambishi vingine ambavyo huundwa kwa mofu huru. Baadhi ya mizizi ya maneno pia huwa ni ya mofu funge kwa sababu mizizi hiyo huwa haiwezi kukaa peke yake ikawa neno kamili. Mifano mizuri ya mizizi ya maneno ya Kiswahili ambayo huundwa kwa mofu funge ni ile ya vitenzi vya silabi moja moja, kama ifuatavyo kwa mfano:

| Mofu funge | Neno |
|---|---|
| {l-) | kula |
| {-j-} | kuja |
| {-p-} | mpe |
| {-ny-} | kunya |
| {-nyw-} | kunywa |

{a} + {me} + {m} + {nyw} + {esh} + {a} amemnywesha

Mizizi ya vitenzi hivi ni mizizi ya mofu-funge kwa sababu haiwezi kutumiwa peke yake kama neno na, pia maana zao huwa hazijitokezi mpaka mizizi iwekewe viambishi.

**(iii) Mofu Tata**

Mofu tata ni mofu ambazo huwa na maana zaidi ya moja au kuanzia mbili na kuendelea.

Mfano:

Saidi alimpigia Mbaraka mpira.

Sentensi hii ni tata kwa sababu ina maana zaidi ya moja.  Utata wa sentensi hii haupo kwenye muundo wake wa kisarufi, bali upo katika kitenzi *alimpigia*.

Kitenzi hiki kina mofu sita, yaani:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| {a-} + | {-li-} + | {-m-} + | {-pig-} + | {-i-} + | {-a} |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |

Kati ya mofu hizi zote sita, mofu ya tano {-i-} ndiyo yenye utata. Mofu {i} ni mofu ya kutendea kwa sababu tukisema: '*Saidi alimpigia Mbaraka mpira',* maana zinazoweza kueleweka na wasikilizaji ni nne:

Saidi aliupiga mpira kwa niaba ya Mbaraka; yaani Mbaraka ndiye aliyetakiwa aupige mpira ule, lakini kwa sababu ambazo hazikuelezwa, badala ya Mbaraka kuupiga mpira ule, Saidi akaupiga.

Saidi aliupiga mpira kuelekea kwa Mbaraka; yaani Saidi na Mbaraka walikuwa wakicheza mpira. Ikapatikana fursa, Saidi akaupiga mpira ule kuelekea kwa Mbaraka. Kwa hiyo, hapa tunazungumzia mwelekeo wa mpira.

Saidi alimpiga Mbaraka kwa kuutumia mpira; yaani, Saidi anautumia mpira kama *ala* (silaha) ya kumpigia Mbaraka.

Saidi alimpiga Mbaraka kwa sababu ya mpira; yaani hapa, mpira ndio sababu kubwa ya Saidi ya kumpiga Mbaraka. Tuseme labda Saidi alikuwa na mpira wake, halafu Mbaraka akauchukuwa kuuchezea na kwa bahati mbaya akaupoteza. Saidi anapogundua kwamba Mbaraka ameupoteza mpira wake, basi ndipo akampiga.

Kwa maelezo hayo, ni wazi kwamba sentensi yetu ina utata kwa kuwa inatupatia maana tofauti tofauti zipatazo n'ne ambazo zimesababishwa na mofu {-i-} ya kutendea.

### (iv) Mofu Changamani

Mofu changamani ni mofu ambazo huundwa kwa kuweka pamoja angalau mofu-sahili mbili au mofu funge na mofu sahili yakafanyiza neno lenye kuleta maana kamili, kwa mfano:

Mofu sahili + Mofu sahili

{askari} + {kanzu} = askari kanzu.

{gari} + {moshi} = gari moshi.

{paka} + {shume} = paka shume.

{m'mbwa} + {mwitu} = m'mbwa mwitu.

{fundi} + {chuma} = fundi chuma.

nk.

Mofu funge + Mofu huru

{mw} + {-ana}+ {nchi} = mwananchi.

{ki} + {-on-} + {a} + {mbali}= kiona mbali.

{mw} + {-ana}+ {hewa }= mwanahewa. nk.

### (v) Mofu Kapa

Mofu kapa ni mofu za pekee ambazo hazina umbo. Mofu kapa hazitamkwi wala kuandikwa. Mofu kapa hazionekani katika neno, lakini athari zinazotokana na hiyo mofu kapa husika hueleweka. Ingawa mofu hizi huwa hatuzioni wala kuzitamka au kuziandika, lakini maana zake tunazipata. Tukichunguza ruwaza ya viambishi awali vya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili, tunaweza kuzigawa nomino za Kiswahili katika makundi makuu man'ne, yaani:

Nomino zilizo na viambishi bayana vya idadi ya umoja na uwingi:

Mfano:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| *m* - tu | *wa* - tu |
| *m* - toto | *wa* - toto |
| *m* - ti | *mi* – ti nk. |

Nomino zilizo na kiambishi awali cha umoja tu, cha wingi hakipo, kwa hivyo, ni kapa (φ)

Mfano:

| Umoja | Wingi | |
|---|---|---|
| *u* - kuta | φ - kuta | |
| *u* - funguo | φ - funguo | |
| *u* – kucha | φ – kucha. | nk. |

(c) Nomino zilizo na kiambishi cha wingi tu, cha umoja hakipo; kwa hivyo, ni kapa (φ)

Mfano:

| Umoja | Wingi | |
|---|---|---|
| φ – kasha | *ma* – kasha. | |
| φ – debe | *ma* – debe. | |
| Φ – jembe | *ma* - jembe | nk. |

(d) Nomino zisizo na kiambishi awali cha umoja wala cha wingi

Mfano:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Φ - mama | Φ - mama. |
| Φ - ng'ombe | Φ - ng'ombe. |
| Φ - baba | Φ - baba. |
| Φ - kaka | Φ - kaka. |
| Φ - dada | Φ - dada. |
| Φ - mbuzi | Φ - mbuzi. |
| Φ - ngamia | Φ - ngamia. |
| Φ - kondoo | Φ - kondoo. |
| Φ - tembo | Φ - tembo. |
| Φ - sungura | Φ - sungura. |
| Φ - nguruwe | Φ - nguruwe. |
| Φ - simba | Φ - simba. nk. |

(e) Sherehe kuhusu Mofu kapa

Katika kuonyesha mofu kapa nomino zina kiambishi awali cha umoja tu, wakati cha wingi hakipo. Kinachotokea hapa ni kwamba ukisema ukucha watu wanaelewa kuwa ni ukucha mmoja tu. Lakini ukisema kucha, watu wataelewa kuwa ni kucha nyingi.

Na hali hii ndivyo ilivyo kwa maneno ufunguo ǂ funguo; ukuta ǂ kuta, nk. inajulikana kuwa ni ufunguo mmoja tu na akisema funguo, ni kwa maana ya wingi; lakini umbo lenyewe linaloileta hiyo maana ya wingi halionekani bayana katika neno.

Ili kuyaeleza haya maumbo ambayo hayapo lakini maana zinazowakilishwana maumbo hayo zipo, Wanaisimu wamekubaliana kuyaita maumbo haya kapa, yaani mofu ambazo hazipo. Mofu hizi ni dhahania tu katika akili zetu kwa kufahamu tu kwamba maana fulani haiwezi kuja tu yenyewe lazima iletwe na mofu fulani. Kwa hivyo, hata kama mofu hiyo haionekani, lakini ipo; ni mofukapa.

Kwa mfano, katika matamshi ya maneno: kasha, debe, jembe, umoja na uwingi wake hudhihirishwa kama ifuatavyo:

| Umoja | Uwingi |
|---|---|
| kasha | makasha |
| debe | madebe |
| jembe | majembe |

Katika nomino hizi mofu ya uwingi ni mofu {ma} lakina mofu ya umoja ni mofu kapa, yaani haipo na huoneshwa kwa alama {Φ}.

Kwa mantiki hiyo, mofu za maneno haya ni kama ifuatavyo:

| Umoja | Uwingi |
|---|---|
| {Φ} + kasha | {ma} + {kasha} |
| {Φ} + debe | {ma}+ {debe} |
| {Φ}+jembe | {ma} + {jembe} |

## Zingatia

Dhana ya mofu inadai kwamba mofu ni vipashio vidogo kabisa ambavyo vina uwezo wa kusetiri maana ya neno ambalo kwavyo limeundwa.

**Mofu huru** ni zile mofu ambazo zinaweza kukaa peke yake kama maneno kamili yenye maana inayoweza kueleweka bila kusaidiwa na mofu nyingine.

**Mofu funge** au Mofu tegemezini mofu ambayo haiwezi kutumiwa peke yake kama neno lililo na maana yake kamili; aghalabu mofu funge hutumiwa kama viambishi tu kinachoambatanishwa na mzizi au viambishi vingine ili kulikamilisha neno husika.

**Mofu tata** ni mofu ambazo huwa na maana zaidi ya moja au kuanzia mbili na kuendelea.

**Mofu changamani** ni mofu ambazo huundwa kwa kuweka pamoja angalau *mofu sahili mbili* au *mofu funge* na *mofu sahili* yakaunda neno kamili lenye kuleta maana kamili.

**Mofu kapa** ni mofu za pekee ambazo hazina umbo. Mofu kapa hazitamkwi wala kuandikwa. Mofu kapa hazionekani katika neno lakini athari zinazotokana na kutokuwepo kwa mofu hii hueleweka, yaani maana ya neno husika inaeleweka.

## Zoezi

1. Fafanua dhana ya mofu
2. Taja aina za mofu za Kiswahili ukitoa mifano muafaka

## 7.3 Alomofu

Alomofu ni vivuli au vipashio au maumbo mbalimbali, yaani {alo}, yanayowakilisha kitu fulani; hapa kitu chenyewe ni mofu.Jumla yavivuli aumaumbo husika, husetiri maana moja ya mofu husika, lakini vivuli hivi havina uwezo wa kubadilisha maana ya mofu husika.

### 7.3.1 Aina za Alomofu

**(i) Alomofu za Mofu Zenye Maana ya Nafsi**

Alomofu za Mofu ya Nafsi zinajitokeza katika hali ya umoja na wingi kama ifuatavyo:

Alomofu za Mofu ya Nafsi katika hali ya *umoja* ni:

Nafsi ya kwanza (mzungumzaji): {ni};

Nafsi ya pili(unayempasha habari): {u};]

Nafsi ya tatu (habari yenyewe), kama ni mtu, alomofu yake ni {a}, na kama ni kitu, alomofu yake ni {ki} ambayo nayo itajibainisha kwa mujibu wa ngeli ya kila kitu husika katika mazungumzo kati ya nafsi ya kwanza na ya pili.

Alomofu za Mofu ya Nafsi katika hali ya *wingi* ni:

Nafsi ya kwanza (mzungumzaji): {tu;

Nafsi ya pili (unayempasha habari): {m}

Nafsi ya tatu (habari yenyewe), kama ni mtu, alomofu yake ni {wa},na kama ni kitu, alomofu yake ni {vi} ambayo nayo itajibainisha kwa mujibu wa ngeli ya kila kitu husika katika mazungumzo kati ya nafsi ya kwanza na ya pili.

Alomofu za Mofu Zenye Maana ya Njeo

Baadhi ya Alomofu zinazowakilisha mofu ya njeo sambamba na njeo husika ni:

| MOFU YA NJEO | ALOMOFU | NJEO |
|---|---|---|
| | {-na-} | iliyopo |
| | {-li-} | iliyopita |
| | {-ta-} | Ijayo |

Alomofu za Mofu ya Masharti/Kutegemeana/Shurutia

Mofu ya masharti/kutegemeana/shurutia inaweza kuwakilishwa na alomofu, yaani maumbile/vivuli mbalimbali vya mofu ya masharti/kutegemeana. Ni mofu ya masharti au kutegemeana kwa sababu jambo mojawapo kati ya mawili yanayotakiwa lazima liwepo ndipo jambo la pili lifanyike, vinginevyo, mambo hayafanyiki.

**Mfano:**

Alomofu {-ki-}, {-nge-}, {-ngali-}, [-japo-}, {endapo}, nk. katika:

Bwana Nihuka akija ICE, atakutana na Dakta Nchimbi.

Bwana Nihuka angekuja ICE, angekutana na Dakta Nchimbi.

Endapo Bwana Nihuka atakuja ICE, atakutana na Dakta Nchimbi.

Bwana Nihuka angalikuja ICE, angalikutana na Dakta Nchimbi.

Ajapo Bwana Nihuka ICE, atakutana na Dakta Nchimbi.

Ilivyo hapa ni kwamba {-ki-}, {-nge-}, {-ngali-}, [-japo-}, {endapo} zote ni alomofu ambazo zinasetiri maana ya mofu moja ambayo ni ya mashariti; ni mofu ya mashariti kwa sababu Bwana Nihuka hawezi kukutana na Dakta Nchimbi mpaka hapo atakapokwenda ICE. Kwa maana nyingine, kukutana kwa Bwana Nihuka na Dakta Nchimbi kunategemea kitendo cha Dakta Nchimbi kuwepo ICE na Bwana Nihuka kwenda hapo ICE.

### (iv) Alomofu za Mofu ya Kutendea {i}

Mofu ya Kutendea {i}inaweza kuwakilishwa na alomofu nne zinazojitokeza katika mazingira kifonolojia wakati wa unyambulishaji wa mofu za vitenzi vyenye asili ya Kiswahili; nazo ni {i}, {e}, {li}, {le}.

*Alomofu {i} ya Mofu ya Kutendea {i}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti katika mzizi ambao una irabu ama /a/, au /i/, au /u/; kwa mfano:

paka => {pak} + {a} => pakia => {pak} + {i} + [a}. kata => {kat} + {a} => katia => {kat} + {i} + [a}.

lima => {lim} + {a} => limia => {lim} + {i} + [a}. zima => {zim} + {a} => zimia => {zim} + {i} + [a}. funga => {fung} + {a} => fungia => {fung} + {i} + [a}.
suka => {suk} + {a} => sukia => {suk} + {i} + [a} nk.

*Alomofu {e} ya Mofu ya Kutendea {i}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti katika mzizi ambao una irabu ama /e/, au /o/; kwa mfano:
teka => {tek} + {a} => tekea => {tek} + {e} + [a}. tenda => {tend} + {a} => tendea => {tend} + {e} + [a}.

toka => {tok} + {a} => tokea => {tok} + {e} + [a}. soma => {som} + {a} => somea => {som} + {e} + [a}. nk.
*Alomofu {le} ya Mofu ya Kutendea {i}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na irabu ama /e/, au /o/; kwa mfano: zoa => {zo} + {a} => zolea => {zo} + {le} + [a}. toa => {to} + {a} => tolea => {to} + {le} + [a}. nk.

*Alomofu {li} ya Mofu ya Kutendea {i}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na irabu ama /a/ /i/ au /u/.; kwa mfano: kaa => {ka} + {a} => kalia => {ka} + {li} + [a} zaa => {za} + {a} => zalia => {za} + {li} + [a} kimbia => {kimbi} + {a} => kimbilia => {kimbi} + {li} + [a} tia => {ti} + {a} => tilia => {ti} + {li} + [a} pakua => {paku} + {a} => pakulia => {paku} + {li} + [a} tua => {tu} + {a} => tulia => {tu} + {li} + [a}

**(v) Alomofu za Mofu ya Kutendeka {ek}**

Mofu ya Kutendeka {ek}inaweza kuwakilishwa na alomofu nne
zinazojitokeza katika mazingira kifonolojia wakati wa unyambulishaji wa mofu za vitenzi vyenye asili ya Kiswahili; nazo ni {ik},{ek},{lik} na {lek}.

*Alomofu {ek} ya Mofu ya Kutendea {ek}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti katika mzizi ambao una irabu /e/; kwa mfano:

penya => {peny} + {a} => penyeka => {peny} + {ek} + [a}. sema => {sem} + {a} => semeka => {sem} + {ek} + [a}.

*Alomofu {ik} ya Mofu ya Kutendea {ik}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti na ambao una irabu /a/,/i/,/na/,/u/ kwa mfano:

kata => {kat} + {a} => katika => {kat} + {ik} + [a}.

lamba => {lamb} + {a} => lambika => {lamb} + {ik} + [a}

pika => (pik) + (a) => pikika

vuta => (vut) + (a) => vutika

*Alomofu {lek} ya Mofu ya Kutendea {ek}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na irabu /o/; kwa mfano:

toboa=> {tobo} + {a} => toboleka => {tobo} + {lek} + [a}.

zoa => {zo} + {a} => zoleka => {zo} + {lek} + {a}.

*Alomofu {lik} ya Mofu ya Kutendea {*ek}hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na irabu /u/; kwa mfano:

chukua=> {chuku} + {a} => chukulika => {chuku} + {lik} + [a}.

sahau=> {sahau} => sahaulika => {sahau} + {lik} + [a}.

**(vi) Alomofu za Mofu ya Kutendesha {esh}**

Mofu ya Kutendesha {esh}inaweza kuwakilishwa na alomofutano zinazojitokeza katika mazingira kifonolojia wakati wa unyambulishaji wa mofu za vitenzi vyenye asili ya Kiswahili; nazo ni {ish},{esh}, {iz}, {lish} na {lesh.

*Alomofu {esh} ya Mofu ya Kutendesha {esh}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti katika mzizi ambao una irabu /e/. au /o/; kwa mfano:

weza=> {wez} + {a} => wezesha => {wez} + {esh} + [a}.

enda => {end} + {a} => endesha => {end} + {esh} + [a}.

lewa => {lew} + {a} => lewesha => {lew} + {esh} + {a}

choka => {chok} + {a} => chokesha => {chok} + {esh} + [a}.

koma => {kom} + {a} => komesha => {kom} + {esh} + [a}.

*Alomofu {ish} ya Mofu ya Kutendesha {esh}*hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti katika mzizi ambao una irabu /a/. /i/, au /u/; kwa mfano:

kata => {kat} + {a} => katisha => {kat} + {ish} + [a}.

lamba => {lamb} + {a} => lambisha => {lamb} + {ish} + [a}.

lipa => {lip} + {a} => lipisha => {lip} + {ish} + {a}.

funda => {fund} + {a} => fundisha => {fund} + {ish} + {a}.

fumba => {fumb} + {a} => fumbisha => {fumb} + {ish} + {a}.

**(vii) Alomofu {fy}, {vy}, {sh}, {z} ya Mofu ya Kutendesha {esh}**

Utokeaji waalomofu {fy}, {vy}, {sh}, {z}ya Mofu ya Kutendesha {esh} haufuati kanuni zinazotabirika; kwa mfano:

ogopa => {ogop} + {a} => ogofya => {ogo} + {fy} + [a}.

lewa => {lew} + {a} => levya => {le} + {vy} + [a} = lewesha

shuka => {shuk} + {a} => shusha => {shu} + {sh} + {a} = shukisha.

lala => laza

**(viii) Alomofu {e}, {i} za Mofu Tamatishi {a}**

Ieleweke kwamba vitenzi asilia vyote katika Kiswahili huishia kwa kiambishi [a], na kwa hiyo, kuitwa Kiambishi Tamati {a} ambacho kazi yake kubwa kuyakinisha tendo linaloashiriwa na kitenzi husika

katika hatua yake ya mwisho ya matumizi katika sentensi. Kwa mantiki hiyo, kiambishi tamati hiki huitwa Mofu Tamatishi {a}. Mofu tamatishi hii ina alomofu zake ambazo ni {e} na {i}.

Alomofu {e} ya Mofu Tamatishi {a}

Alomofu {e} ya mofu tamatishi {a}, hutokea wakati mofu tamatishi {a} inapoashiria tendo la kuiamrisha nafsi ya tatu,kwa mfano:

| Kitenzi | Tendo la Kuiamrisha Nafsi ya Pili | Tendo la Kuiamrisha Nafsi ya Tatu |
|---|---|---|
| Kukimbi-a | kimbi-a | akimbi-e |
| Kulip-a | lip-a | Alip-e |

nk.

Alomofu {i} ya Mofu Tamatishi {a}

Alomofu {i} ya mofu tamatishi {a}, hutokea wakati mofu tamatishi {a} inapoashiria tendo la kukanusha ambalo hufanywa na nafsi zote tatu katika umoja na wingi wake, kwa mfano:

| Tendo la Kuiamrisha Nafsi ya Pili | Kukanushwa kwa Tendo na Nafsi Zote Tatu – Umoja | Kukanushwa kwa Tendo na<br>Nafsi Zote Tatu – Wingi |
|---|---|---|
| kimbi-a | Nafsi -1: *si*kimbi-i<br>Nafsi -2: *hu*kimbi-i<br>Nafsi -3: *ha*kimbi-i | Nafsi -1: *hatu*kimbi-I<br>Nafsi -2: *ham*kimbi-i<br>Nafsi -3: *hawa*kimbi-i |
| lip-a | Nafsi -1: *si*lip-i<br>Nafsi -2: *hu*lip-i<br>Nafsi -3: *ha*lipi-i | Nafsi -1: *hatu*lip-I<br>Nafsi -2: *ham*lip-i<br>Nafsi -3: *hawa*lipi-i |

.

## Zingatia

Dhana ya alo-mofu inadai kwamba alomofu ni vivuli au vipashio au maumbo mbalimbali, yaani {-alo}, yanowakilisha kitu Fulani, hapa kitu chenyewe ni mofu jusika. Lakini vivuli hivi havina uwezo wa kubadilisha maana ya mofu husika

## Zoezi

1. Fafanua dhana ya alo-mofu
2. Taja aina za alo-mofu za Kiswahili huku ukitoa mifano muafaka

# 7.4 Mofimu

Wanaisimu kadhaa wa Kiswahili wametoa dhana ya *mofimu;* baadhi yao ni hawa wafuatao: Rubanza, Y.I. (1996:1) anadai: 'mofimu ni kipashio kidogo chenye maana ya kisarufi au ya kileksika.' Anaendelea kudai (1996:13): 'mofimu ni kipashio kidogo kabisa cha kiisimu ambacho kina maana.' TUKI (1990:40) wanadai: '... mofimu ni kipashio kidogo kabisa amilifu katika maumbo ya maneno.'

Dhana ya mofimu kama zilivyofafanuliwa na TUKI (1990:40) na Rubanza (1996:1) zinafanana; lakini fafanuzi hizi zinakanganya kati ya dhana ya mofu na alomofu. Habwe na Karanja, (2004:240) wanadai: 'mofimu ni maana katika lugha ambayo haigawiki. Husitiriwa na mofu. Wanaendelea kudai kwamba:

'mofu ni umbo lenye kubeba mofimu.'

Kutokana na maelezo haya kuhusu dhana ya mofimu, ni vigumu kujua ni kwa dhana ipi ya mofimu ambayo ingetufaa kutuelimisha kwa hilo. Inadaiwa kwamba 'mofimu ni kipashio kidogo kabisa cha kiisimu ambacho kina maana.' Lakini inavyoeleweka na wanaiisimu ni kwamba mofu ni umbo halisi katika lugha; huaandikwa, huonekana na kusomeka lakini mofimu ni maana ambayo wenye lugha

huipata kwa kutafsiri umbo halisi la mofu lililoandikwa, likaonekana na kusomeka. Umbo hilo hutolewa tafsiri kwa sababu tafsiri husika haionekani katika umbo la mofu husika; tafsiri ya mofu imesetiriwa, imehifadhiwa au kufichwa katika hiyo mofu. Sasa iweje basi dhana ya mofu iwe sawa na ile ya mofimu? Kwa kuzingatia mantiki hiyo hapo juu, ni dhahiri kwamba mofimu ni maana ambayo imesetiriwa/imehifadhiwa/imefichwa na mofu au (vivuli vya mofu, yaani) alomofu.

**Kwa mfano:**

| | Neno | Mofu | Mofimu (Maana) | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Neno | Mofu | Mofimu (Maana) | |
| | {a – na – lim – a} | {a - } | (i) | mtenda (= kiima) |
| | | | (ii) | kiambishi kiwakilishi cha upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya kwanza. |
| | | | (iii) | nafsi ya tatu. |
| | | | (iv) | umoja. |

(b) Neno:{anapigana}, yaani{a – na – pig – an – a} linaweza kuwa sentesi kamili ambapo sehemu za sentensi kisintaksia zimewakilishwa na mofu (maumbo) mbalimbali zenye maana tofauti kisintaksia kama ifuatavyo:

| Neno | Mofu(maumbo) | Mofimu (Maana) |
|---|---|---|
| {anapigana} | {a-} | kiima |
| | {-na-} | wakati (njeo) iliyopo |
| | {-pig-} | mzizi wenye maana ya kileksika ya kugonga |
| | {-an-} | kitendo cha kufanyana |
| | {-a} | kiishilizi cha kuundia kitenzi katika Kiswahili |

Zingatia kwamba yote tuliyoyaandika, kuyaona na kuyasoma kwenye upande wa mofimu (maana) hatuyaoni kwenye upande wa mofu. Hii ni tafsiri ya Waswahili ambayo imefichwa katika mofu (maumbo).

**Zingatia**

Dhana ya Mofimu ni maana ambayo imesetiriwa/imehifadhiwa/imefichwa na mofu (vivuli vya mofu) alomofu

**Zoezi**

1. Fafanua dhana ya alo-mofu
2. Taja aina za alo-mofu za Kiswahili huku ukitoa mifano muafaka

## 7.5 Neno ni Nini?

Mpaka sasa Wataalamu hawajafikia muafaka kuhusu maana au dhana ya neno neno. Maelezo yaliyotolewa na TUKI (1990:58) kuhusu dhana au maana ya neno neno yatasadifu kwa sasa wanapodai kuwa neno ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa na kuleta maana.

**Mfano:**

i. Nyati
ii. Mtoro

Neno hujengwa na mofu moja au zaidi ya moja.


### *(i) Neno Sahili*

Neno lililojengwa kwa mofu moja, ni *neno-sahili* kwa sababu halina viambishi, kwa mfano: kaka, (ii) nyau, (iii) mama, (iv) baba, nk.

Kama mifano hii inavyoonesha, neno-sahili limeundwa kwa mzizi peke yake.

(ii) ***Neno Changamani***

Neno lililojengwa kwa mofu zaidi ya moja huitwa neno changamani. Neno changamani linaundwa kwa aina mbili za mofu, mzizi na viambishi. Maelezo hayo yanaweza kuelezwa kimchoro kama ifuatavyo:




Maneno mengi katika lugha ya Kiswahili ni changamani.Tungo za maneno zinaweza kuwa katika aina zifuatazo za maneno.

| Aina ya Neno | Neno-Mfano | Mofu |
|---|---|---|
| Nomino | mwalimu (changamano) | mw-alimu |
| Kivumishi | safi (sahili) mimi (sahili) | safi |
| Kiwakilishi | analima (changamano) | mimi a-na-lim-a |
| Kitenzi | kabisa (sahili) kwa | kabisa kwa na |
| Kielezi | (sahili) na (sahili) | lo! |
| Kihusishi | lo! (sahili) | |
| Kiunganishi | | |
| Kihisishi | | |

# MUHADHARA 8

# Uambishaji na Mnyambuliko wa Maneno

## 8.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu, tunakusudia kuelezea maana ya uambishaji na mnyambuliko wa maneno. Pia tutajifunza aina za viambishi kwa kutumia mifano ya kutosha. Vile vile tunakusudia kukuelekeza jinsi mnyambuliko wa maneno unavyotokea katika lugha ya Kiswahili.

Kiswahili kina maneno ya aina mbili:

(a) Maneno yasiyobadili umbo lake, nayo ni:

(i) Viunganishi [**U**]: na, kwa katika, nk.

(ii) Vihisishi [**H**]: loo, ewa…, la hasha, nk.

(iii) Vielezi asilia [**E**]: mapema, asubuhi, mbali, sana, nk.

(b) Neno linalobadili umbo lake kwa kuongezewa mofu fulani mwanzoni au mwishoni mwa sehemu fulani katika neno husika; sehemu ya neno huitwa mzizi.

Kwa mantiki hii, maneno yanayoundwa hupewa maana ama mpya, au ya ziada au hata yakageuza hali yake ya asili na kuchukua nafasi nyingine katika muundo wa kishazi; kwa mfano:

(i) chumba [**N**] => chumba**ni** [**E**]

(ii) piga [**T**] => pig**o** [**J**]

(iii) refu [**V**] => refu**sha** [T]

(iv) rahisi [**E**] => rahis**isha** [T]

(v) sawa [**E**] => sawa**zisha** [**T**]

(vi) kadiri [**U**] => kadiri**a** [**T**] => kadir**isha** [**T**]

(vii) karibu [**E**] => karib**ia** [**T**] =>karib**isha**

(viii) **tu**-**ta**-**m**-pig-**an**-**ish**-**a**-**je**? (na marafiki zake) =>[**S**].

Elewa kwamba katika neno, *piga:pig*-ni mzizi wa neno *piga*. *piga* ni shina la neno *piga.Shina* = mzizi + a, yaani

piga = pig + a

(c) Kwa mantiki hiyo hapo juu,

(i) Dhana ya mzizi wa neno inadai kwamba ni sehemu ya neno ambayo huwa haibadiliki licha ya kuongezewa mofu.

(ii) Dhana ya shina la neno inadai kwamba ni jumla ya mzizi + a

Aidha, istilahi zinazotumika ili kuwakilisha dhana/maana na shughuli zote kuhusu mabadiliko ya maneno hayo ni uambishaji na mnyambuliko.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu unatarajiwa kuweza:

- Kueleza maana ya uambishaji na unyambulishaji wa maneno.
- Kutaja aina za viambishi
- Kufafanua dhima za viambishi katika maneno.

## 8.2 Uambishaji

Neno uambishaji linatokana na kitenzi kuambisha ambalo nalo latokana na kitenzi kuamba. Kuamba maana yake ni kukifunga kitu fulani kwenye kitu kingine ili kibakie hapo; au kukinatisha kitu fulani kwenye kitu kingine. Neno kuambisha lina maana ya kukifanya kitu kinate mahali fulani.

Katika Kiswahili, uambishaji unafanyika kwa kuongeza mofu fulani mwanzoni au mwishoni mwa **mzizi** wa neno. Kwa mantiki hii, maneno yanayoundwa hupewa maana ama mpya, au ya ziada au hata yakageuza hali yake ya asili na kuchukua nafasi nyingine katika muundo wa **kishazi.**

Kinachoambishwa huitwa kiambishi ambacho, aghalabu, hubeba maana katika lugha; na kwa mantiki hiyo, kiambishi ni sawa na mofu.

Kwa mfano, katika neno piga, **pig** ni mzizi, na **a** ni kiambishi/mofu ishilizi au tamatishi katika kila kitenzi asilia cha Kiswahili.

Tunaweza kunatisha viambishi kadhaa mwanzoni mwa mzizi **pig** kama ifuatavyo:

tu-ta-m-**pig -** a,

**lakini** pia tunaweza kunatisha viambishi kadhaa mwishoni mwa mzizi uo huo **pig** kama ifuatavyo:

**pig**-an-ish-a

au hata pengine tunaweza kuvinatisha viambishi vya mwanzoni na vya mwishoni mwishoni mwa mzizi huo huo **pig** na kupata tungo kama ifuatavyo:

tu-ta-m- **pig -**an-ish-a; au

tu-ta-m-**pig -** an-ish-a-**je ?** (na wenzake).

## 8.3 Mnyambuliko

Mnyambuliko ni neno ambalo maana yake inatokana na maana ya maneno mawili:

(i) Kunyambua m.y. kata vipande vipande.

(ii) Kunyumbua m.y. vuta na kutanua kitu chororo, mfano kama kamba ya mpira.

Katika sarufi, mnyambuliko ni ule uwezo wa mzizi au shina kuambishwa mofu mwanzoni au mwishoni mwake. Matokeo yake ni kupanua maana ya neno husika. Na hii ni kazi ya kila kiambishi. Kujenga mizizi mipya na mashina mapya ya maneno ambayo huitwa mashina au mizizi ya mnyambuliko. Na hii ni kazi ya viambishi vya mnyambuliko au viambishi vijenzi. Aghalabu, viambishi vijenzi hutokea mwishoni mwa shina au mzizi, na kwa mantiki hiyo, vimeendelea kuitwa viambishi tamati-vijenzi.

Kwa mantiki hiyo, mnyambuliko unahusisha viambishi vya aina mbili:

*(a) Viambishi-Maana,* ambavyo hutokea mwanzoni mwa **mzizi** wa neno. Viambishi hivi vinaweza kutanua maana ya neno bila ya kubadilisha mzizi wa neno.

Kwa mfano:

tu-ta-m-**pig**-an-ish-a.

Tunaona hapa kwamba:

(i) **-pig-** ni mzizi wa neno tutampiganisha.

(ii) **tu-ta-m-** ni viambishi vya mwanzoni mwa mzizi **–pig-**

(iii) **–an-ish-a**ni viambishi vya mwishoni mwa mzizi –**pig-**

Viambishi vya mwanzoni na vile vya mwishoni mwa mzizi -**pig-**vinaleta maana tafauti tafauti kama ifuatavyo:

(i) Kiambishi **tu-** ni cha nafsi ya kwanza wingi (sisi).

(ii) Kiambishi -**ta-** ni cha njeo ijayo.

(iii) Kiambishi -**m-** ni cha kumrejesha mtendwa, nafsi ya tatu, umoja (yeye).

(iv) Kiambishi -**an-** ni cha kutendeana.

(v) Kiambishi **–ish-** ni cha kutendesha.

(vi) Kiambishi **-a-** ni cha kutamatisha kauli

*(b) Viambishi-vijenzi/mnyambuliko* ambavyo hutokea mwishoni mwa **shina** la neno. Viambishi hivi vina kazi tatu:

(i) kutanua maana ya neno

(ii) kujenga mzizi au shina la mnyambuliko

(iii) Kubadilisha neno kutoka aina moja na kuingia katika aina nyingine ya neno.

Kwa mfano:

(i) Kutanua Maana na Kujenga Mzizi na Shina la Mnyambuliko

| **Kitenzi** | **Mzizi** | **Shina** | **Mnyambulisho** | **Mzizi wa Mnyambulisho** | **Shina** |
|---|---|---|---|---|---|
| piga | pig- | piga | pigana | pigan- | pigana |
| cheza | chez- | cheza | chezeka | chezek- | chezeka |
| imba | imb- | imba | imbisha | imbish- | imbisha |
| ruka | ruk- | ruka | rukana | rukan- | rukana |
| lima | lim | lima | limika | limik- | limika |

(ii) Kubadilisha Neno Kutoka Aina Moja na Kuingia Katika Aina Nyingine ya Neno

**Mfano:**

(i) *ku*-omba = omboleza

=ombolez- (=mzizi wa mnyambulisho)

= ombi, ombolezo (= majina) (ii) *ku*-sifu = sifia; sifiana.

= sifa, wasifu (= majina).

Aghalabu, *viambishi-vijenzi* hutokea mwishoni mwa shina na kwa mantiki hiyo, huitwa *viambishi tamati-vijenzi*.

## 8.4 Aina za Viambishi

Ziko aina kuu tatu za viambishi vinavyonatishwa kwenye mzizi, nazo ni:

***(i) Viambishi awali***

Kati ya hivi Viambishi vya mwanzoni mwanzoni mwa mzizi, kuna:

(a) kile cha kwanza kabisa ambacho kiko mbali na mzizi ambacho hujulikana ama Kiambishi-Ngeli, au
Kiambishi cha Idadi, au Kiambishi Nafsi (mtenda, mtendwa au mtendewa).

(b) kile cha kwanza kabisa kinachogusana na mzizi.

(c) kile kilichoko/vile vilivyoko kati ya kile cha kwanza kabisa ambacho kiko mbali na mzizi na kile cha kwanzakabisa kinachogusana na mzizi.

Kwa mfano, katika neno tutampiganisha (= tu-ta-m -pig - an-ish-a) :

- tu-ta-m- ni viambishi vya mwanzoni mwanzoni mwa mzizi, -pig-.
- tu- ni kiambishi cha kwanza kabisa ambacho kiko mbali na mzizi, -pig-, (mtenda).
- -m- ni kiambishi cha kwanza kabisa kinachogusana na mzizi, -pig-, (mtendwa).

(d) -ta- ni kiambishi kilichoko kati ya kile cha kwanza kabisa ambacho kiko mbali na mzizi na kile cha kwanza kabisa kinachogusana na mzizi, -pig, (njeo ijayo).

***(ii) Viambishi Tamati***

Kati ya hivi Viambishi tamatii, kuna:

(a) kile cha mwisho kabisa ambacho kiko mbali na mzizi na ambacho aghalabu huitwa kiambishi tamatishi.

(b) kile cha mwisho, lakini cha kwanza kugusana na mzizi.

(c) kile kilichoko/vilivyoko kati ya kile cha mwisho kabisa ambacho kiko mbali na mzizi na kile cha mwisho, lakini cha kwanza kugusana na mzizi.

Kwa mfano, katika neno tutampiganisha (tu-ta-m -pig - an-ish-a)

- -an-ish-a ni viambishi vya mwishoni mwishoni mwa mzizi, -pig-.
- -a ni kiambishi cha mwisho kabisa ambacho kiko mbali na mzizi, -pig-, (kiyakinishi cha kauli).
- -an- ni kiambishi cha kwanza kabisa kinachogusana na mzizi, -pig-, (kitendeana cha kauli).
- -ish- ni kiambishi kilichoko kati ya kile cha mwisho kabisa [a} ambacho kiko mbali na mzizi na kile cha kwanza kabisa {an} kinachogusana na mzizi, -pig-, (kitendea cha kauli).

## 8.5 Dhima ya Viambishi Katika Neno

Viambishi vya mnyambuliko vyote hubadili sana hali na tabia ya neno, kama ifuatavyo:

**(a)** Jinsi kitenzikinavyozidi kupokea viambishi vya mnyambuliko, ndivyo kitenzikinavyozidi kujijengea mizizi na mashina mapya.

**Kwa mfano:**

| Kitenzi | Mzizi | Shina | Mnyambulisho | Mzizi wa Shina | Mnyambulisho |
|---|---|---|---|---|---|
| piga | pig- | piga | pigana | pigan- | pigana |

Aidha, kitenzi hicho hicho kinaweza kujengeka upya na kupata hali na tabia za kipashio kipya, kama vile nomino:

| **Kitenzi** | **Nomino** |
|---|---|
| pig-a | (i) pig-o, |
| | (ii) ma-pig-o, |
| | (iii) pig-an-o, |
| | (iv) ma-pig-an-o. |

(b) Viambishi vya mnyambuliko huyafanya maneno yabadili asili yake ya kipashio na kuwa kipashio kipya na kupokea tabia na hali zote za kipashio hicho kipya, kwa mfano:

(i) mtulivu (N) => tuli-a (T) => tulizan-a (T) => tulivu (V) => mtulizaji (N) =>tuli (E).

(ii) msafishaji (N) =>safisha (T)=>safishan-a (T) => safi (V).

(iii) mkaribishaji (N) => karibi-a (T) => karibish-a (T) => karibishan-a ( T) => karibish-o (J )

(iv) sawa (V) => sawazish-a (T) => sawazish-o(N).

(c) Baadhi ya vivumishi hupokea kiambishi awali ki- au vi- na kuweza kufanya kazi ya kielezi, kwa mfano:

(i) zuri (V) => vi-zuri;

(ii) ema (V) => vy-ema, v-ema;

(iii) kubwa => ki-kubwa.

## 8.6 Hitimisho

Baada ya kuelezea uambishaji, mnyambuliko, aina ya viambishi, hali na tabia ya neno, tunafikia muafaka wa kuielezea mofolojia ya mofu kwa kielezo kifuatacho:

## M O F U

| **Mofu-Huru** | **Mofu-Tegemezi** | |
|---|---|---|
| **Neno-Huru** | **Mofu-mwanzoni** | **Mzizi** **Mofu-Mwisho** |
| adui | a-na-tu | **pig** an-ish-a |

## Zingatia

(a) Dhana ya Neno:
Neno ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa ili kuleta maana.

(b) Uambishaji
Uongezaji wa mofu Fulani Fulani mwanzoni au mwishoni mwishoni mwa mzizi wa neno.

(c) Kiambishi
Dhana ya Kiambishi cha Mzizi inadai kwamba ni mofu-tegemezi inayoambishwa kwenye mzizi wa neno.

(d) Viambishi awali (mwanzoni) vya mzizi wa neon katika neno.

(e) Viambishi tamatii (mwishoni) vya mzizi wa neon katika neno.

## Zoezi

1. Kwa kutumia mifano eleza maana ya istilahi zifuatazo: (i) Neno (ii) Mzizi.
2. Kwa kutumia mifano eleza tofauti kati ya maneno ya yafuatayo:
   (i) Mofu-huru na mofu-tegemezi
   (ii) Mofu na viambishi
   (ii) Mzizi na shina
   (iii) Viambishi vya mwanzoni mwanzoni na viambishi vya mwishoni mwishoni mwa *mzizi*.
3. Bainisha *mofu* katika maneno yafuatayo na eleza *uamilifu (kazi)* wa kila mofu.
   (i) Kitakachopatikana (ii) Kikikitangulia
   (iii) Hawajapendekezwa (iv) Sitakuamsha
   (v) Ulinisahihishia (vi) Aliyekunong'oneza
   (vii) Akijikinga (viii) Asiyekujua
   (ix) Someka (x) Msichokijua
   (xii) Kikuingiacho.
4. Kwa kutumia mifano, eleza dhamira na onesha matumizi sahihi ya viambishi vi fuatavyo katika sentensi:
   (i) -ngeli-
   (ii) -ngali-
   (iii) -nge-
   (iv)-ki-

## Marejeo


1. Mgullu, Richard, S. (1999),*Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*,
2. Rubanza, Y. I. (1996), *Mofolojia ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
3. TUKI (1990), *Kamusi Sanifu Ya Isimu Na Lugha.* Dar es Salaam: TUKI

# MUHADHARA 9

# Mawanda ya Sintaksia

## 9 .1 Utangulizi

Katika taaluma inayochunguza lugha, ambayo hujulikana kama isimu, lugha hugawanywa katika Nyanja kuu nne ambazo ni *fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki*. Hivyo, sintaksia ni nyanja mojawapo ya isimu ya lugha. *Sintaksia ni nini?*

## Madhumuni ya Muhadhara

Malengo makuu ya muhadhara huu mwanafunzi ataweza:

(i) Kueleza mawanda ya Sintaksia;

(ii) Kueleza maana ya muundo kisintaksia;

(iii) Kutambua kategoria za kileksia na kidhima:

(iv) Kutambua kategoria kwenye ngazi ya Virai\

## 9.2 Fasili ya Sintaksia

Kwa mujibu wa Harper (2001-2010) *Online Etymology Dictionary*, neno sintaksia liliibuka takribani miaka ya 1600 na linatokana na neno la Kifaransa *syntaxé* au la Kilatini au Kigiriki *syntaxis* ambalo maana yake ni kupanga au kuweka vitu pamoja katika mpango. Hata hivyo, wataalamu wengi wa masuala ya sintaksia wanakubaliana kuwa neno hili lina asili ya Kigiriki kwa kuwa Wagiriki ndio wakongwe katika taaluma mbalimbali hapa duniani, ikiwa ni pamoja na taaluma ya lugha. Hata hivyo historia ya isimu inaonesha kuwa, uchunguzi wa kwanza wa lugha ulianza na Wamisri mnamo karne ya 5 Kabla ya Kuzaliwa Kristo (KK), Wagiriki ndio walioweka msingi wa taaluma ya lugha tuijuavyo hivi leo (Khamis & Kiango, 2002: 1).

Katika taaluma za sayansi ya kompyuta, sintaksia ni kanuni zifafanuazo jinsi alama zitumikazo katika lugha ya kikompyuta zinavyounganishwa pamoja kwa mpangilio unaokubalika kuwa ni muundo sahihi katika lugha hiyo ya kikompyuta (Programming Language).

Katika kozi hii hatutahusika na mpango wa vitu kwa ujumla wake wala kanuni fafanuzi za matumizi ya maneno na virai katika lugha ya kikompyuta, bali tutajikita zaidi katika taaluma ya isimu. *Kwa hiyo, sintaksia ni nini katika taaluma ya isimu?*

Besha (1994: 84), sintaksia ni taaluma inayojihusisha na uchambuzi na ufafanuzi wa muundo wa sentensi za lugha; kwa mujibu wa O'Grady (1996: 181), sintaksia ni taaluma inayochunguza jinsi maneno yanavyounganishwa ili kuunda sentensi. Sintaksia kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2009: 34) ni, "Utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake." Wanaendelea kusema kuwa katika utanzu huu kinachochunguzwa ni zile sheria au kanuni ambazo hazina budi kufuatwa katika kuyapanga maneno ya lugha katika mfuatano (neno moja baada ya jingine) kwa namna ambayo itayafanya maneno hayo yalete maana inayokubalika na kueleweka katika lugha husika.

Fasili hizi chache tumezitoa kama mifano tu ya kushadidia hoja ya kwamba kuna fasili nyingi za sintaksia. Pamoja na kuwapo kwa fasili nyingi, mtu akichunguza atagundua kwamba fasili takriban zote zinabainisha kuwa sintaksia ni tawi la isimu linalojihusisha na uchunguzi wa:

(a) Jinsi maneno yanavyopangwa katika tungo

(b) Kanuni au taratibu za lugha zinazotumika na zinavyotumika katika kuyaweka maneno hayo pamoja

Kwa hiyo, sintaksia inaweza kufasiliwa kuwa ni taaluma inayochunguza miundo ya tungo na kanuni mbalimbali za lugha zinazotawala miundo hiyo. Katika uchunguzi huo, sintaksia huhusika na mpangilio wa maneno katika miundo mitatu iliyopangwa kidarajia, yaani jinsi maneno yanavyopangwa ili kuunda virai, vishazi na sentensi.

## 9.3 Malengo ya Ufafanuzi wa Kisintaksia

Lengo kuu la ufafanuzi wa kisintaksia ni kupata sarufi inayotosheleza kwa usahihi miundo ya lugha. Hivi ni kusema, wanasintaksia hufafanua miundo ya sintaksia wakiwa na shabaha ya kupata njia sahihi na toshelevu zitakazosaidia kupata miundo sahihi na kukataa miundo isiyo sahihi katika lugha.

Tangu awali taaluma ya lugha ilipoanzishwa, enzi za Wagiriki na Walatini, kumekuwa na mbinu mbalimbali za uchanganuzi wa mfuatano wa vipashio katika muundo wa mlalo. Kwa mfano, sentensi:

1. Mtoto ana bahati

   Ni sentensi sahili ambayo ni sahihi. Ni utungo ambao una maneno yaliyopangwa kimlalo kwa kufuata sulubu maalumu. Maneno hayohayo yaliyotumika katika sentensi (1) yanaweza kupangwa vinginevyo na kutupatia miundo mbalimbali sahihi na isiyo sahihi. Mathalan:

2. Bahati ana mtoto
2. Ana bahati mtoto
3. *Mtoto bahati ana
4. *Ana mtoto bahati

Vivyo hivyo, sentensi:

5. Tukiwa tunakula, nitakwambia vitu

Kimsingi hii, ni sentensi changamano, ni utungo ambao una maneno yaliyopangwa kwa kufuata sulubu maalumu. Maneno hayohayo yaliyotumika katika sentensi (6) yanaweza kupangwa vinginevyo na kutupatia miundo mbalimbali sahihi na isiyo sahihi kama vile:

6. Tukiwa tunakula vitu, nitakwambia
7. Nitakwambia, tukiwa tunakula vitu
8. *Tunakula vitu, nitakwambia tukiwa
9. *Tukiwa nitakwambia vitu tunakula

Sentensi zisizo na alama ya kinyota zimefuata sulubu inayokubalika katika lugha ya Kiswahili na kwa hiyo ndizo sentensi sahihi na zile zenye alama hiyo hazikufuata sulubu hiyo na kwa hiyo si sahihi. Je, tunajuaje kuwa sentensi hizi sahihi ni sahihi na nyingine zisizo sahihi si sahihi?

Tukitaka kujua usahihi na utosahihi wa tungo hizo, tunahitaji njia za uchanganuzi zitakazotupatia mbinu ya kujua mfuatano fulani wa vipashio katika tungo sahihi na zisizo sahihi kuzikataa. Lengo la wanasintaksia, ambalo hasa ndilo lengo la ufafanuzi wa kisintaksia, siku zote limekuwa ni kutafuta njia hizo za kuzikubali sentensi sahihi na kuzikataa sentensi zisizo sahihi. Njia hizo za kufanyia uchanganuzi wa sentensi ndizo huitwa **sarufi** (kwa maana yake finyu). Je, mwanasintaksia anafikiaje hatua ya kupata sarufi ya lugha inayohusika?

Kwanza, mwanasintaksia huchambua na kueleza maarifa aliyo nayo mjua lugha kuhusu miundo ya lugha yake. Na pili, huunda nadharia kulingana na ugunduzi wake kuhusiana na maarifa hayo ya mjua lugha.

## Zoezi

1. Sintaksia ni nini?
2. Lengo kuu la ufafanuzi wa kisintaksia ni lipi

## Marejeo


1. Besha, R.M. (1994) *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
2. Crystal, D. (1989) *Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.
3. Khamisi, A.M (2008) *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.
4. Massamba, D.P.B. na wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.
5. O'Grady, W. na wenzake (1997) *Contemporary Linguistics. An Introduction Language*. London: Longman.

# MUHADHARA 10

## Kategoria za Kisintaksia na Ushahidi wa Kuwepo Kwazo

## 10.1 Utangulizi

Katika mhadhara uliopita tulipokuwa tunafasili dhana ya sintaksia tulidokeza kuwa sintaksia huchunguza jinsi maneno yanavyopangwa katika tungo. Jambo hili linatuambia kuwa katika lugha kuna maneno. Maneno hayo katika kila lugha hayajakaa kivoloya bali huwa yanahusiana kiasi cha kuweza kuwekwa katika makundi madogo. Akishadidia hoja hii, O'Grady, (1996: 182) anaeleza kuwa

Ukweli wa msingi kuhusu maneno katika lugha zote za binadamu ni kwamba yanaweza kuwekwa katika makundi madogo zaidi yajulikanayo kama kategoria za kisintaksia. Kauli hii ya O'Grady inatuingiza katika udadisi wa kutaka kujua maana ya kategoria. Hivyo, tunajiuliza, "Kategoria ni nini?" Kusudi la muhadhara huu ni kujaribu kufasili dhana ya kategoria na kuangalia kama kweli kategoria zipo au la.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu unatarajiwa kuweza:

- Kufafanua dhana ya kategoria
- Kutaja kategoria za kisintaksia
- Kueleza ushahidi wa kuwepo kwa kategoria za kileksika

## 10.2 Dhana ya Kategoria

Kwa mujibu wa Khamisi na Kiango (2002: 9) dhana ya kategoria ilitumiwa na wanasarufi mapokeo kwa namna tofauti na inavyotumiwa na wanasarufi mamboleo. Neno kategoria kama lilivyotumika

katika sarufi mapokeo ya akina Aristotle limetokana na neno la Kigiriki na kutafsiriwa kama uarifu (predication). Wao walitumia dhana ya kategoria kuwa ni sifa bainifu, yaani zile sifa zinazoambatana au zinazoambikwa kwenye aina za maneno kama vile idadi, nafsi, kauli, ngeli, njeo, dhamira na uhusika.

Kategoria kwa mtazamo wa kisarufi mamboleo ni jamii, seti, kundi au makundi ya maneno yanayofanya kazi ya kufanana. Aidha, darajia yoyote ya vipashio inayotambuliwa katika uchambuzi wa lugha fulani huitwa **kategoria**.

Kwa sasa kategoria zipo katika viwango au darajia tatu: kiwango cha neno, kiwango cha kimuundo au kirai na kiwango cha kidhima. Kategoria hizi tatu zinajulikana kwa majina ya:

- Kategoria za kileksika
- Kategoria za virai
- Kategoria za kidhima

### 10.2.1 Kategoria za Kileksika

Kategoria za kileksika ni kategoria za kiwango cha neno moja moja. Wataalamu mbalimbali wametofautiana katika idadi na istilahi za kategoria hizo. Kuna wanaotaja kategoria nne (tazama O'Grady, 1996: 182), saba (tazama Nkwera, 1978; Kapinga, 1983) na nane (tazama Kihore, 1996). Kategoria za kileksika zilizoainishwa mpaka sasa ni hizi zifuatazo:

***Kategoria Mifano***

(a) Nomino (N): Masanja, kijana, mtu, kitabu, vumbi, maziwa, utoto, ugonjwa n.k.

(b) Kitenzi (T): tembea, sema, totoa, ugua, kuwa n.k.

(c) Kivumishi (V): (-)dogo, -eusi, (-)zito, zuri n.k.

(d) Kihusishi (H): cha, katika, la, tena, hadi n.k.

(e) Kielezi (E): kijinga, vizuri, kabisa, sana, hasa, wima n.k.

(f) Kiwakilishi (W): mimi, wao n.k.

(g) Kiunganishi (U): na, lakini, ila, au, ama n.k.

(h) Kibainishi (B): yule, huyu, hawa n.k.

(i) Kiingizi/Kihisishi (K): abe!, naam!, hebu! n.k.

Kama tulivyobainisha kuhitilafiana kwa wataalamu juu ya ukategorishaji wa maneno, O'Grady (1996: 182) anaona kuwa kategoria za kileksika ni (a) mpaka (e) tu na kategoria zinazobaki ni kategoria zisizo za kileksika au ni kategoria za kidhima kwa kuwa maana za vipashio hivyo si rahisi kufasilika au kuelezeka. Aidha, katika kategoria za virai, ni kategoria za (a) mpaka (e) tu ndizo hutokea kama maneno makuu ya virai husika.

Kuna mkanganyiko unaoweza kujitokeza kuwa kuna maneno yanayoweza kuwa katika kategoria zaidi ya moja. Je, ni vigezo gani vinatumika ili kubaini kategoria za maneno? Vigezo vinavyotumika kubaini kategoria za maneno ndizo hutumiwa pia kama ushahidi wa kuwapo kwa kategoria katika lugha.

## 10.3 Ushahidi wa Kuwapo kwa Kategoria za Kileksika

Ushahidi unaounga mkono kuwapo kwa kategoria za kileksika ni wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki.

### 10.3.1 Ushahidi wa kifonolojia

Katika ushahidi huu kigezo kinachotumiwa ni mkazo au shadda. Neno moja linakuwa katika kategoria tofauti kutokana na uwekaji wa mkazo. Tutazame mifano ifuatayo:

1) Wafanyakazi wote wamejenga baraBAra

2) Kazi zote zimefanyika baRAbara

3) We need to imPORT new technology

4) We need an IMport of new technology

Katika mifano hiyo hapo juu, neno la mwisho katika sentensi 1) ni nomino na katika sentensi 2) ni kielezi. Katika sentensi 3) neno la nne ni kitenzi na neno hilohilo katika sentensi 4) ni nomino. Maneno ni yaleyale lakini yamekuwa katika kategoria tofauti kutokana na uwekaji wa mkazo mahali tofauti. Kwa hiyo, mkazo unathibitisha kuwapo kwa kategoria za kileksika. Unathibitisha kuwa kuna kategoria mbili za neno moja. Hapa tunaona kuwa kanuni fulani za kifonolojia lazima zijue taarifa za kikategoria kabla ya kutumika. Kwa hiyo, tunahitimisha kwa kusema kwamba lile dai la O'Graddy (1996) la kwamba maneno yamegawanyika katika makundi mbalimbali lina ukweli ndani yake.

### 10.3.2 Ushahidi wa kimofolojia

Katika ushahidi huu kinachoangaliwa ni uambikatizi. Viambishi fulani vya kisarufi huweza kuambikwa kwenye maneno yaliyo katika kategoria fulani tu na haviwezi kuambikwa kwenye maneno ya kategoria tofauti.

Kwa mfano, O'Graddy (1996) anasema katika lugha ya Kiingereza kiambishi cha wingi –s huambikwa kwenye maneno ya kategoria ya nomino, kiambishi cha njeo iliyopita –ed na cha hali ya kuendelea huambikwa kwenye vitenzi, na viambishi vya ukadirifu *-er, -est* huambikwa kwenye vivumishi. Vivyo hivyo, katika lugha ya Kiswahili, viambishi vya idadi na ngeli huambikwa katika nomino na vivumishi, viambishi vya njeo, kauli, na usababishi huambikwa katika vitenzi n.k.

### 10.3.3 Ushahidi wa kisintaksia

Hapa kigezo kinachotumika na ambacho yasemekana ndicho kinachoaminika zaidi (O'Grady, 1996: 184) ni kile cha mtawanyo. Tunaangalia nafasi ambayo maneno yanachukua katika tungo.

Kwa mfano, maneno ya kategoria ya nomino ndiyo yanayoweza kuchukua nafasi iliyo wazi katika utungo ufuatao:

___________ anaweza kuwa mnyama hatari sana.

Simba

Chui

Nyoka n.k.

### 10.3.4 Ushahidi wa kisemantiki

O'Grady (1996: 183) anasema kuwa kigezo kinachohusika hapa ni maana. Kwa maneno mengine, tunajua kuwa neno fulani liko katika kategoria fulani kutokana na linavyofasiliwa. Kwa mfano:

Nomino: maneno yanayotaja vitu

Vitenzi: maneno yanayotaja vitendo

Vivumishi: maneno ambayo hutaja sifa za nomino

Vielezi: maneno ambayo hueleza namna ambavyo tendo linafanyika

Vihusishi: maneno yanayohusisha

Vibainishi: maneno ambayo huweka vitu bayana

Tutakubaliana sote kuwa kigezo hiki hakiwezi kuwa cha kuaminika sana. Kunaweza kuwa na mapungufu mengi mtu akitumia fasili katika kuchanganua kategoria za maneno. Tuangalie mifano michache ya maneno kutoka lugha ya Kiingereza.

-  "Assasination" linaonyesha hali ya kutenda lakini ni nomino
-  "Fast food" katika neno ambatano hili, neno "fast" linadokeza namna ambavyo chakula kinavyotengenezwa (haraka haraka). Kwa jinsi hii neno fast linaonekana kuwa ni kielezi ilhali ni kivumishi.Aidha, kategoria ya vivumishi inaweza kuwa ngumu kuibainisha ikiwa peke yake kwa sababu Huweza kuwa kiwakilishi.

Kigezo kizuri kinachofaa kutumika katika ushahidi wa kisemantiki ni utata. Utata ndicho kigezo kizuri cha kuonyesha kuwa maneno yana kategoria mbili au zaidi. Utata ni kipengele kinachodhihirisha tafsiri zaidi ya moja. Yaani ni hali ya kipashio kimoja kuwa na maana zaidi ya moja. Upo utata wa kileksia na wa kimuundo. Katika utata wa kileksia, leksimu au neno moja linakuwa na maana zaidi ya moja.

**Kwa mfano:**

*Kaa*

1. Mnyama wa majini, gegeleka (Nomino)
2. Kijinga cha moto (Nomino)
3. Keti (Kitenzi)

*Panda*

1. Tia mbegu ardhini (Kitenzi)
2. Jamiiana (Kitenzi)
3. Kwea (Kitenzi)
4. Njia iliyogawantika (Nomino)

Katika utata wa kimuundo, tafsiri zaidi ya moja zinaibuka kutokana na jinsi utungo ulivyotungwa.

**Kwa mfano:**

Hali halali

N V: Hali ambayo si haramu; ile inayoturuhusu kufanya jambo fulani

T T: Hawezi kula wala kulala

## 10.4 Hitimisho

Kutokana na ushahidi wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki, ni dhahiri kuwa maneno hugawika katika makundi mbalimbali madogo zaidi kama ilivyodaiwa na O'Grady (1997).

### Zoezi

**1.** Taja kategoria za kisintaksia

**2.** Je,kuna ushahidi wa kuwepo kwa kategoria za kisintaksia ? Tumia mifano anuai

### Marejeo


1. Besha, R.M. (1994) *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
2. Crystal, D. (1989) *Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.
3. Khamisi, A.M (2008) *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.

   Massamba, D.P.B. na wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo.* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.
4. O'Grady, W. na wenzake (1997) *Contemporary Linguistics. An Introduction Language.* London: Longman.
5. Radford, A. na wenzake (1999) *Linguistics. An Introduction*. London: CUP.

# MUHADHARA 11

# Kategoria za Virai

## 11.1 Utangulizi

O'Grady (1996: 185) anaeleza kuwa sentensi haziundwi kwa kuweka tu maneno pamoja katika mkururo kama mtungo wa shanga. Bali zina muundo wa kidarajia ambamo maneno huwekwa pamoja kuunda vipashio vya kimuundo vilivyovikubwa zaidi. Anachotuambia hapa O'Grady ni kwamba katika kategoria za kileksika tulizozitaja, watumiaji wa lugha wanaweza kuchukua maneno ya kategoria moja na kuyaweka pamoja na maneno ya kategoria nyingine ili kuunda kikundi cha maneno. Aidha, O'Grady anatuhadharisha kwamba maneno hayo hayawekwi tu kama shanga kwenye mtungo wake. Bali maneno ambayo yanahusiana tu ndiyo huwekwa pamoja. Mathalan, **nomino** inaweza kuhusishwa na **kivumishi** ikatupatia **kikundi nomino**. Vikundi vya maneno kama hiki ndivyo hujulikana kama virai. Kama yalivyo maneno katika lugha, virai navyo hugawanyika katika kategoria mbalimbali ambazo ndizo wanasintaksia huziita kategoria za virai. Mhadhara huu unahusika na kategoria hizo za virai.

## Madhumuni ya Muhadhara

Mwishoni mwa mhadhara huu mwanafunzi ataweza:

i Kufasili dhana ya kirai

ii Kuainisha kategoria mbalimbali za virai

iii Kufafanua sifa za kila kirai

iv Kutoa ushahidi wa kiisimu unaoonyesha kuwapo kwa kategoria za virai katika lugha

## 11.2 Dhana ya Kirai

Ama kuhusu dhana ya kirai, wataalamu mbalimbali wanahitilafiana kiistilahi na fasili zao. Kuna wanaoita kirai (tazama Nkwera, 1978; Matei, 2008; Massamba na wenzake, 2009) na kuna wanaoita kikundi (tazama Mdee, 2007). Katika kutalii na kupekuapekua maandiko kadha wa kadha, tumekutana na fsili hizi:

-  Kirai ni kifungu chochote cha maneno, kuanzia maneno mawili, chenye kuleta maana fulani, ambacho lakini kinaposimama peke yake hakina kiima wala kiarifu; na chenyewe pekee si kiima wala kiarifu (Nkwera, 1978)
-  Kirai ni fungu la maneno ambalo hufanya kazi kama neno moja. Kirai hudokeza maana lakini maana hiyo si kamili...na hakina muundo wa kiima-kiarifu (Matei, 2008)
-  Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima kiarifu (Massamba na wenzake, 2009)
-  Kikundi hujengwa na maneno mawili au zaidi yasiyo na kiima wala kiarifu ambayo husimama sambamba katika tungo (Mdee, 2007).

**Katika fasili hizi kunajidhihirisha mitazamo miwili:**

-  Kuna wanaoona kirai ni kipashio kinachoanzia maneno mawili.
-  Kuna wanaoona kuwa kira kinaweza kuwa neno moja

Aidha, wengi wao wanaona

-  Kirai ni aina ya tungo isiyojitosheleza kimaana.
-  Kirai ni kifungu cha maneno kisichokuwa na muundo wa kiima na kiarifu.

Hivi ni kusema kirai chaweza kuwa kiima au kiarifu. Hivyo ni kipashio cha kimuundo kikubwa kuliko neno na kidogo kuliko kishazi au sentensi. Kwa mfano,

1. Mwalimu msanii anafundisha sintaksia
   **K** **A**
2. Mpishi wa ndizi anaumwa na njaa
   **K** **A**

Kwa hiyo, katika sentensi hizo mbili, vifungu vya maneno vilivyowekwa juu ya msimbo **K** ni virai na vilivyo juu ya msimbo **A** ni virai pia.

## 11.3 Muundo wa Kirai

Wataalamu wengi wanakubaliana kwamba kirai ni kipashio cha mimuundo ambacho kinaundwa na sehemu kuu mbili ambazo ni: (i) neno kuu; na(ii) kijalizo

***Neno kuu ni nini?***

Akitumia mfano wa ndoano, O'Grady (1996: 185) anaeleza kuwa vishazi hujengwa katika kiunzi chenye viwango viwili kama inavyoonyeshwa katika kielelezo hiki hapa chini (msimbo K ukisimama badala ya kirai):

KN KT KV KE KH ← kiwango cha kirai
| | | | |
N T V E H ← kiwango cha neno

Anaendelea kusema kuwa kila kiwango cha muundo wa kirai kinaweza kufikiriwa kama ndoano fulani ambapo vipashio vya aina aina vinaweza kupachikwa. Kiwango cha chini kabisa ni kwa ajili ya neno ambalo

kwalo kirai ndio hujengwa – N kwa upande wa KN, T kwa upande wa KT, V kwa upande wa KV, E kwa upande wa KE na H kwa upande wa KH. Kipashio hiki ndicho huitwa **neno kuu**. Kwa hiyo, kutokana na maelezo ya O'Grady, tunaweza kusema kuwa **Neno kuu ni neno linalotawala kirai chote**. Neno kuu linachukuliwa kuwa linatawala kirai kwa kuwa linaweza kutokea peke yake katika kirai kama mifano ifuatayo invyoonyesha:

1) KN
N
(Anapenda) **vitabu**
(Watoto wamefanya) **mtihani**

2) KT
T
(viumbe hai wote) **hula**
(Simu yako) **inaita**

3) KV
V
(Huu ni mchezo) **mgumu**

4) KE
E
Wewe unapika) **vizuri**

Hata hivyo, katika sarufi ya Kiswahili, neno kuu la kirai kihusishi, kama inavyoonekana katika mfano wa 5 hapa chini, haliwezi kujitosheleza likiwa peke yake bila kijalizo chake.

5) KH
*(Watakuja chuoni) kwa
(Watakuja chuoni) kwa gari
Kwa hiyo, ingawa ni kweli kwamba neno kuu huweza kuwa peke yake katika kirai, muundo wa kirai kihusishi hutofautiana na miundo ya virai vingine kwa sababu neno kuu la kirai kihusishi halijitoshelezi kimuundo bila kijalizo chake.

***Kijalizo***

Kijalizo ni kile kipashio kinachojalizia/kamilisha neno kuu. Kwa mfano, katika mfano wa 5 hapo juu, nomino ***gari*** ni kijalizo cha kihusishi ***kwa.*** Kijalizo kinaweza kuwa neno moja au kifungu cha maneno mawili au zaidi. Katika kirai, neno kuu hutangulia na kijalizo chake hufuatia.

Kutokana na muundo huu wa kirai, tunaweza kuzikataa fasili zote za kirai zinazodai kuwa kirai ni kifungu cha maneno mawili au zaidi kwa kuwa imedhihiri kuwa kirai kinaweza kuundwa na neno kuu peke yake. Hivyo, kirai kinaweza kufasiliwa kuwa ni neno au kifungu cha maneno kinachotawaliwa na neno-kuu moja.

## 11.4 Aina za Virai

Kwa kawaida, katika uainishaji wa virai, kategoria ya neno kuu ndiyo hutumiwa kutambulisha aina ya kirai kinachohusika. Kwa hiyo, kama ambavyo tuliona katika mifano 1 – 5 hapo juu, tuna aina zifuatazo za virai.

1) Virai nomino (KN)

2) Virai vitenzi (wengine huviita virai tenzi) (KT)

3) Virai vivumishi (wengine huviita virai vumishi) (KV)

4) Virai vielezi (wengine huviita virai elezi) (KE)

5) Virai vihusishi (wengine huviita virai husishi) (KH)

Hata hivyo, wapo wataalamu ambao hawaungi mkono idadi hii ya virai. Wao wanaona vipo pugufu. Kwa mfano, Mdee (2007) anatambua kuwapo kwa aina tatu za virai: vikundi nomino, vikundi vitenzi na vikundi vielezi lakini anapoviainisha anaona kuna aina mbili tu za virai: kikundi nomino na kikundi kielezi. Nkwera (1989) naye anatambua kuwapo kwa aina tatu tu za virai: virai vya nomino, virai vya vivumishi na virai vya vielezi. Si lengo letu kuhoji usahihi au upotofu wa mtazamo wa Mdee na Nkwera. Tunachoweza kusema tu hapa ni kwamba mtazamo wao kwa sasa unakosa mashiko kwa kuwa utafiti umethibitisha kuwapo kwa virai vingi zaidi ya hivyo vinavyotajwa na watu hawa.

Aidha, wapo wataalamu wengine ambao wana idadi hii ya aina tano za virai lakini hawajumuishi aina zingine tulizozitaja hapo juu. Mathalan, Massamba na wenzake wana virai viunganishi lakini hawana virai vihusishi.

Tutajaribu kuvipitia kwa ufupi virai tulivyovibainisha hapo juu aina moja baada ya nyingine.

### *1) Kirai nomino*

Neno kuu la kirai nomino ni nomino. Vijalizo vyake vinaweza kuwa vikumushi mbalimbali kama vile vivumishi (mwalimu mgeni, ugonjwa hatari), au virai vivumishi (mwanamke mwenye maziwa makubwa sana), virai viunganishi (mama *na mwana*, mume *na mke*), virai vihusishi (mpishi wa shule, safari ya ndege, suala la kijinsia), sentensi (mwalimu aliyetufundisha mwakajana), na muunganiko wa vikumushi kama vivumishi, vionyeshi na sentensi (mtoto wako yule mzuri uliyemtuma kukuleta kuni jana).

Kidhima, kirai nomino kinaweza kuwa kiima, yambwa, yambiwa, kijalizo cha kirai kihusishi na kinaweza kukaa mahali pengine popote ambapo nomino inakaa.

**Kwa mfano**

Walimu wakuu waliwapa wanafunzi wao wote vyeti vyao kwa siku moja

Kiima yambiwa yambwa kijalizo cha KH

***2) Kirai kitenzi***

Neno kuu la kirai kitenzi ni kitenzi. Vijalizo vyake vinaweza kuwa kitenzi (ilikuwa inanyesha) kirai nomino (anapika ndizi, utawapenda watu wote), kirai kihusishi (anacheza kwa magongo ya miti, atasafiri kwa ndege), kirai kielezi (usisogee huko, wanacheza vizuri mno) na sentensi (anafundisha alivyotufundisha mwaka jana).

Kidhima, kirai kitenzi kinaweza kuwa kiarifu.

***3) Kirai kivumishi***

Neno kuu la kirai kivumishi ni kivumishi. Vijalizo vyake vinaweza kuwa vikumushi vyake mbalimbali kama vile vivumishi (mrefu mweusi, mweusi mtanashatitanshati), virai vielezi (mzuri mno, mwembana sana), virai nomino (mwenye kipara kipana), virai vihusishi (mlimbwende wa Tanzania, mtoro wa mwaka), na sentensi (mtundu anayewahangaisha polisi).

Kidhima, kirai kivumishi kinaweza kuwa kikumushi cha kirai nomino (mtoto mdogo mjanja), kiima cha sentensi (wadogo wote wamesonga mbele).

***4) Kirai kielezi***

Kirai kielezi ni kirai ambacho neno lake kuu ni kielezi. Vijalizo vyake vinaweza kuwa vielezi vingine (vizuri sana, kwa mfano katika: umesoma vizuri *sana*, ughaibuni *milele*, kwa mfano katika nakwambia wewe hutafika ughaibuni *milele*), virai vihusishi (usiku *wa manane,* ofisini *kwa mwalimu wangu*), vivumishi (shuleni *kwetu*).

Kidhima kirai kielezi kinaweza kuwa kikumushi cha kirai kitenzi (anatembea *kibatabata*, wameimba *kishamba mno*), kiima cha sentensi (nyumbani kwao kuna wageni, kibatabata ni mwendo wanaotembea walimbwende majukwaani).

***5) Kirai kihusishi***

Kirai kihusishi ni kikundi ambacho neno lake kuu ni kihusishi. Vijalizo vyake vinaweza kuwa kikundi nomino (katika *kituo cha mabasi*, ya *udongo mwekundu*), kishazi cha kitenzi jina (kwa*kutia saini mkataba*, kwa *kupokea zawadi nono*, ya *kutoa nakala ya kitabu hiki*), kishazi/sentensi rejeshi ((amepewa kipigo) kwa *alichokifanya usiku wa kuamkia leo*) na katika miundo mingine, ambayo watu wengi

nilipowasaili walidai si Kiswahili safi, kikundi kihusishi kinaweza kuundwa na kihusishi na kishazi cha kwamba (neno la Bwana linasema ya *kwamba Hagai alimzaa Yonamu*).

Kidhima kihusishi kinaweza kuwa kikumushi cha nomino (mganda *ya miti*, mtumbwi *wa makuti makavu*), kikumushi cha kitenzi (Osama amekufa *kwa aibu kubwa*), au kiima cha sentensi (yaani kinaweza kufanya kazi kama kiwakilishi (*Kwa mkuu wa shule* kumewekwa matangazo mengi)).

## Zoezi

**1.** Tunga sentensi mbilimbili kubainisha:

(i) Kirai nomino

(ii) Kirai kitenzi

(iii) Kirai kihusishi

(iv) Kirai kivumishi

**2.** Tumia kirai kihusishi katika sentensi kama:

(i) Kielezi

(ii) Kivumishi

(iii) Kiwakilishi

## Marejeo


1. Besha, R.M. (1994) *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
2. Crystal, D. (1989) *Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.
3. Khamisi, A.M (2008) *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.
4. Massamba, D.P.B. na wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo.* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.
5. O'Grady, W. na wenzake (1997) *Contemporary Linguistics. An Introduction Language.* London: Longman.

# MUHADHARA 12

# Uainishaji wa Sentensi

## 12.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu utajifunza dhana ya sentensi, aina za sentensi kwa kutumia kigezo cha uamilifu na kigezo cha miundo.

## Madhumuni ya Muhadhara huu

Baada ya kumaliza kusoma muhadhara huu unategemewa kuweza:

(i) Kueleza kwa ufasaha sentensi ni nini

(ii) Kujua aina za sentensi kwa kutumia kigezo cha uamilifu na kigezo cha muundo.

## 12.2 Dhana ya Sentensi

Dhana ya sentensi kama inavyojulikana na Wanaisimu kadhaa ni kama ifuatavyo:
"Sentensi ni neno au kifungu cha maneno si chenye kiima na kiarifu tu, bali pia chenye kuleta maana kamili iliyokusudiwa".

Maneno ni baadhi tu ya vipashio vinavyounda sentensi. Katika Kiswahili au katika lugha kwa jumla, vipashio hivyo hujiweka katika mpangilio maalumu. Mpangilio huo wa vipashio, ndio unaomfanya mzungumzaji wa Kiswahili atambue mara moja dosari za mzungumzaji mwenzake mara inapotokea.

Mpangilio huo wa vipashio, aghalabu ni wa maneno. Maneno hayo yana tabia asilia za kutenda kazi katika sentensi mbalimbali. Maneno yenyewe yamejigawa katika **aina saba**, kama ifuatavyo:

## 12.3 Aina za Sentensi

Sentensi huweza kuainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali. Vigezo hivyo ni pamoja na *kigezo cha taarifa (maana au amilifu)* na *kigezo cha kisintaksia (miundo)*. Tutavijadili vigezo hivi hapa chini kama ifuatavyo:

**1. AINA ZA SENTENSI KIMAANA/KIGEZO CHA UAMILIFU(SEMANTIKI)**

Katika kigezo hiki sentensi huainishwa ka kuzingatia uamilifu wake hususan ujumbe uliobebwa na sentensi hiyo au unaowasilishwa.

Kigezo hiki kilitumiwa sana na wanamapokeo. Mwanamapokeo wa kwanza kutumia kigezo hiki ni PROTOGORAS na akapata sentensi kama *swali, maelezo* na *amri*. Kwa hiyo, kwa kuzingatia kigezo cha kisemantiki, sentensi huweza kuainishwa katika kategoria zifuatazo:

- Sentensi maelezo: HABWE NA KARANJA (2004:142) wanaziita *sentensi taarifa* au sentensi arifu, kwa maana kwamba ni sentensi ambazo hulenga kutoa taarifa fulani. Sentensi hizi huishia na nukta/ kituo kikuu. Mifano ya sentensi za aina hii ni kama ifuatavyo:
    a) Naibu waziri atahutubia wananchi saa nane mchana.
    b) Waziri mkuu amejiuzulu.
    c) Ufisadi unatishia utangamano wan chi yetu.
    d) Walimu wetu wanafundisha vizuri.
    e) Wanafunzi wanasoma kwa bidii.

- Sentensi amri/ amrishi: HABWE NA KARANJA (K.K.K) wanaziita sentensi agizi. Sentensi hizi kwa kawaida huwa hazina kiima na huwa na lengo la kuamuru tendo fulani lifanywe. Huundwa na kitenzi cha kuamuru. Sentensi hizi huishia na alama ya mshangao kama ifuatavyo:
    a) Ondoka!
    b) Njoo hapa!
    c) Fanya haraka!
    d) Acheni kuibia mitihani!

- Sentensi swali: HABWE NA KARANJA (K.K.K) wanaziita sentensi ulizi. Sentensi hizi uamilifu wake ni kuuliza. Kwa kawaida sentensi hizi huwa na pengo la taarifa linalohitaji kujazwa na taarifa fulani na hutambulishwa kwa uwepo wa alama ya kuuliza. Mifano ya sentensi hizi ni kama ifuatavyo:
  a) Karamagi naye kajiuzulu?
  b) Wanafunzi wanasoma kweli?
  c) Nani ameharibu kazi hii?
  d) Juma yuko wapi?

- Sentensi mshangao: hizi ni sentensi zinazooyesha kushangazwa kwa msemaji na tukio fulani. Ni sentensi za kitashititi ambazo huweza kuuliza swali ambalo jibu lake linafahamika:
  a) Baba kafariki kweli?
  b) Timu yetu imefungwa kweli?
  c) Hata wewe umefeli
  d) Waziri wetu kajiuzulu kweli!

- Sentensi shurutia: hizi ni sentensi zenye kuonyesha masharti ambazo huundwa na vitenzi viwili. Kitenzi cha kwanza hukamilishwa na kitenzi cha pili ili kuonyesha uhusiano wa mashati. Vitenzi hivyo huambikwa viambishi vya masharti. Kwa kawaida sentensi hizi huwa na masharti ya aina mbili: *masharti ya wakati uliopita* na *masharti ya wakati ujao*. Mifano ya sentensi kama hii ni kama ifuatavyo:

I. Masharti ya wakati uliopita: sentensi hizi huwa na viambishi **-nge-,** -**ngali-** na **-ngeli-** ambazo hutumika kwa kanuni maalumu. Kanuni ya matumizi yake ni kama ifuatavyo:

- ***nge……………………nge………..***
- ***ngeli…………………..ngeli……….***
- ***ngali…………………..ngali………..***

mifano ya sentensi hizi ni kama ifuatavyo:

a) A*nge*jieleza mapema asi*nge*fukuzwa kazi.

b) A*nge*niambia ni*nge*msaidia.

c) A*ngeli*fika mapema asi*ngeli*kosa nafasi.

d) A*ngali*kuwa ndugu yangu ni*ngali*muonya.

II. Masharti ya wakati ujao: sentensi hizi hutumia kiambishi cha masharti **–ki-** na maneno ya masharti kama: **kama, iwapo, ikiwa** n.k.

a) A*ki*ja mapema nitamsaidia.

b) *Kama* akija nitamkopesha fedha.

c) *Iwapo* hatafika nitamfukuza kazi.

d) *Ikiwa* nitamwona nitamwambia ukweli.

Soma pia Gichochi waihiga, SARUFI FAFANUZI YA KISWAHILI (1999), Longhorn publishers, Nairobi

**2. AINA ZA SENTENSI KIMIUNDO**

Uainishaji wa sentensi kimuundo huzingatia muundo wa sentensi hususan muundo wa vipashio vilivyounda sentensi na mahusiano ya vipashio hivyo.

Kimuundo sentensi huweza kuainishwa katika makundi yafuatyo:

-  Sentensi sahili
-  Sentensi changamani
-  Sentensi ambatano.

Labda tuanze kuzichambua mojamoja ili kuelewa miundo yake.

a) SENTENSI SAHILI

i. Hizi ni sentensi zinazoundwa kimsingi na kishazi kikuu/huru kimoja ambacho maana yake ni kamilifu. Mara nyingi sentensi sahili huwa na muundo wa kiima na kiarifu. Vile vile sentensi sahili huwa na wazo moja.

Mifano:

-  Mkulima *analima*.
-  Wanafunzi *wanasikiliza* kwa makini.
-  Rais *anahutubia* taifa.

ii. Kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi

Mifano:

- Mama *alikuwa anapika* chakula.
- Mama *alikuwa anataka kupika* chakula.
- Watoto *wanataka kucheza* mpira.

iii. Kitenzi kishirikishi.

Mifano:

- Ndizi *zi* mbovu.
- Mimi *si* fisadi.
- Maji *yana* uchafu.
- Kapu *halina* kitu.

b) SENTENSI CHANGAMANI

Hizi ni sentensi zinazoundwa na kishazi kikuu/ huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja au zaidi. Vishazi hivi haviunganishwi na viunganishi. Sifa muhimu ya sentensi hizi ni matumizi ya viambishi rejeshi amba-, -o-, au –ye-Rejea mifano ifuatayo:

- Kisu *kilichonolewa* jana *kimeibiwa*.

Kish. Tg. Kish. kikuu

- Mtoto *aliyeumia* jana *amelazwa* hospitlini.

Kish. Tg. Kish. kikuu

- Gari *lililopinduka* jana *lilipokuwa* safarini, *limeinuliwa*.

Kish. Tg. Kish. Tg. Kish. kikuu

- *Akiniambia nitamsadia*.

Kish. Tg. Kish. Tg.

Pia huweza kuundwa na vishazi tegemezi viwili vinavyokamilishana. Rejea mifano ifuatayo:

 *Ungelijua* madhara ya uvivu *ungeliacha* mara moja.
Kish. Tg. Kish. Tg.

 *Angekuja* kuniomba *ningemsaidia*
Kish. Tg. Kish. Tg.

 Mama *angalikuwa* hapa *nisingalipata* tabu.
Kish. Tg. Kish. Tg.

c) SENTENSI AMBATANI/AMBATANO

Hizi ni sentensi ambazo zina miundo ifuatayo:

i. Zinaundwa na vishazi vikuu viwili au zaidi vilivyoambatanishwa kwa kutumia kiunganishi kiambatishi au mkato (sentensi sahili mbili au zaidi)

Sentensi hizo huunganishwa na viunganishi kama: lakini, na, ingawa, tena, ila, wala, n.k Rejea mifano ifuatayo:

 *Mama analima* na *kupanda*.
 *Wanafunzi wanasoma* na *kuandika*.
 *Nimekununulia* ili *unisaidie kazi*.
 *Nilikusubiri* lakini *sikukuona*.
 *Hana sahani* wala *kijiko*
 Baba na mama wameenda shambani ila watoto wanacheza.

Sentensi ambatano hutumia viunganishi au vihusishi kama vile pia,na, ingawa, badala ya, baada n.k. Vilevile huweza kuunganishwa na alama ya mkato au nukta mkato.

## 12.4 Hitimisho

Swala tungo na aina zake si swala rahisi kama wengi wanavyoliona na ni vigumu kubainisha mipaka kati ya tungo moja na nyingine.

## Zoezi

1. Tunga sentensi moja moja ya aina zifuatazo:
   - (i) Sahili
   - (ii) Ambatano
   - (iii) Changamano
   - (iv) Ulizi
   - (v) Ya masharti
   - (vi) Arifu
   - (vii) Husishi
2. Taja aina za sentensi zifuatazo kwa kuzingatia muundo wake :
   - (i) Hojaji tuliyojaza ilikuwa na maswali funge.
   - (ii) Kaka na dada wanaandika.
   - (iii) Kongoo alikuwa na nafasi ya kufanya vyema ila hakuitumia ipasavyo.
   - (iv) Kaka analima, dada anakula.

## Marejeo


1. Besha, R.M. (1994) *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
2. Crystal, D. (1989) *Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.

Khamisi, A.M (2008) *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.

# MUHADHARA 13

# Kategoria za Kidhima

## 13.1 Utangulizi

Katika mihadhara iliyotangulia tumeona maana ya kategoria kwa mujibu wa wanamapokeo na wanamamboleo na aina za kategoria. Kwenye muhadhara huu tutajifunza kwa kina kategoria za kidhima na kuona jinsi zinavyofanya kazi.

## Madhumuni ya Muhadhara huu

Mwishoni mwa mhadhara huu mwanafunzi ataweza:

(i) Kufasili dhana ya Kategoria za Kidhima

(ii) Kuainisha kategoria mbalimbali za kidhima

(iii) Kufafanua sifa za kila Kategoria za Kidhima

## 13.2 Kategoria za Kidhima

Kategoria za kidhima ni vile vipashio ambavyo vinaonesha kazi inayofanywa na neno, kirai, kishazi au hata sentensi katika tungo fulani.

Kuna kategoria kadhaa za kidhima, nazo ni:

i. Kiima
ii. Kiarifu
iii. Chagizo
iv. Shamirisho
v. Yambwa
vi. Yambiwa
vii. Kikumushi
viii. Kijalizo.

Kwa mujibu wa sarufi mapokeo elementi za sentensi ni kategoria maalumu za sentensi ambazo huundwa kwa neno au kundi la maneno na kwamba kategoria hizo zikipangwa kwa utaratibu husika wa lugha fulani maalumu zinakuwa viambajengo vya sentensi.

## Zingatia

- Sentensi ina sehemu kuu mbili **Kiima** na **Kiarifu**.
- Elementi za sentensi ni kategoria maalum zinazojenga sentensi.
- Elementi za sentensi ni viambajengo vya sentensi.

## 13.2.1 Kiima Na Kiarifu

Sentensi inaweza kuchambuliwa kwa namna mbalimbali kulingana na nadharia au mtazamo autumiao mwanasarufi. Kwa mujibu wa sarufi mapokeo ambayo huchambulia lugha kwa elementi za kifalsafa na mantiki, wanasarufi mapokeo wanaona kwamba katika sentensi kuna kile kinachozungumzwa na yale yasemwayo kuhusiana na kile kinachozungumzwa. Kutokana na hali hiyo basi. Sarufi mapokeo kwa kutumia istilahi mahususi, inaigawa sentensi katika sehemu kuu mbili, **Kiima** na **Kiarifu**. Katika mgao huu wa uwili wa sentensi na kwa mujibu wa muundo wa lugha ya Kiswahili kwa kawaida kiima ni sehemu ya mwanzo wa tungo kabla ya kutaja kitenzi na kiarifu ni sehemu ya pili iliyobaki katika tungo kuanzia kwenye kitenzi.

### 13.2.1.1 Kiima

Kama tulivyosema hapo juu, ukiigawa sentensi katika sehemu kuu mbili, sehemu ya kwanza ikianzia mwanzo wa sentensi hadi neno la mwisho kabla ya kitenzi na sehemu ya pili ikianzia kitenzi hadi neno la mwisho katika sentensi, basi Kiima ni ile sehemu ya mwanzo. Sehemu hiyo inaweza kuundwa na neno moja au kundi la maneno. Kama ni neno moja, neno hilo laweza kuwa nomino kwa mfano Juma au kiwakilishi kwa mfano huyu. Kama ni kundi la maneno, kundi hilo laweza kuwa kirai kwa mfano mtoto mdogo au kishazi kwa mfano mtoto aliyekuja jana. Kwa mfano (2.3) hapo chini:

(a) Mtoto amevunja kikombe

(b) Huyu amevunja kikombe

(c) Mtoto mdogo amevunja kikombe

(d) Mtoto aliyekuja jana amevunja kikombe

Kulingana na mahusiano ya kikazi ya viambajengo vinavyounda sentensi, wakati mwingine kiima hufanya kazi kama mtenda wa tendo katika sentensi. Njia hii ya kubainisha kiima cha sentensi kwa kuangalia uhusiano wa kikazi sio ya kuaminika sana kwa vile sio wakati wote kiima kinafanya kazi kama mtenda katika sentensi. Kwa mfano katika mfano (2.4) hapo chini:

Kikombe kimevunjwa na mtoto

Kikombe ndio **kiima** cha sentensi ya mfano (2.4) kwa vile neno kikombe liko upande wa mwanzo wa sentensi kabla ya kitenzi. Hata hivyo katika sentensi (2.4) kikombe sio **mtenda** bali ni **mtendwa**. Kwa hiyo, kubainisha kiima cha sentensi kwa kutumia kigezo cha nafasi za maneno katika sentensi ni sahihi zaidi kuliko nje ya kuangalia uhusiano wa kikazi wa viambajengo katika sentensi. Hivyo, basi, katika sarufi mapokeo kiima cha sentensi tutakibainisha kwa kuzingatia nafasi yake katika tungo na wala sio kwa kuangalia uhusiano wa kikazi wa maneno/viambajengo vya sentensi.

## Zingatia

- Kiima ni sehemu ya mwanzo katika tungo.
- Kiima ni kile tunachoelezewa habari zake.
- Kiima kinaundwa na neno au kundi la maneno.
- Kama huundwa na neno, basi neno hilo laweza kuwa nomino au kiwakilishi.
- Kama huundwa na kundi la maneno, basi kundi hilo laweza kuwa kirai au kishazi.

### 13.2.1.2 Kiarifu

Hii ni kategoria maalum katika sentensi inayotaja kiambajengo kikubwa kimojawapo katika muundo wa sentensi. Kwa mujibu wa sarufi mapokeo ambayo imegawa sentensi katika sehemu kuu mbili kiima na kiarifu, basi kiarifu ni ile sehemu ya pili inayofuatia kiima ambapo viambajengo vingine vyote muhimu vya sentensi vikitanguliwa na kitenzi kujadiliwa pamoja. Ni kategoria ambayo kwa ujumbe wake hutupa habari kuhusu kiima cha sentensi.

Tuangalie mfano (5) hapo chini:

(a) Mtoto anakula chungwa.

(b) Mama amenunua kikombe kizuri.

(c ) Wageni wamefika nyumbani.

(d) Askari ametunukiwa zawadi nono.

Katika mfano wa (2.5) wenye sentensi (a-d) tunaona kuwa sehemu ya pili ya sentensi hizo kuanzia kwenye kitenzi ni viarifu. Ni sehemu ambazo hutoa habari kuhusu viima vya sentensi. Kwa hiyo amekula chungwa ni kiarifu katika 2.5(a); 'amenunua kikombe kizuri' ni kiarifu katika 2.5(b); 'wamefika nyumbani' ni kiarifu katika 2.5(c ) na' amenunukiwa zawadi nono ' ni kiarifu katika 2.5 (d).

## Zingatia

Kiarifu ni kategoria kuu ya pili ya muundo wa sentensi inayotupa habari zinazohusu kiima cha sentensi. Kiambajengo kikuu ndani ya kiarifu ni kitenzi.

### 13.2.2 Kijalizo

Kijalizo ni elementi muhimu **a** ya lazima katika sentensi ambayo kwa mujibu wa sarufi mapokeo inahusika na ukamilishaji wa taarifa muhimu za tendo linalotajwa na kitenzi cha sentensi. Kwa hali hiyo basi kijalizo ni elementi ya ujumla ambayo inajumuisha viambajengo kadhaa vya lazima vilivyo ndani ya kiarifu ukiondoa vitenzi kama tutakavyoona hapo chini.

### 13.2.3 Yambwa

Katika uchambuzi wa sentensi yambwa inatambulika kuwa ni kijalizo kimojawapo. Yambwa ni neno au kundi la maneno ambalo hutaja kitu au mtu ambaye tendo linalotajwa na kitenzi elekezi linaelekezwa kwake. Kwa kawaida yambwa hujibu maswali kama vile nini? Au nani? Kwa mfano :

(a) Mwalimu amemfundisha nani?

Mwalimu amefundisha mwanafunzi.

(b) Mwanafunzi amenunua nini?
    Mwanafunzi amenunua kalamu.

Katika mfano wa 2.6 (a-b) tunaona kwamba mwanafunzi na kalamu ni yambwa kwa sababu kitenzi amefundisha kinaelekezwa kwa wanafunzi na kitenzi amenunua kinaelekezwa kwa kalamu. Kwa hiyo yambwa ni kijalizo kimojawapo kwa sababu ni kiambajengo cha sentensi ndani ya kiarifu ambacho hufanya kazi ya kukamilisha taarifa muhimu za kitenzi.

### 13.2.4 Yambiwa

Katika uchambuzi wa sentensi, yambiwa inatambuliwa pia kuwa ni kujalizo kimojawapo. Yambiwa ni neno ambalo linaonyesha tendo limefanywa kwa ajili ya nani. Kwa mfano:

(a) Mwalimu amempa mtoto kitabu.

(b) Mama amemletea mgonjwa maziwa.

Katika mfano 2.7 (a) kuna tendo la kumpa fulani kitabu na katika mfano 2.7 (b) kuna tendo la kumletea fulani maziwa. Anayenufaika kwenye tendo la 2.7 (a) ni mtoto na anayenufaika kwenye tendo la 2.7 (b) ni mgonjwa. Kwa hiyo katika sentensi 2.7 (a) na (b) mtoto na mgonjwa ndiyo yambiwa. Kwa kuzingatia mfano wa 2.7 (a) na (b) tunahitimisha kuwa yambiwa ni kijalizo pia kwa vile ni kiambajengo cha sentensi ambacho ni sehemu ya kiarifu na kama ilivyo kwa yambwa, hufanya kazi ya kukamilisha taarifa muhimu za kitenzi.

**Vijalizo Vinavyofuatia Vitenzi husishi**

Kuna vijalizo vingine ambavyo vinapatikana katika sentensi zenye vitenzi husishi kama vile **ni, si , yu** n.k. Kwa kuanzia hapa tutataja aina mbili tu ambazo ni kivumishi arifu na nomino arifu.

**Kivumishi Arifu**

Kivumishi arifu hutambuliwa kuwa ni kijalizo kimojawapo. Kivumishi arifu ni neno linalotoa habari zaidi kuhusu kiima cha sentensi ila tu hakikai upande wa kiima bali hukaa upande wa kiarifu na huja mara tu baada ya kitenzi husishi. Kwa mfano:

(a) Mama ni mpole.

(b) Dada si mweupe.

(c) Baba yu mcheshi.

Utaona kwamba katika sentensi (a) neno mpole hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino ya kiima mama, katika sentensi (b) neno mweupe hutoa taarifa zaidi ya nomino ya kiima dada na katika sentensi (c) neno mcheshi hutoa taarifa zaidi ya nomino ya kiima baba. Neno lolote ambalo hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino huitwa kivumishi, na mara nyingi huja mara baada ya nomino k.m. Mama mrefu, dada mweupe au baba mcheshi. Lakini wakati mwingine kivumishi hicho chaweza kuja baada ya kitenzi husishi ndani ya kiarifu na kukamilisha taarifa za kitenzi husishi pia. Kwa hiyo hutambuliwa kama kijalizo.

**Nomino Arifu**

Nomino arifu hutambuliwa kuwa ni kijalizo pia. Nomino arifu ni neno linalofanya kazi ya kutaja kiima au kukibainisha. Hutokea sehemu ya kiarifu na huja mara tu baada ya kitenzi husishi kwa mfano:

(a) Mlima mrefu Barani Afrika ni Kilimanjaro.

(b) Yule kijana ni Askari.

Utaona kwamba katika sentensi 9 (a) neno Kilimanjaro hufanyakazi ya kubainisha kiima kinachoelezwa kwenye sentensi na sentensi 9 (b) neno askari hutaja au hubainisha kiima ni nani. Kwa kuwa maneno haya ni viambajengo vya sentensi na yako ndani ya kiarifu na hukamilisha taarifa za vitenzi husishi basi hutambuliwa kuwa ni vijalizo.

## Zingatia

- Kijalizo hukamilisha taarifa muhimu za tendo linalotajwa na kitenzi.
- Vijalizo muhimu ndani ya kiarifu ni yambwa na yambiwa.
- Vijalizo vinavyoambatana na vitenzi husishi ni kivumishi arifu na nomino arifu.

### 13.2.5 Chagizo

Chagizo ni elementi ya sentensi iliyo ndani ya kiarifu ambayo kazi yake ni kutoa taarifa za ziada ambazo wakati mwingine sio za lazima katika kukamilisha sentensi. Kunaweza kuwa na aina mbalimbali za chagizo lakini aina mojawapo inayotambuliwa sana ni Kielezi. Kwa hiyo kielezi ni kijalizo kimojawapo. Kielezi ni neno katika kiarifu ambalo hutumika kutoa taarifa za ziada kuhusu kitenzi. Kwa mfano tendo linalotajwa na kitenzi limefanyika wapi, lini au kwa namna ipi?

Kwa mfano:

(a) Wasafiri wamekula hotelini.

(b) Juma atakuja kesho.

(c) Harusi inatembea polepole.

Katika sentensi 2.10 (a-c) maneno yenye herufi nene ni vielezi. Neno hotelini hutaja wapi tendo la kula linafanyika, neno kesho hutaja lini tendo la kutembea litafanyika na neno polepole hutaja kwa namna ipi tendo la kutembea linafanyika. Maneno yote haya ni vielezi kwa vile maneno haya ni viambajengo vya sentensi ndani ya kiarifu na hutoa taarifa za ziada kuhusu vitenzi basi hutambuliwa kama chagizo.

## Zingatia

i. Chagizo ni elementi ambayo iko ndani ya kiarifu.
ii. Chagizo sio elementi ya lazima kama ilivyo kijalizo.
iii. Chagizo hutoa taarifa za ziada kuhusu kitenzi.
iv. Kategoria mojawapo ndani ya chagizo ni kielezi.

## 13.3 Hitimisho

Katika somo hili, umejifunza jinsi ya kuitambua sentensi pamoja na elementi zake. Umejifunza kuwa sentensi ina sehemu kuu mbili: **kiima** na **kiarifu**.

Umejifunza pia kuwa katika sehemu zile kuu mbili za sentensi, kiima ndio sehemu ya kwanza.
Kuhusu kiarifu umejifunza kuwa hii ni sehemu kuu ya pili katika muundo wa sentensi. Kadhalika umejifunza kuwa kiambajengo muhimu katika kiarifu ni kitenzi. Hata hivyo, ili kukamilisha taarifa za vitenzi, kiarifu huwa kina vipashio vya lazima ambavyo kijumla hujulikana kama vijalizo, lakini kimoja huitwa **yambwa** na kingine huitwa **yambiwa.**

Zaidi ya hayo, ndani ya kiarifu kunaweza kuwa na elementi nyingine ambayo sio ya lazima sana kama kijalizo katika kukamilisha taarifa za sentensi. Elementi hiyo huitwa **chagizo** na **kipashio** kimojawapo ambacho kimo ndani ya chagizo ni kielezi.

Elementi zote hizi tulizozitaja katika somo hili ndiyo viambajengo muhimu vinavyojenga muundo unaoitwa sentensi katika lugha.

### Zoezi

Jibu maswali yafuatayo kikamilifu:

1. Kwa kutumia mfano, eleza ukamilifu wa sentensi unatokana na nini?
2. Taja sehemu kuu mbili za sentensi na eleza sababu za msingi za mgawanyo huo.
3. Kutokana na muundo wa lugha ya Kiswahili, katika mgawo wa uwili wa sentensi, ni sehemu ipi muhimu zaidi kati ya sehemu hizo kuu mbili za sentensi.
4. Tunga sentensi na kuonesha **kiima** na **kiarifu**.
5. Tunga sentensi inayoonesha **kiima** na **kiarifu.** Ndani ya kiarifu onesha **kitenzi, kijalizo** na **chagizo.** Ndani ya kijalizo onesha **yambwa** na **yambiwa** na ndani ya chagizo onesha **kielezi**.

## Marejeo


1. Ashton E.O. (1944) Swahili Grammar and Intonation, Longiman. London.
2. Brain B, (1969) , Basic Swahili Structure, New York.
3. Broomfied G.W. (1975), Sarufi ya Kiswahili .OUP: Nairobi.
4. Dornan Edward A. na Charles W. Dawe, (1984), The Brief English. Handbook, Little Brown and Brown and Company: Boston, Toronto.
5. Kiango J.G. (2000). Bantu Lexicography, ILCAA: Tokyo.
6. Kihore Y.M. D.P.B Massamba, Y.P. Msanjila (2001). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, TUKI . Dar es Salaam.
7. Kihore Y.M. D.P.B. Massamba Y.P. Msanjila (2000) Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, TUKI, Dar es salaam.

# MUHADHARA 14

## Uchambuzi/Uchanganuzi wa Sentensi

### 14.1 Utangulizi

Katika uchambuzi au uchanganuzi wa sentensi,neno uchambuzi na neno uchanganuzi yana maana sawa:mchanganuzi au mchambuzi hana budi kutambulisha:

(i) Aina ya sentensi yaani kama ni sahili, ambatano, changamano au shurtia.

(ii) Kiima na kiarifu.

(iii)Vikundi nomino, vikundi vivumishi, vikundi vitenzi na vikundi vielezi. (iv) Aina za maneno yaliyotumika katika sentesi.

### Madhumuni ya Muhadhara huu

Baada ya kumaliza kusoma muhadhara huu inabidi uweze:

- Kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi, maelezo na njia ya mishale.

### 14.2 Mifano ya Uchambuzi/Uchanganuzi wa Sentensi kwa Njia ya Maelezo

Huu ni uchanganuzi unaotumia maelezo kuonyesha kila kipashio;

Kwa mfano:

(a) Huu si ugonjwa wa kutisha.

**Maelezo:**

(i) Hii ni sentesi sahihi.

(ii) Sentensi hii ina kiima na kiarifu. Kiima ni *Huu*. Kiarifu ni si *ugonjwa wa kutisha*.

(iii) Kiima hicho kimejengwa na kikundi nomino chenye kiwakilishi kimoja tu ambacho ni *Huu*.

(iv) Kiarifu kimeundwa na kikundi tenzi na kikundi nomino. Kikundi tenzi kimeundwa na kitenzi kishirikishi *si*. Kikundi nomino kimeundwa na nomino *ugonjwa* pamoja na kivumishi *wakutisha***.**

(b) Shida yao inajulikana lakini msaada haujapatikana.

**Maelezo:**

(i) Hii ni sentesi ambatani.

(ii) Imeundwa kwa sentesi sahili; ambazo ni:

- Shida yao inajulikana.
- Msaada haujapatikana.

(iii) Sentesi ya kwanza ina kiima na kiarifu. Kiima ni shida yao; na kiarifu ni inajulikana

(i) Kiima cha sentesi hiyo kimeundwa na kikundi-nomino chenye nomino shida na kivumishi yao.

(ii) Kiarifu cha sentesi ya kwanza kimejegwa kwa kikundi-tenzi chenye kitenzi kikuu kimoja inajulikana.

(iii) Sentesi ya pili ina kiima na kiarifu. Kiima ni Msaada na kiarifu ni haujapatikana.

(iv) Kiima cha sentesi hiyo kimeundwa na kikundi nomino chenye nomino moja msaada

(v) Kiarifu kimejengwa kwa kikundi tenzi chenye kitenzi kikuu kimoja haujapatikana.

(vi) Sentesi ya kwanza na ya pili zimeunganishwa kwa kutumia kiunganishi lakini.

(vii) Wanafunzi walilima kisha wakapanda mahindi.

**Maelezo:**

(i) Hii ni sentesi ambatano yenye sentesisahili mbili:

- Wanafunzi walilima.
- Wanafunzi walipanda.

(ii) Sentensi ya kwanza imeundwa kwa kikundi-nomino chenye nomino moja, wanafunzi

- Sentesi hiyo ina kiima na kiarifu; kiima ni wanafunzi na kiarifu ni walilima.
- Kiarifu kimeundwa kwa kikundi-tenzi chenye kitenzi kikuu kimoja. walilima.

(iii) Sentesi ya pili ina kiima na kiarifu. Kiima ni wanafunzi (japokuwa hakiko dhahiri), kiarifu ni walipanda mahindi.

(iv) Kiima cha sentesi ya pili kimeundwa kwa kikundi-nomino chenye nomino wanafunzi.

(v) Kiarifu kimeundwa kwa kikundi kitenzi kimoja na kikundi nomino. Kikundi tenzi kina kitenzi kimoja, walipanda. Kikundi nomino kimejengwa kwa nomino moja, mahindi.

(vi) Sentesi ya kwanza na ya pili zimeunganishwa/kuambatanishwa kwa kiunganishi kisha.

## 14.3 Kwa Njia ya Mishale

Uchanganuzi wa sentesi kwa kutumia mishale unafanana na ule wa maelezo. Tofauti ni kwamba hapa mishale hutumika badala ya maelezo.

Tuangalie mifano ifuatayo ya uchanganuzi wa sentesi kwa njia ya mishale:

(a) Watoto wema huwatii wazazi wao. [Hii ni sentesi-sahili]

**Uchanganuzi**

⟶ **S** Watoto wema huwatii wazazi wao.

**S** ⟶ **KN + KT**

**KN** ⟶ N + V

N ⟶ *watoto*

V ⟶ *Wema*

**KT** ⟶ T + KN

T ⟶ *huwatii*

**KN** → N + V

N → *wazazi*

V → *wao*

(b) Wanyama waliojeruhiwa walikimbilia porini.

[Hii ni sentesi changamano]

**S** → **KN + KT**

N → *Wanyama*

**KN** → N + V

V → *waliojeruhiwa*

**KT** → T + KE

T → *walikimbilia*

**KE** → **E**

E → *porini*

(c) Baba amenunua kitabu kikubwa sana.

[Hii ni sentesi-sahili]

(i) S → KN + KT

KN →

(ii) N →

N →

KT →

(iii) *Baba*

T →

(iv) T + KN

(v) *amenunua*

(vi) KN → N + KV

(vii) N *kitabu*

(viii) KV V + E

(ix) V *kizuri*


(x) E *sana*

## 14.4 Kwa Njia ya Matawi

***Mifano:***


(a) Baba amerudi

[sentesi-sahili]





(b) Baba mdogo amerudi leo.

[sentesi sahili]




(c) Baba mdogo wa mwisho amerudi leo leo

[sentesi sahili]




(d) Baba mkubwa amenunua kitabu kizuri sana sana.

[sentesi sahili]




## Zoezi

1. Changanua sentesi zifuatazo kwa kutumia njia ya mishale na maelezo.
   (i) Kule kwako kuna milima mirefu.
   (ii) Tukila matunda tutapata afya bora.
   (iii) Basi litaondoka asubuhi sana.

2. Kwa kutumia mifano, eleza tabia tano za vitenzi .

3. Ongeza viambishi vya urejeshi, wakati na nafsi katika vitenzi vifuatavyo, kisha tunga sentesi kutumia vitenzi hivyo: cheza, imba, kata, chonga.

4. Kwa kila kauli iliyotajwa, tunga sentesi mbili kuonesha matumizi ya kauli hiyo:
   (a) Kutenda
   (b) Kutendwa
   (c) Kutendewa
   (d) Kutendea
   (e) Kutendana

3. Eleza sababu za kuongeza msamiati katika lugha.

4. Unda maneno mingine manne kwa kila neno kwa kutumia herufi za maneno yafuatayo:

   (a) ona (b) mto (c) ita

5. Ongeza viambishi katika maneno yafuatayo ili kuunda maneno mengine matano kwa kila neno moja.

(a) pika (b) chora (c ) ita

Changanua sentensi zifuataazo kwa njia ya maelezo na ya mishale

(a) Maua yanachanua wakati wa kipupwe.
(b) Siku hizi sukari imeadimika.
(c) Sina muda wa kupoteza
(d) Sinema hazileti neema nchini.

7. Changanua sentesi zifuatazo kwa kutumia njia ya matawi au visanduku.

(a) Mvua hizo ziliandamana na upepo mkali na ngurumo.
(b) Pilau haishindi biriani.
(c) Mtoto aliyepotea jana asubuhi, ameonekana sasa hivi.
(d) Wanafunzi wote wamefika, ingawa wengi wamechelewa sana

## Marejeo


1. Besha, R.M. (1994) *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
2. Crystal, D. (1989) *Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.
3. Khamisi, A.M (2008) *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.
4. Massamba, D.P.B. na wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.
5. O'Grady, W. na wenzake (1997) *Contemporary Linguistics*. *An Introduction Language*. London: Longman.
6. Radford, A. na wenzake (1999) *Linguistics*. *An Introduction*. London: CUP.

# MUHADHARA 15

# Semantiki

## 15.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu, tunakusudia kuelezea semantiki. Awali neno semantiki lilitumika kumaanisha sayansi ya "maana" kwa ujumla, hivi kwamba ilishughulikiwa na wanafilosofia, wanasaikolojia, wanamantiki, wanaanthropolojia na wengineo. Baadaye stadi hii ilijishughulisha zaidi na maana katika muktadha wa mwanadamu. Katika muhadhara huu tutashughulikia semantiki katika muktadha huu yaani maana katika misingi ya kinadharia ya isimu.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kumaliza kusoma muhadhara huu, mwanafunzi ataweza:

(i) Kueleza maana ya maana

(ii) Kuainisha aina za maana

(iii) Kueleza na kutofautisha uhusiano wa maana

(iv) Kueleza dhana ya maana kiutendaji

## 15.2 Maana

Neno maana linafahiwa nyingi. Watu wa kawaida wamelitumia kumaanisha vitu mbalimbali:

a. Una maana gani kwa kufika umechelewa

b. Yale mawingu meusi yana maana mvua itanyesha sasa hivi

c. Hiyo nguo nyekundu inamaanisha hatari

d. Mradi huu una maana kubwa

e. "Baba" maana yake MZAZI WA KIUME

Maana inayoyorejelewa katika lugha ni ile katika sentensi ya "e". Dhana ya maana ni ya kidhahania kwa sababu haina muundo thabiti kama vile viambajengo vya lugha kama vile vya: kifonolojia, kimofolojia au kisintaksia. Maana pia hutegemea dhamira ya mtoa ujumbe na fasiri ya mpokea ujumbe.

## 15.3 Aina za Maana

Wanaisimu mbalimbali wameeleza dhana ya aina za maana katika vitengo viwili vikuu; maana ya msingi na maana ya ziada. Hata hivyo Leech (1981) amebainisha aina za maana zifuatazo:

### 15.3 1 Maana ya msingi (conceptual meaning)

- Hii ni aina ya maana ambayo haibadiliki mfano; mwanamke, mwanaume. Hutaja sifa zake kuu. Zile sifa bainifu ndizo hupelekea kupata maana kuhusu mtu.

### 15.3.2 Maana dokezi (connotative meaning)

- Ni aina ya maana ambayo hutokana na umbo la kitu, kisaikolojia, kimatamshi mf. Kiumbo kushika mimba, kisaikolojia umama.

### 15.3.3 Maana ya kijamii / kimtindo (social meaning)

- Ni aina ya maana ambayo hupatikana kutokana na mazingira ya kijamii, wakati, utamaduni, kijiografia, kiuwasilishaji, hadhi, ubinafsi n.k

### 15.3.4 Maana ya kihisi (emotive meaning)

- Ni maana za kihisia ambazo hutokana na upotoshaji wa aina fulani wa maana ya msingi. Ni maana itokanayo na utumizi usio wa moja kwa moja ili kutoa maana. Maana ya kitu huwa ni ya mzunguko, fiche, kwa mfano maana za hisia hutegemea sana Kiimbo kiwekwacho katika neno au Kiimbo kiwekwacho katika sentensi.

### 15.3.5 Maana tangamani (collocative meaning)

- Maana ambatani au tangamano, ni aina ya maana itokanayo na utangamano au uambatani wa baadhi ya maneno kwa mfano: Mrembo – Msichana

: Ujamali – Mvulana

: Jitu hili ni la miraba mine – Mwanaume

- Katika lugha maneno pia hujengwa kwa mtindo huo mifano zaidi Samaki – Kiumbe wa majini/baharini au Swala - Kiumbe wa msituni. Ukitaja kimoja tu mfano samaki unakuwa umekiondoa kingine swala.

### 15.3.6 Maana ya kidhima/kidhamira (thematic meaning)

- Hizi ni aiana za maana ambazo ujumbe wake unapangwa kufuatana na msisitizo wa kitu. Maana hutokana na dhamira ambayo msemaji alikusudia ili imfikie msikilizaji, kwa mfano sentensi zifuatazo:

- (a) Mwalimu amempiga mtoto (Mwl. Mtenda)
- (b) Mtoto amepigwa na mwalimu (Mtoto Mtendwa)
- (c) Msichana yupo darasani (Jibu la swali lililoulizwa) – Msichana yuko wapi?
- (d) Darasani kuna msichana (Swali)

### 15.3.7 Maana akisi/Kimwangwi (reflected meaning)

- Ni maana ambazo ukitaji kitu fulani au maana fulani unakonyeza maana nyingine. Maana akisi haziachani kwa mfano: Jamii – Mkusanyiko wa watu pamoja

## 15.4 Uhusiano wa Maana

Katika taaluma ya semantiki, kuna uhusiano wa aina tatu wa maana; Utajo, Urejeleo na Fahiwati.

### 15.4.1 Utajo (Notion).

Huu ni uhusiano wa maana kutokana na kutaja kitu kama kilivyo katika ulimwengu halisi. Utajo hutaja kitu kama kilivyo kwa ujumla. Kwa mfano dhana ya meza katika ulimwengu huu tunaoufahamu maana zake ni nyingi lakini kuna sifa za kisemantiki zinazotofautisha meza na kitu kingine katika utamaduni. Kamusi moja (D. Crystal (1991: 97)* ilifafanua kuwa maana ya utajo ni sawa sawa na maana ya Kiurejeleo. Katika kubainisha maana kiutajo, rejelea sifa za kisemantiki unazozifahamu kimalimwengu. Mfano Mwanaume au Mwanamke (taja sifa za kila mmoja).

Utajo huhusu uhusiano baina ya leksimu au kipashio cha kiisimu na seti ya vitu ambayo inarejelewa na kipashio hicho katika ulimwengu halisi. Kwa mfano, utajo wa leksimu meza ni vitu vyote katika

dunia ambavyo kwa hakika vinaitwa meza. (Kama nilivyosema, wataalamu wengine wanauita uhusiano huu urejeleo pia, lakini huku ni kuchanganya dhana!).

### 15.4.2 Fahiwati (Sense)

Fahiwa ya kiyambo ni seti ya mahusiano yaliyopo baina ya kiyambo hicho na viyambo vingine katika lugha. Mahusiano hayo huitwa mahusiano ya kifahiwa au ya kisemantiki. Mifano ya mahusiano hayo ni usawe (k.m. mwanaume, rijali), unyume (utu, unyama), n.k. Mahusiano hayo ndiyo yanayoukilia fahiwa ya kiyambo chochote kile.

**Swali:**

Je, "fahiwa" ina uhusiano gani na "utajo"? Dhana hizi zinatofautianaje na zinafananaje?

Tofauti baina ya fahiwa na utajo ni kwamba fahiwa ni uhusiano baina ya viyambo vya kileksia – yaani uhusiano ulio ndani ya lugha – wakati utajo ni uhusiano baina ya viyambo vya kileksia na seti ya vitu vilivyo duniani.

Ufanano baina ya fahiwa na utajo unaweza kuelezwa ifuatavyo. Dhana hizi kwa pamoja hutumika kwa viyambo sahili vya kileksia na viyambo changamani vya kileksia ambavyo fahiwa na utajo wake hutegemea fahiwa na utajo wa leksimu zinazounda viyambo hivyo. Kwa mfano, "mwanamke" ni kiyambo sahili wakati "mwanamke aliyezaa mtoto" ni kiyambo changamani. Fahiwa na utajo wa viyambo hivi unategemea fahiwa na utajo wa leksimu zinazoviunda.

Uhusiano mwingine uliopo baina ya fahiwa na utajo ni ule wa kutegemeana – yaani haiwezekani kufahamu fahiwa pasipo kufahamu utajo.

Uhusiano mwingine uliopo kati ya fahiwa na utajo ni ule ambao twaweza kuuita uhusiano pindu, ambao waweza kuelezwa ifuatavyo: iwapo utajo unazingatia dhana pana (yaani "utajo ni mkubwa"), basi fahiwa huwa ni finyu (yaani "dhana ndogo"). Tutatumia mfano wa mnyama na paka kuelezea jambo hili. Utajo wa "mnyama" ni mkubwa (yaani unzangatia viumbe wengi zaidi); fahiwa ya "mnyama" inajumuiza "paka" (paka wote ni wanyama, ila wanyama wote si paka) lakini si mahususi, na inaingizwa katika fahiwa ya "paka".

* D. Crystal 1991. A DICTIONARY OF LINGUISTICS AND PHONETICS, TOLEO LA 3. Oxford: Blackwell.

### 15.4.3 Urejeleo (Reference)

Urejeleo ni uhusiano baina ya viyambo vya kiisimu na viwakilisho vyake duniani wakati maalumu wa semo. Ni kipengele cha maana ya semo kinachotegemea muktadha. Masafa ya urejeleo ya viyambo rejelezi hutegemea utajo na fahiwa, lakini urejeleo halisi wa viyambo hivyo hutegemea mambo kadhaa yahusianayo na muktadha. Mfano wa viyambo rejelezi ni Machumu, mtoto yule, kijana aliyekuja sasa hivi, n.k. Sifa bainifu ya viyambo hivi vyote ni kwamba vinarejelea kitu mahususi katika ulimwengu wa masilugha, na kwamba vitu hivi vinaukiliwa na muktadha.

## 15.5 Viwango vya Maana

Dhana ya maana ni dhana ya kidhahania, hivyo wataalamu wa isimu wamejaribu kueleza dhana hii kiutendaji. Kiutendaji maana inaweza kubainishwa katika kiwango cha neno na kiwango cha tungo/sentensi.

(a) Maana katika Kiwango cha neno (Maana ya Kileksika)

- Hizi nia aina za maana zinazowakilishwa na vidahizo katika kamusi. Vidahizo hivi ni kwa mfano maeno kama vile “gari”, “mtu”, “barabara”. Maana kileksika pia hujulikana kama maana ya msingi. Maana msingi ndiyo maana kuu ya neno. Maana hii kwa kawaida huwa haibadiliki kutegemea athari za kimazingira au muktadha.
- Aina nyingine ya maana ya kileksikaa, ni ile maana kisarufi. Hii hurejelea maana ya neno katika muktadha wa matumizi

(b) Maana katika Kiwango cha Tungo

Tungo ni matokeo ya kuweka au kupanga pamoja vipashio sahili ili kujenga vipashio vikubwa zaidi vyenye maana. Mpangilio huo huzingatia kanuni fulani za kisarufi ili kuleta maana. Ukibadilisha uunganifu huo, maana nayo kadhalika hubadilika. Maana hupatikana kutokana na mpangilio kubalifu wa vipashio. Maana za tungo au sentensi hutawaliwa na kanuni ya utungamanifu.

Kanuni ya Utungamanifu: Miongoni mwa mambo yanayoukilia maana ya sentensi ni kanuni ya utungamanifu: kanuni inasema kwamba maana ya kiyambo changamani cha kisintaksia (kirai, sentensi) inatokana na maana za viambajengo vya kiyambo hicho na mpangilio au mahusiano yao ya kisarufi.

Umuhimu wa kanuni hiyo unadhihirika pindi maneno yaleyale yanapotumika kuunda sentensi zenye maana tofauti kutokana na tofauti za kimpangilio zilizojikita kwenye tofauti za mahusiano ya kisarufi. Chunguza mifano ifuatayo:

1. Msichana alimkimbia mbwa
2. Mbwa alimkimbia msichana

Tofauti baina ya sentensi (1) na (2) inatokana na nomino mbwa na msichana kubadilishana nafasi za kiima na yambwa. Hapa tunaona kuwa tofauti za mahusiano ya kisarufi zinazotokana na tofauti za mpangilio wa maneno huchangia katika maana ya sentensi.

Sifa na Mahusiano ya Kimaana

Baadhi ya sifa na mahusiano muhimu ya kimaana kwenye kiwango cha sentensi ni:

1. Usawe
2. Utata
3. Ukinzani
4. Upotoo
5. Uziada-dufu

**Usawe**

Huu ni uhusiano baina ya sentensi mbili ua zaidi zenye kudhihirisha maana moja ya msingi. Mifano ya usawe ni hii ifuatayo:

5. Kasoga alitupa jiwe likampiga Kwezi.
6. Kasoga alivugumiza jiwe likamnasa Kwezi.

Katika mifano hii, vitenzi *tupa* na *vugumiza* vina maana ileile, na vitenzi *piga* na *nasa* vina maana ileile.

Usawe wa sentensi unafanana na usawe wa maneno kwa kuwa ni mahusiano yanayodhihirisha "uchopezi" bila badiliko la maana ya msingi.

Upo usawe wa namna mbili:

- Usawe wa kileksia
- Usawe wa kimuundo

Usawe wa kileksia unahusu sentensi mbili au zaidi ambazo zina maneno yenye maana ileile ya msingi katika nafasi ileile. Mifano (3) na (4) ni ya usawe wa namna hii.

Usawe wa kimuundo unatokana na maana ya msingi ya sentensi mbili au zaidi kubaki ileile japo sentensi zina mpangilio tofauti. Usawe huu ni wa kimuundo kwa sababu hauhusiani na usawa wa maana za maneno au virai – kwani maneno ama ni yale yale au yanatofautiana kidogo sana. Mifano:

7. (a)Hakuna aliyeelewa maneno yake ya ajabu.
   (b) Maneno yake ya ajabu hayakueleweka.

8. (a) Maelezo yake yalikuwa magumu kufahamika.
   (b) Ilikuwa vigumu kufahamu maelezo yake.

Sentensi (a) na (b) katika (5) na (6) zina maana ileile ya msingi. Sentensi za namna hii hutokana na mchakato ambao kiisimu huitwa uhamishaji. Mchakato huu huhamisha vipashio kadha toka mwishoni na kuvipeleka mwanzoni, na vya mwanzoni kuvipeleka mwishoni.

**Utata**

Utata ni kipengele kinachodhihirisha tafsiri zaidi ya moja. Upo utata wa kileksia na wa kimuundo.

Utata wa kileksia unatokana na polisemia au homonimia, kwa mfano:

9. Baada ya shida nyingi alifanikiwa kumleta papa nyumbani.

10. Bei ya kanga ni shilingi elfu nne.

Katika sentensi ya (7) papa anaweza kuwa papa mnyama au papa mkuu wa kanisa katoliki, na katika sentensi ya (8) kanga anaweza kuwa kanga ndege au kanga nguo.

Utata wa kimuundo unatokana na jinsi sentensi ilivyopangiliwa au umbo, neno au kirai kuwa katika nafasi maalumu ya sentensi. Mifano ni:

11. Wanawake na wanaume waangalifu walikaa kando.

12. Alimwandikia barua baba yake.

13. Walipigana nasi.

Katika sentensi ya (9) tafsiri ni mbili: ama wanawake waangalifu na wanaume waangalifu au anawake na wanaume waangalifu. Katika sentensi ya (10) tafsiri ni mbili pia: ama aliandika barua kwa ajili au kwa niaba ya baba yake; au aliandika barua kwa baba yake. Na sentensi ya (11) ni tata: tafsiri ni ama: walipigana katika kundi letu dhidi ya adui yetu au walipigana dhidi yetu.

Usawa na utata vina uhusiano linganuzi. Katika usawe tungo kadhaa hupewa tafsiri moja, wakati katika utata tungo moja hupewa tafsiri zaidi ya moja. Uhusiano huu unaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo:

Maana 1

Maana 2

UTATA WA TUNGO TUNGO 1 Maana 3

Maana 4

Maana …

Tungo 1

Tungo 2

USAWE WA TUNGO Tungo 3 MAANA 1

Tungo 4

Tungo…

**Ukinzani**

Kiyambo kinzani ni kile kinachodhihirisha vigambe viwili siganifu wakati mmoja. Kiyambo cha namna hii hunena kwamba fulani au kitu fulani kina sifa fulani na wakati huohuo hakina sifa hizo. Mifano ya viyambo kinzani ni:

14. Yule mwanamme ni mwanamke.

15. Yule mtu mzima ni mtoto.

16. Hapo juu ndio chini.

Vigambe vinavyotolewa na sentensi hizo havikubaliani na ujuzi wetu wa malimwengu. Kwa mfano, mtu hawezi kuwa [+ME] na [-ME] wakati huohuo. Mifano mingine ya ukinzani ni:

17. Nilishuka juu, nikapanda chini.

18. Nilikwenda mbele, nikabaki nyuma.

Ukinzani kama huu hutumiwa sana na baadhi ya washairi wanapotaka kueleza jambo ambalo lina ukinzani ndani yake.

Upotoo

Huu ni ukiushi wa kisemantiki utokeao pindi vijenzi-semantiki viwili siganifu vinapounganishwa kueleza jambo au kitu.

Mifano ya upotoo ni:

19. Alichora barua kwa mguu wa kushoto.

20. Alimpiga teke kwa kalamu nyeusi.

Hapa upotoo unadhihirika baina ya chora na barua, na baina ya chora na mguu; kadhalika upo baina ya piga teke na kalamu.

**Uziada-dufu**

Uziada-dufu ni urudiaji usiohitajika; tazama mifano ifuatayo:

21. Mke wangu ni mke wangu.

22. Mbwa ni mnyama.

23. Wanafunzi ni wanafunzi.

24. Walimu ni walimu.

Kuna mambo mawili ambayo ni muhimu kuyataja kuhusiana na uziada-dufu:

• Ni urudiaji usio na jambo jipya; wala hauufanyi ujumbe ukawa wazi.

Sentensi yenye uziada-dufu ni kweli kwa mujibu wa maana za maneno yanayoiunda

## Zoezi

1. Eleza kwa muhtasari maana ya "maana".
2. Jadili aina zifuatazo za maana:
   (i) Maana ya kimsingi.
   (ii) Maana ya ziada.
   (iii) Maana husishi
   (iv) Maana kileksia
   (v) Maana kisarufi

## Marejeo


1. Besha, R.M. (1994) *Utangulizi wa Lugha na Isimu.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
2. Crystal, D. (1989) *Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.
3. Khamisi, A.M (2008) *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.
4. Massamba, D.P.B. na wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo.* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI


.

# MUHADHARA 16

# Fasihi kwa Ujumla

## 16.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu, tutafafanua dhana ya fasihi. Tutayapitia na kuyahakiki maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana hiyo na tutajaribu kutoa maana ya fasihi ambayo tunadhani inakidhi mahitaji ya kozi hii. Tutaziangalia pia nadharia mbalimbali kuhusu chimbuko la fasihi, na kuhusu uhusiano wa fasihi na jamii. Muhadhara huu utakuwa na sehemu mbili: sehemu ya kwanza itahusu maana ya fasihi. Sehemu ya pili itazungumzia chimbuko la fasihi.

## Malengo ya Muhadhara huu:

Muhadhara huu utakuwezesha:

i Kuielewa dhana ya fasihi kwa kina na mapana yake.

ii Kujua nadharia mbalimbali za chimbuko la fasihi na dosari au ubora wa nadharia hizo.

## 16.2 Maana ya Fasihi

Dhana ya fasihi imekuwa ikijadiliwa kwa karne nyingi na wataalamu mbalimbali ulimwenguni kote. Huko Ulaya, dhana hii imekuwa ikihusishwa na neno la Kilatini Littera ambalo maana yake ya asili ni "herufi" au uandikaji". Neno la Kiingereza "literature" limechipuka hapo. Mitazamo iliyotawala kuhusu dhana hii ni mitano.

Mtazamo wa kwanza ni ule unaodai kuwa "literature" ni jumla ya maandishi yote katika lugha fulani. Wellek naWarren wanauelezea mtazamo huu hivi.

Njia mojawapo ya kuielezea fasihi ni kuichukulia kuwa jumla ya machapisho yote.

Dosari kuu za mtazamo huu ni mbili. Kwanza, unaupanua sana uwanja wa fasihi na kuingiza vitu ambavyo kwa kawaida watu hawavifikirii kuwa ni fasihi. Iwapo kila kilichoandikwa au kupigwa chapa ni fasihi, basi hata matangazo ya biashara au maelezo tu ya habari fulani yataitwa fasihi.

Dosari ya pili, kama wanavyodokeza Wellek na Warren, ni kwamba mtazamo juu unaibagua sehemu kubwa ya fasihi ya ulimwengu - - ile ambayo haikuandikwa au kupigwa chapa.

Katika taaluma ya Kiswahili, mtazamo wa aina hii ulijitokeza kidogo kwenye miaka ya mwanzo ya 1970 (Mulokozi 1973' Sengo na Kiango 1973:1) .Wakati huo taaluma ya fasihi ya Kiswahili ilikuwa ingali katika hatua za mwanzo.Hata dhana yenyewe ya "literature" ilikuwa bado inatafutiwa istilahi yake ya Kiswahili. Baadhi ya maneno yaliyopendekezwa ni "adabu ya lugha" na "fasihi". Hatimaye neno "fasihi" lilishinda na kupewa ufafanuzi wake wa sasa – yaani sanaa ya lugha, bila kujali kama imeandikwa au la.

Mtazamo wa pili unaifinya dhana hiyo na kudai kuwa "literature" ni maandishi bora au jamii ya kisanaa yenye manufaa ya kufumu. Hollis Summers unaofafanua hivi mtazamo huo:

Mtazamo huu unaupa uzito usanii na uwezo wa kubuni, lakini pia unaifinya fasihi kwa kuihusisha na maandiko yaliyo bora tu.

## 16.3 Chimbuko la Fasihi

Kuna nadharia kuu nne za chimbuko la fasihi.

**Nadharia ya kwanza**, ambayo baadhi ya watu wameiita ya "kidhanifu", yaani yenye fasihi ni Mungu. Nadharia hii ni kongwe sana, ilikuwako hata kabla ya kuzaliwa Kristo. Mathalani, Wayunani wa kale huko Ulaya walikuwa na Miungu wa ushairi na muzingi waliowaita Muse, ambao yasemekana ndio waliowapa watunzi muhu au kariha (msukumo wa kiroho, kinafsi na kijaziba (inspiration) wa kutunga. Maelezo ya wafuasi na nadharia hiyo yanadai kwamba Mungu ndiye msanii mkuu. Kauumba ulimwengu kwa usanii wa ajabu. Mwanadamu pia ni zao la sanaa ya Mungu. Hivyo uwezo wa mwanadamu wa kubuni kampa Mungu, ambaye ndiye msanii mkuu.

Maandishi ya wasomi wa kale wa Kiyunani, hasa Hesiod na Plato, yanaanzia kwenye imani hii.

Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi imekuwapo tangu kuwapo kwa mwanadamu duniani, haikugunduliwa au kutokea katika kipindi Fulani tu cha maendeleo ya mwanadamu, bali ni zawadi ya Mungu kwa wanadamu.

Dosari kuu ya nadharia hii ni kwamba inachanganya imani ya taaluma. Ni nadharia isiyo na uthibitisho au ushahidi kisayansi, hivyo ni ngumu kuijadili kitaaluma.

Dosari nyingine ni kwamba nadharia hii inatafuta chimbuko la vitu vya kitamaduni nje ya maisha ya mwanadamu, na nje ya dunia hii, na hivyo kukanusha athari ya mazingira na mapambano ya mwanadamu katika kumuumba mtu au utamaduni wake.

Katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili, nadharia hii inajitokeza katika kazi za Nkwera (1976) na Ramadhani (Mulika 3:5).

**Nkwera anatwambia:**

"*Ulimwengu, mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo ni Sanaa Kuu ya Mungu. Siyo sanaa nzima lakini, bali ni sehemu tu yake inayotupwa kwenye kioo kwa wakati moja (!) na mwanadamu akaiangalia. Na kila nukta aangaliapo katika kioo hicho huona ufundi mpya, ufundi unaomwajabisha zaidi kila dakika.Sanaa isiyo lugha ya kuieleza kikomo. Kila siku Mwanadamu anatalii, anaongelea na kuranda ndani ya hiyo sanaa, mwenyewe akiwa sehemu ya hiyo sanaa, apate kuiweka sanaa hiyo nzima katika ukurasa mdogo wa akili yake. Ataweza wapi*?(uk.45).

"…..Fasihi ni sanaa inayoambatanishwa na lugha. Ni moja tu, nayo inafanya duara kubwa. Huanzia kwa Muumba, humfikia mtu katika vipengele mbalimbali, cha mwisho akiwa darasani, halafu huungana tena na Muumba wake '(uk.62).

**Nadharia ya pili** inayoelezea chimbiko la fasihi  ni ile inayyodai kuwa fasihi na sanaa zilitokana na sihiri. Istilahi ya "sihiri" hapa ina maana ya uwezo au nguvu ya kimiujiza inayotumiwa na watu kusababisha matokeo fulani. Katika lugha ya Kiingereza istilahi inayotumika ni magic.

Watetezi wa nadharia hii hudai kuwa chimbiko la fasihi na sanaa ni haja ya mwanadamu ya kukabiliana na kujaribu kuyadhibiti mazingira yake. Hata hivyo, katika hatua za mwanzo za

maendeleo ya mwanadamu, haikutimilika ipasavyo kwa kuwa uwezo wa kisayansi na kiteknolojia wa mwanadamu wa wakati huo ulikuwa bado uko katika kiwango cha mwanzo. Hivyo, sihiri – au imani katika miujiza – aghalabu ilichukua nafasi ya sayansi na ugunduzi . Fasihi na sanaa zilichipukakama vyombo vya sihiri hiyo katika kujaribu kuyashinda mazingira. Kwa mfano wawindaji walichora kwanza picha ya mnyama waliyetaka kumwinda kasha wakaichoma picha hiyo mkuki au mshale kwa kuamini kuwa kitendo hicho kitatoke kuwa kweli watakapokwenda kuwinda. Nyimbo walizoimba na maneno waliyonuizia wakati wa kufanya sihiri hiyo ndiyo ushairi wa mwanzo.

Dosari ya nadharia hii ni kwamba inachanganya dhima na chimbuko. Kutumika kwa fasihi katika sihiri hakuthibitishi kuwa sihiri ndiyo chimbuko lake. Sihiri ni amali moja tu kati ya amali nyingi za wanadamu wa mwanzo zilizotumia sanaa na fasihi.

**Nadharia ya tatu** ya chimbuko la fasihi inadai kuwa **fasihi imetokana na wigo** (uigaji). Katika nadharia hi, ambayo kwa lugha ya Kiingereza inatiwa mimesis, inaelezwa kuwa mwanadamu alianza kuwa mbunifu kwa kuiga maumbile yaliyomzunguka, hivyo sanaa za mwanzo mara nyingi zilijaribu kusawiri vitu vilivyomo katika mazingira , kwa mfano wanyama, ndege, miti, watu na kadhalika.

Nadharia hii vilevile ni ya kale, ilianzishwa na wanataaluma wa Kiyunani. Walioieneza zaidi ni Plato katika kitabu chake cha Republic na Aristole katika Poetics. Aristotle (1958) anatuambia.

Plato anauhusisha wingo na dhana ya uungu. Anaeleza kuwa maumbile na vilivyomo ni wigo tu wa sanaa chasili (archetype) za kiungu. Hivyo sanaa ya mwanadamu (hususan ushairi) ambao huiga tu mambo hayo yaliyomo katika maumbile haiwezi kuwa na ukweli au uhalisi, kwa kuwa inaiga maumbile ambayo nayo yanaiga kazi ya Mungu. Hivyo alishauri aina Fulani za ushairi zipigwe marufuku kwa sababu zinapotosha ukweli.

Dosari ya nadharia hii ni kwamba inasisitiza mno uigaji na kusahau suala la ubunifu katika sanaa na fasihi. Ni wazi kuwa kama watunzi na wasanii wangiga maisha na mazingira tu, sanaa yao ingepwaya sana, na haingekuwa tofauti na picha ya fotografia au maelezo ya matendo ya mazingira na matendo ya kila siku ya mwanadamu. Kwa kawaida watu hufurahia sanaa kwa kuwa inawapa kitu ambacho hawakipati katika maisha na uzoefu wao wa kawaida.

**Nadharia ya nne** ya chimbuko la fasihi ni ile ya **kiyakinif**u. Nadharia hii, ambayo imejikita kwenye fikra za Marx na Engels (rej. On Literature and Artm 1976) hudai kuwa mwanadamu ni zao la maumbile asilia ya ulimwengu, kuwa mabadiliko ya mwanadamu kutoka katika hali ya unyama kuingia katika hali ya utu yamechukua mamilion ya miaka, halikuwa tukio la siku au wiki moja tu. Utamaduni, ikiwemo ugha ya fasihi , ni zao la mabadiliko hayo.

Nadharia hiyo inafafanua kuwa mwanadamu alianza kubadilika alipoanza kuwa mfanyakazi, kuzalisha mali, na hivyo kubadili mazingira ya kimaumbile aliyoyakuta. Katika uzalishaji huo wamali, mwanadamu ilibidi ashirikiane na wenzake. Hivyo alihitaji chombo cha kumwezesha kuwasiliana na kuelewana nao. Logha ilianza kama njia tu ya kurahisisha mawasiliano hayo. Baadaye lugha hiyo ikawa chombo cha sanaa yaani fasihi. Fasihi hiyo ya awali ilitumika kama zana ya uzalishaji, yaani kwa lengo hilohilo la kuchapa kazi. Aidha, ilitumika kujenga hisia za kijinsia katika mahusiano ya uzazi, ambao ndio uliokuwa msingi wa pili wa maisha ya jamii ya wakati huo. Kwa kadiri maendeleo ya uzalishaji mali yaliyoongezeka na kumpa mwanadamu muda wa ziada wa kujiburudisha na kustarehe kwa njia ya sanaa, fasihi ilianza kujitenga na kazi za uzalishaji , ikiwa ni sanaa ya burudani au ya shughuli maalumu za kijamii, kwa mfano sherehe, ibada na kadhalika.

Dosari za mtazamo huu ni kwamba baadhi ya maelezo yahusuyo mabadiliko ya mwanadamu kutoka katika usokwe kuingia katika utu, na hatua zake za mwanzo za kujenga utamaduni na lugha, bado ni mambo ya kinadharia ambayo hayajathibitishwa kwa ukamilifu, japo ushaidi unazidi kukusanywa kila uchao kutokana na ugunduzi wa saikolojia, sayansi  za biolojia, kemia na kadhalika. Hata hivyo, nadharia ya kiyakinifu inaeleka kubadilika zaidi kitaaluma kuliko nadharia ya kidhanifu na ile ya wigo.

| | **Zoezi** |
|---|---|
| 1. | Eleza maana (dhana) ya fasihi. |
| 2. | Huku ukitoa mifano eleza chimbuko la fasihi. |

## Marejeo


1. Nkwera, Fr. F. V. (2003), *Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo*. Creative Prints Ltd: Dar es Salaam.
2. Senkoro, F.E.M.K (1987), *Fasihi na Jamii*. Press and Publicity Centre.
3. Wamitila, K.W (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.Vide ~Muwa Publishers Limited, Nairobi.*

# MUHADHARA 17

# Fasihi ya Kiswahili

## 17.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu tunategemea kueleza maana ya fasihi ya waswahili, fasihi kwa kiswahili, fasihi ya Kiswahili na uhusiano uliopo baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

## Malengo ya Muhadhara

Utakapomaliza kuusoma muhadhara huu utaweza kueleza:

i. Maana ya Fasihi ya Waswahili
ii. Maana ya Fasihi kwa Kiswahili
iii. Maana ya Fasihi ya Kiswahili
iv. Aina ya Fasihi ya Kiswahili
v. Uhusiano wa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi

## 17.2 Fasihi ya Kiswahili ni ipi?

Dhana ya "Fasihi ya Kiswahili" imezua mjadala mkubwa miongoni kwa wanataaluma wa miaka ya 1970-1990. kiini cha mgogoro kilikuwa ni madai ya baadhi ya watu kwamba kuna njama za kuwameza waswahili, au kukanusha kuwepo kwa "kabila" hilo la Waswahili (chiraghdin, S., 1974: 35 – 41: Chiraghdini, 1974:57-61: Chiragdin na Mnyampala, 1977" viii – xii; Shariff, 1988: 8:11). Ilidaiwa kwamba Waswahili ni watu wenye asili ya Mwambao wa Afrika Mashariki, na kwamba watu hao wanayo fasihi yao ambayo, japo huelezwa kwa kugha ya Kiswahili, lakini ni tofauti na fasihi inayoandikwa na watu wa bara kwa lugha hiyo hiyo ya Kiswahili. Hivyo kuna njama za kuwapoka Waswahili utaifa na utambulisho wao. Katika kujaribu kuutanzua mgogoro huu, wataalamu mbalimbali walijitokeza kuujadili. Maoni yaliyojitokeza ni ya aina tatu.

Kuna wale waliona kuwa Waswahili ni kabila au taifa mahsusi (Sengo 1987: 217), na hivyo wanayo fasihi yao mahsusi, ambayo ndiyo inayostahiki kuitwa "fasihi ya Kiswahili." Fasihi nyingine zinazotumia Kiswahili ziitwe "fasihi katika Kiswahili".

Kuna walioona kuwa hakuna kabila ya Waswahili, na hivyo, kwa mantiki hiyo, hakuna fasihi ya Waswahili. Mathalan Senkoro (1988:11)alisema.

" Tunaamua kuwa kazi fulani ni ya fasihi ya Kiswahili au la Kutokana na jinsi navyojitambulisha na inavyojihusisha na utamaduni wa Waswahili. Hapa neno "Waswahili" halimaanishi kabila la Waswahili kwani kabila la namna hiyo halipo leo. Waswahili hapa ni mwananchi wa Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla na wala si wale tu wanaoishi katika pwani ya nchi hizi".

iii Kuna wale walioona kuwa fasihi ya Kiswahili ni fasihi yote inayoelezwa kwa lugha ya Kiswahili (mazingwa (1991: 18: Syambo na Mazrui (1992:ix).

Msimamo wetu kuhusu mjadala huu utaelezwa katika kifungu cha kwanza hapo chini. Kifungu cha pili kitazungumzia aina mbili za fasihi ya Kiswahili, yaani fasihi simulizi na fasihi – andishi , na uhusiano wao.

## 17.3 Fasihi ya Waswahili

Madai ya baadhi ya watu kuwa hakuna "Waswahili" hayakubaliki kwa sababu watu hao wapo na wamekuwapo kwa karne nyingi.

Inawezekana kuwa waliitwa au kujiita kwa majina mbalimbali (Waamu, Wapatu, Wamvita, Wapemba, Waunguja n.k.). Hata hivyo, waunganishwa na lugha moja na utamaduni wa aina moja. Wote ni wenyeji wa Mwambo wa Afrika Mashariki na Visiwa vyake, na ndio wajulikanao kwa jina la "Waswahili" .Ikiwa watu hao wapo, basi bila shaka wanayo fasihi yao, ambayo tutataiita"Fasihi ya Waswahili". Mifano mizuri ni Utenzi wa Fumo Liyongo na nyimbo mbalimbali za shughuli za kijamii, mathalani nyimbo ziimbwazo kwenye sherehe, arusi, uvuvi, unyago na kadhalika.

## 17.4 Fasihi ya Kiswahili

Kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika sehemu nyingi za Afrika Mashariki kumeifanya lugha hiyo iwe ni chombo cha fasihi ya watu wote wanaoitumia, hasa tangu walipoingia wakoloni mwishoni mwa karne ya 19. Fasihi hiyo ndiyo tutakayoiita "Fasihi ya Kiswahili" katika muhadhara huu. Hapa tunakubaliana na kauli ya Syambo na Mazrui (1992:ix) kuwa:

**" … hatuna budi kuichukulia fasihi ya Kiswahili kuwa ni ile iliyoandikwa kwa Kiswahili tu , iwapo inazungumzia utamaduni wa Kiswahili au utamaduni mwingineo. Maadamu fasihi hiyo imetumia lugha ya Kiswahili na imefuata mbinu za ufasaha wa lugha hiyo, basi, kwa tafsili yetu, ni Fasihi ya Kiswahili".**

Kuenea kwa Kiswahili ndani na nje ya Afrika Mashariki, na hata nje ya bara la Afrika, na maingiliano kati ya wazungumzaji wa Kiswahili na mataifa mengine, kumezua fungu la fasihi ya kigeni katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano tafsiri mbalimbali. Mifano mizuri ni Biblia, Shakespeare, Mabepari wa Venisi (Mfasiri J.K. Nyerere, OUP 1969), Kitereza Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Nutulanalwo na Bulihwali (TPH 1980). Tafsiri ya mtunzi), hadithi za Alfu Lela – Ulela (Wafasiri E.W. Brenn na f. Johnson, 1928) na kadhalika. Fasihi ya aina hiyo ndiyo tunayoiita "Fasihi kwa Kiswahili".

### 17.4.1 Aina za Fasihi ya Kiswahili

Aina kuu za fasihi ya Kiswahili ni mbili:

(iv) Fasihi Simulizi, na

(v) Fasihi Andishi

#### 17.4.1.1 Fasihi Simulizi

Fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi. Hivyo fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani ya kijamii, na kutawaliwa na mwingiliano wa mambo sita:

- Fanani (msanii)
- Hadhira

- Fani inayotendwa
- Tukio
- Mahali na
- Wakati

**Fanani** ndiye msanii anayetunga na kuiwasilisha fani yake kwa hadhira katika muktadha wa tukio fulani.

**Hadhira** ni wasikilizaji , ambao mara nyingi pia ni washiriki wa sanaa hiyo inayowasilishwa na fanani.

**Fani inayotendwa** ni ile sanaa yenyewe, kwa mfano hadithi, wimbo, methali, kitendawili au utenzi ambayo inawasilishwa na fanani.

**Tukio** ni shughuli ya kijamii ambayo ndiyo muktadha wa utendaji huo wa sanaa, mathalan arusi, kazi Fulani, sherehe, msiba, ibada, vita.
**Mahali** ni eneo mahsusi ambapo sanaa hiyo inatendewa.
**Wakati** ni muda maalumu kihistoria, au majira maalumu , ya utendaji huo.

Kwa kawaida fasihi simulizi hutungwa kichwani kabla ama wakati ule ule wa kutambwa. Tungo fupifupi, kwa mfano nyimbo na baadhi ya majigambo, huweza kutungwa kabla ya kuhifadhiwa kichwani hadi wakati wa uwasilishaji. Hata hivyo, fanani (msanii) huwa na uhuru wa kubadilisha matini (maneno) ya tungo hizo wakati wowote ili kukidhi mahitaji ya muktadha wa utendaji. Kwa upande wa tungo ndefu za kimasimulizi, kwa mfano ngano na tendi, kwa kawaida kiini cha hadithi hubuniwa kabla ya uwasilishaji, nap engine hupokewa na fanani kutoka kwa wasanii waliomtangulia, lakini matini na mbinu za kisanii hutungwa papo kwa papo wakati wa uwasilishaji. Hivyo tungo hizo hazikaririwi kama baadhi ya watu wanavyofikiri.

Kadhalika, hadhira huwa si wasikilizaji tu bali pia ni wachangiaji (kwa mfano waitikiaji) na wahakiki wa sanaa hiyo inayowasilishwa.

Tanzu za fasihi simulizi ni nyingi, na hutofautiana kati ya jamii na jamii, bali kwa jumla tunaweza kuzigawa katika makundi makuu yafuatayo:

**(a) Mazungumzo:**

Baadhi ya tanzu zilizomo katika kundi hili ni: Hotuba, Malumbano ya watani, soga, mawaidha.

**(b) Masimulizi:**

Tanzu mbalimbali za hadithi zinaingia hapa, kwa mfano ngano, hekaya, hurafa,. Kadhalika simulio za kihistoria na kiasili kama vile visakale, mapisi, tarihi, kumbukumbu ns visasili.

**(c) Maigizo:**

Hapa zinaingia tanzu mbalimbali kutegemea shabaha na miktadha

**(d) Ushairi:**

Aina mbalimbali za nyimbo, maghani ya kinafsi, na maghani ya kimasimulizi.

**(e) Semi:**

Misemo ya kisanii yenye kutoa ujumbe, kuonya au kuchemsha bongo, kwa mfano methali, vitendawili, simo (misimu), mafumbo, lakabu.

**(f) Ngomezi:**

Hii ni fasihi simulizi inayowasilishwa kwa kutumia mlio wa ngoma badala ya mdomo; tunaiweka katika kundi la fasihi simulizi kwa vile ishara za ngoma zinazotumika huiga misemo, tamathali na viimbo vya usemaji wa lugha inayohusika.

### 17.4.1.2 Fasihi Andishi

Fasihi andishi ni sanaa ya lugha inayotungwa na kuwasilishwa kwa hadhira (wasomaji) kwa njia ya maandishi.

Kuwapo kwa fasihi andishi hutegemea mambo matatu: mtunzi (ambaye kwa kawaida ndiye mwandishi); hadhira (wasomaji): mchapishaji chapa kazi iliyoandikwa na kuiwasilisha kwa wasomaji katika umbo linalofaa). Kama andiko linalohusika ni ngonjera au tamthiliya (mchezo wa kuigiza), badala ya mchapishaji huenda akahitajika mtoaji, ambaye atatafuta waigizaji mchezo huo mbele ya hadhara.

Fasihi andishi imegawanyika katika makundi makuu mawili" Nudhumu (ushairi) na nathari. Nudhumu ni tungo za kishairi, na nathari ni maandishi ya kimjazo yasiyofuata kanuni za kishairi. Baadhi ya maandishi yako katikati – yaani yatumia mbinu za kinathari na za kinudhumu. Mfano mzuri ni baadhi ya tamthiliya, kwa mfano zile za Shakespeare (Mabepari wa Venisi, khj) au Alamin Mazrui (Kilio cha Haki).

Katika kundi la nudhumu zimo tanzu nyingi, kwa mfano, tenzi, tendi, mashairi, mauve (mtiririko au ushairi – huru), sukui (masivina). Katika kundi la nathari kuna tamthiliya (drama) na hadithi (riwaya, visa na baadhi ya wasifu na tawasifu)

## 17.5 Uhusiano wa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi

Kwa kuwa fasihi andishi hutegemea uandishi, ni wazi kuwa ni fasihi changa zaidi kwa vile haikuwepo kabla ya kugunduliwa kwa maandishi. Isitoshe, ilianza kwa kukopa fani na mbunu kutoka katika fasihi simulizi, na mpaka leo bado inaathiriwa na fasihi simulizi. Kadhalika, fasihi simulizi, kwa kiasi Fulani, huathiriwa na fasihi andishi: kwa mfano baadhi ya hadithi au misemo ya waandishi mashuhuri hutokea kupendwa sana na watu hadi kuingia katika mkondo wa asihi simulizi ya watu hao. Kadhalika, misahafu kama Biblia ni miongoni kwa fasihi andishi ambayo imekuwa na athari kubwa kwenye fasihi simulizi ya mataifa mengi.

Fasihi simulizi na fasihi andishi zina mambo Fulani yanayofanana. Baadhi ni haya yafuatayo:

(a) Zote hutumia ufundi wa lugha ili kuwasilisha ujumbe wake.

(b) Zote hujadili dhamira zinazotokana na migogoro na matatizo ya mwanadamu katika mazingira yake, kama vile maana ya maisha, mapenzi, mauti, upweke, ubinafsi, choyo, tama,

woga , ushujaa, migongano ya kitabaka, migongano ya kijinsia, ndoa, mila, malezi, dini , sayansi n.k.

(c) Zote zina dhima inayofanana, ambayo ni kusawiri maisha na matatizo ya mwanadamu katika mazingira yake, kuliwaza, kuburudisha, kufurahisha, kuelimisha, kuadibu, kuhifadhi mila, maarifa na lugha ya jamii , kutoa ujumbe na kuhifadhi na kueneza itikadi fulani.

(d) Zote huzaliwa, hustawi na hufa kufuatana na wakati.

## 17.6 Tofauti za Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi

Tofauti za aina hizi mbili za fasihi zimeorodheshwa katika jedwali ifuatayo:

| FASIHI SIMULIZI | FASIHI ANDISHI |
|---|---|
| **i. Utunzi** | |
| Kwa kawaida hutungwa papo kwa paop wakati wa utendaji. | Hutungwa kwa utulivu kwa kipindi kirefu kabla ya kuwasilishwa kwa hadhira. |
| **ii. Uwasilishaji** | |
| Huwasilishwa kwa mdomo na matendo. | Huwasilishwa kwa njia ya maadhishi au maigizo. |
| **iii. Mazingira ya uwasilishaji:** | |
| Huambatana na tukio maalumu la kijamii kunako wakati maalumu | Kujisomea au kusomewa. Tamthiliya huweza kusomwa tu au kuonyeshwa hadharani. |
| **iv. Hadhira** | |
| Ni watu wote wa jamii au kundi linalohusika. Hushiriki katika utendaji. | Zaidi ni wale tu wajuao kusoma. |
| **v. Umri:** | |
| Ni fasihi ya kale zaidi | Ni fasihi changa zaidi. |
| **vi. Umilikaji:** | |
| Kwa kawaida ikisha tendwa hugeuka kuwa mali ya jamii. | Kwa kawaida ni mali ya mtunzi. |
| **vii. Lugha** | |
| Hutumia lugha ya hadhira inayohusika. | Hutumia lugha anayoimudu zaidi mtunzi au ile ya wasomaji waliokusudiwa. |
| **viii. Kuhifadhika** | |

| | |
|---|---|
| Huhifadhika kwa njia ya mapokeo. | Huhifadhika kwa njia ya maandishi katika maktaba, hifadhi ya nyaraka n.k. |
| **ix. Kubadilika:** | |
| Hubadilika haraka kutegemea mahitaji ya hadhira na wakati. Ni nadra kudumu katika hali ile ile baada ya mtunzi kufariki. | Haibadiliki kutegemea mahitaji ya hadhira au wakati. Huwezi kudumu katika hali ileile kwa muda mrefu baada ya mwandishi wake kufariki. |
| **x. Marekebisho/Masahihisho** | |
| Mtunzi huweza kusahihisha au kurekebisha kazi yake wakati wa kuiwasilisha au baadaye kidogo kutegemea maoni na hisia za hadhira yake. | Huweza kufanywa wakati wa kutunga au wakati wa kutoa chapa mpya, lakini mara nyingi mtunzi hana fursa ya kuwasiliana na wasomaji wake. Kitabu kikiisha toka mitamboni ni vigumu kukifanyia masahihisho au marekebisho. |
| **xi. Wahusika:** | |
| Hutumia sana wahusika wasiokuwa binadamu k.m. wanyama, mimea, vitu visivyokuwa na uhai n.k. | Zaidi hutumia wahusika wanadamu; mara chache huweza kutumia wahusika wasiokuwa binadamu, k.m. wanyama, mimea, vitu visivyo kuwa na uhai n.k. |

## Zingatia

**Dhana ya Fasihi -** 'Fasihi ni sanaa ya lugha inayoshughulikia masuala yanayomhusu binadamu, matatizo yake, ndoto zake, matumaini yake, migogoro yake na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake.'

**Umuhimu wa Fasihi Simulizi Katika Jamii -** Kwa ujumla, umuhimu wa fasihi simulizi unajitokeza kwenye majukumu yanayohusiana na burudani, elimu, ujitambuaji na ujijuaji, hali ya kujihisi kuwa ni sehemu ya jamii au 'ujijamiishaji' na ukuzaji wa stadi za lugha

## Zoezi

1. Eleza maana (dhana) ya fasihi
2. Huku ukitoa mifano, eleza umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii yako.

## 17.7 Hitimisho

Aina zote hizi mbili za fasihi zina dhima kubwa kwa umma, jamii ikitumiwa inavyopasika. Kauli hii ya mwisho ni muhimu sana kwa kuzingatia ukweli kwamba sio kila kazi ya fasihi inaweza kuleta mchango chanya kwa umma.

Ziko kazi za fasihi zinazoweza kuleta athari hasa kwa jamii. Kwa msingi huo, inafaa uchambuzi wa ndani ufanywe ili kubaini ni aina gani ya fasihi huleta mchango mzuri kwa umma na zipi ni chanzo cha vurugu na matatizo. Umma wenyewe ukipevuka katika masuala mbalimbali ya kifasihi unayo nafasi kubwa ya kujiamulia nini kinafaa na nini hakifai.

## Zoezi

1. Eleza tanzu za fasihi kwa ujumla.
2. Eleza tanzu za fasihi simulizi.
3. Eleza tanzu za fasihi andishi.
4. Eleza sifa za fasihi simulizi.
5. Eleza sifa za fasihi andishi.
6. Eleza sifa za fasihi simulizi dhidi ya fasihi andishi
7. Kwa kutumia mchoro vichambue vipera vya fasihi simulizi

## Marejeo


1. Nkwera, Fr. F. V. (2003), *Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo.* Creative Prints Ltd: Dar es Salaam.
2. Senkoro, F.E.M.K (1987), *Fasihi na Jamii.* Press and Publicity Centre.
3. Wamitila, K.W (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.Vide ~Muwa Publishers*

# MUHADHARA 18

# Fani na Maudhui katika Fasihi

## 18.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu utasoma vipengele vya fani na maudhui na jinsi vinavyohusiana.

## Madhumuni ya Muhadhara

Baada ya kumaliza kusoma muhadhara huu, utaweza :

(i) Kufafanua vipengele vya fani na maudhui.

(ii) Kuhusianisha vipengele vya fani na maudhui

## 18.2 Fani na Maudhui

**Fani** katika kazi za fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia mwandishi kufikisha ujumbe kwa jamii aliyokusudia. Fani inahusisha mambo yafuatayo; Muundo, Mtindo, Matumizi ya lugha, Wahusika naMandhari. **Maudhui** katika fasihi ni yale mawazo yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu mawazo hayo. Nayo,yaliyomsukuma mtunzi kutunga na kusana kazi fulani ya sanaa. Pia katika maudhui kuna falsafa ya mwandishi.

Kuna mitazamo miwili inayojadili uhusiano wa fani na maudhui. Mitazamo hiyo ni mtazamo wa kidhanifu na mtazamo wa kiyakinifu.

Mtazamo wa kidhanifu ni ule unaoona kuwa fani na maudhui ni vipengele ambavyo havina uhusiano wowote, kwamba vinaweza kutenganishwa. Wataalamu kadhaa wanalinganisha fani na maudhui na kikombe cha chai. Kikombe kinachukuliwa kama ndiyo fani na upande mwingine chai iliyomo ndiyo maudhui. Mnywaji wa chai hiyo analinganishwa na wasomaji wa kazi ya fasihi.

Vilevile wanafafanua kuwa fani na maudhui hulinganishwa na chungwa ambalo lina sehemu ya nje na ndani. Maudhui ya kazi ya fasihi yanalinganishwa na nyamanyama za chungwa na fani ni sehemu ya nje (ganda). Kwa ufupi hawa wanaona kuwa fani ni umbo la nje la kazi ya fasihi na maudhui ni umbo la ndani.

Mtazamo huu una udhaifu wake (mkubwa) na unaweza kuwachanganya wasomaji. Kwa sababu hauonyeshi ama kuwakilisha ukweli wa mambo juu ya uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui katika kazi ya fasihi.

Mtazamo wa kiyakinifu unaeleza vizuri ukweli wa mambo ulivyo. Ni kwamba vitu hivi viwili hutegemeana na kuathiriana na wala havitazamwi katika utengano.

Wanafasihi wenye mtazamo huu, wanalinganisha fani na maudhui na sura mbili za sarafu moja, na si rahisi wala sahihi huzitenga na kuzieleza katika upweke, bila kuhusisha upande mmoja na nyingine. Sura moja ya sarafu ikikosekana, basi sarafu hiyo haiwezi kuwa na hadhi ya kisarafu. Jambo la muhimu ni kuona jinsi kitu kimoja (fani) kinavyoweza kukikamilisha kingine (maudhui).

Wanafasihi hawa wanaonesha kuwa kila kimoja cha kigezo cha fani na maudhui kimo ndani ya chenziwe, kushirikiana na kuathiriana katika ama kijenga vizuri au kubomoa kazi ya sanaa.

Kama kazi ya fasihi itakuwa na fani duni, lakini maudhui yake ni mazuri basi hata maudhui yaliyokusudiwa hayatatoa ujumbe unaokusudiwa ipasavyo. Mfano mzuri ni riwaya ya kikasuku zilizoandikwa baada ya Azimio la Arusha zinazojadili dhamira ya ujenzi wa jamii mpya kama vile *Shida, Mtu ni Utu, Ufunguo Wenye Hazina, Njozi za Usiku, Ndoto za Ndaria* n.k. zilisisitiza zaidi maiudhui na kuupuzia kipengele cha fani.

Vile vile kama maudhui ni duni na fani ni bora, pia jamii itapata hasara ya kufikiwa na maudhui yasiyo na maana. Mfano mzuri ni riwaya pendwa zote zimeweka msisitizo kwenye fani na kusahau kipengele cha maudhui. Katika riwaya pendwa kama vile riwaya za upelelezi , mapenzi na uhalifu, zina wahusika ambao hawaaminiki kwani wanapewa sifa ambazo si rahisi kuziona kwa binadamu wa kawaida. (Toa mifano ya riwaya hizo).

Fani na maudhui ni vitu viwili ambavyo huwiana, hutegemeana hatimaye kuathiriana. Uhusiano huo ndio unaojenga kazi bora ya fasihi. Msanii hutumia vipengele mbalimbali vya maudhui katika kuijenga fani na hutumia vipengele mbalimbali vya fani katika kujenga maudhui.

## 18.3 Vipengele muhimu vya fani na maudhui vijengavyo kazi ya fasihi andishi

*Katika fasihi andishi, fani hujumuisha vipengele vifuatavyo*:

Kwanza ni muundo ambao ni mpangilio na mtiririko wa matukio toka mwanzo hadi mwisho. Hapa tunaangalia jinsi msanii alivyounda na alivyounganisha tukio moja na linguine, kitendo kimoja na lingine sura na sura, ubeti na ubeti n.k. Katika hadithi na Tamthiliya muundo unaweza kuwa wa moja kwa moja (Msago), wa Kioo (Rejeshi) au wa rukia. Katika ushairi muundo unaweza kuwa wa Tathnia, Tathlitha, Tarbia au Sabilia.

*Pili, Mtindo*, ambao ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi andishi kwa njia ambayo hatimaye huonesha nafsi au labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo. Katika riwaya, mtindo unaweza kuwa na masimulizi, monolojia au doyolojia na katika tamthiliya mtindo wake ni dayolojia (majibizano). Katika ushairi mtindo unaweza kuwa wa kimapokeo au wa kisasa.

*Kipengele cha tatu ni wahusika ambao hutumiwa na msanii kufikisha ujumbe kwa jamii yake*. Katika hadithi na Tamthiliya kuna wahusika wakuu, wadodo (wasaidizi) na wajenzi. Wahusika wakuu na wadogo wanaweza kuwa wahusika bapa, mviringo (duara) au shinda (wafoili).

*Kipengele kingine ni matumizi ya lugha*, ambayo mwandishi hutumia kuyaibusha mawazo yake katika kazi hiyo. Vipengele vya lugha wanavyotumia sana ni:

- Matumizi ya semi – Misemo, Nahau, Methali, Misimu, Mafumbo n.k.
- Matumizi ya tamathali za semi
- Matumizi ya mbinu nyingine za kisanaa
- Matumizi ya taswira
- Matumizi ya ucheshi

*Pia kuna Kipengele cha Mandhari hii ni sehemu ambapo matukio muhimu ya kazi ya fasihi hutokea*. Mandhari inaweza kuwa ya kubuni au ya kweli. Katika masimulizi mengi ya kihistoria mandhari yake ni ya kweli na kazi za kubuni mandhari yake ni ya kubuni.

*Kipengele kingine ni jarada* kazi za fasihi huwa na michoro au picha na hata rangi kwenye majarada yake.Inawezekana majarada hayo yakawa na uhusiano na dhamira au maudhui ya kazi zinazohusika.Picha hizi huweza kuwa kielekezi muhimu cha fani kwenye uchambuzi wa kazi ya kifasihi.mfano picha za majarada ya Nyota ya Rehema ya M.S.Mohamed,Kufa Kuzikana ya K.Walibora,Babu alipofufuka ya M.S.Mohamed na Bina-Adamu ya K.W.Wamitila na nyingi nyinginezo Hata hivyo ni muhimu kutambua kuwa sio kazi zote za kifasihi ambazo zinaonesha uwiano kati ya majarada yake na yaliyomo.

***Vipengele vya maudhui, kipengele cha kwanza ni dhamira.***

Dhamira ni wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya fasihi andishi. Dhamira hutokana na jamii. Katika dhamira, kuna dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo.

*Kipengele cha pili ni mtazamo wa mwandishi*. Hapa ni hali ya kuyaona mambo katika maisha kwa kuzingatia mazingira aliyonayo msanii mwenyewe. Mtazamo wa msanii unaweza kuwa wa kiyakinifu au wa kidhanifu.

*Kipengele kingine ni msimamo wa mwandishi ambayo ili hali ya mwandishi kuamua kufuata na kushikilia jambo fulani*. Jambo hili linaweza kuwa halikubaliki na wengi, lakini yeye atalishikilia tu.

Msimamo wa msanii ndio unaosababisha kazi ya sanaa iwe na mwelekeo maalum na hata kutofautiana na kazi za wasanii wengine.

*Kipengele cha nne ni falsafa ya mwandishi*. Ambao huu ni mwelekeo wa imani ya msanii. Msanii anaweza kuamini kwa mfano "Mungu hayupo".

Maadili na ujumbe ni kipengele kingine cha maudhui.Katika fasihi andishi, ujumbe ni mafunzo mbalimbali ambayo hupatikana baada ya kusoma kazi Fulani ya fasihi andishi.

*Mwisho, migogoro, ambayo ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi ya fasihi*. Katika migogoro tunapata migogoro kati ya wahusika ama vikundi vya wahusika, familia zao, matabaka yao n.k. na migogoro hii mara nyingi hujikita katika mahusiano ya jamii. Migogoro yaweza kuwa ya kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na kinafsia.

## 18.4 Wahusika katika Fasihi ya Kiswahili

*Wahusika ni watu*, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia fulani za watu katika kazi za fasihi.

**Mitazamo mbalimbali juu ya Mhusika ni nani?**

Jonathan Culler katika kitabu chake cha Structural Poetics anasema kuwa uhusika ni kipengele cha msingi katika riwaya, kwani kila tukio lipo ili kumfafanua mhusika na maendeleo yake. Naye Barthes katika kitabu hichohicho anasema kuwa mhusika ni kitu kilichochorwa kwa fikra (maneno) kwa msingi wa vielelezo vya kitamaduni, kwa maana kwamba mhusika wa fasihi ya jamii fulani ataeleweka vizuri na kwa urahisi zaidi na jamii hiyo husika.

Nao Kasper na Wuckel wanasema kuwa mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi, na ni kiini cha vyote vipya, dhamira na mada za fasihi: Wanaendelea kudai kuwa katika mhusika kuna uwili: kwanza kuna usawiri wa kisanaa na mtu kwa upande mmoja, na sura ya mtu kwa upande mwingine. Yaani, katika mhusika kuna hali ya welekeo binafsi (subject) na uhalisi (object). Aidha, dunia ni ghala ya wahusika wa namna mbalimbali kwa fikra, hisia na utendaji, na hayo ndiyo yanayosababisha maendeleo tofauti.

Aristole akizungumzia mwigo katika utanzu mkuu wa zama zake, yaani tanzia, alisema kuwa mhusika hufunua uadilifu na kuonyesha lipi zuri baya, kwani tanzua tanzia ni mwigo wa watu.

Naye Hegel, alisema kuwa mhusika ni kitovu katika usawiri wa kisanaa, na anapaswa kutazamwa katika utatu huu:

a. Kama mtu binafsi mkamilifu;
b. Kama mtu katika upekee;
c. Kama mtu mwenye tabia maalum ililiiyojijenga ndani yake.

Karl Marx na F rederick Engels, kwa kutumia upembuzi wa kiyakinifu, walikubaliana na Hegel kuhusu umuhimu wa mhusika, isipokuwa utatu wake usiangaliwe katika ombwe, bali katika mazingira yake kama ifuatavyo:

a. Kama mtu binafsi, kwa sababu ni zao la upekee usioweza kujirudia;

b. Kama mtu tabaka, kwa sababu ni kiwakilishi cha kijamii kinachosimamia tabaka, au kikundi maalum na maendeleo maalum ya kipindi cha historia;

c. Kama mtu jamii, kwa sababu ni mtu mwenyewe sifa za mtu na za kijamii.

Sifa mbili ni bayana, kwani hujionyesha kupitia matendeo. Lakini sifa ya tatu ni ya kidhahania, au ya kufikirika.

Kutokana na ufafanuzi huu mhusika, tunaona kuwa wahusika ni watu au viumbe katika kazi ya fasihi waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu katika maisha halisi. Wahusika katika hadithi za mapokeo na baadhi ya hadithi fupi, kwa kawaida huwa ni wanyama, wadudu, mimea, mashetani, miungu, n.k. kama ndio wahusika wakuu. Kitabia, wahusika hawa hugawika katika makundi makubwa ya ubaya na wema. Katika riwaya, hasa zile za mwanzomwanzo (za akina Shaaban Robert, Mathias Mnyampala na Faraji Katalambullah), uundaji wa wahusika uliathiriwa na ule wa hadithi za kimapokeo. Lakini wahusika katika riwaya halisi huwa ni wahusika halisi wanaoendana kwa karibu sana na maisha ya kila siku kwa sura yao, mavazi yao, lugha yao, na hulka yao kwa ujumla. Na kitabia, hawagawanyiki kwa urahisi katika makundi mawili, bali huwa na tabia mchangamano: *hawana sifa za uungu na kuwa wazuri moja kwa moja, wala hawana sifa za shetani wakawa wabaya mia kwa mia.*

Je, ni jambo gani huwezesha mabadiliko ya mhusika? Sababu ya msingi ni kule kujitokeza kwa wajibu mpya wa fasihi kutoka kipindi kimoja hadi kingine unaotelekezwa na ukweli wa maisha, kwa njia ya mahusiano ya kijamii. Mhusika wa kipindi cha ukoloni hawezi kuwa na wajibu sawa na mhusika wa kipindi cha baada ya Azimio la Arusha; wala kamwe hawezi kuwa sawa na Yule wa baada ya kufia kwa uchumi huria.

## AINA ZA WAHUSIKA KATIKA FASIHI

### (i) Wahusika Wakuu

*Hawa ni wale ambao wanajitokeza kila mara katika kazi ya fasihi tangu mwanzo hadi mwisho*. Wahusika hawa hubeba kiini cha dhamira kuu na maana ya hadithi yote. Vituko na matendo yote hujengwa kuwahusu ama kutokana nao. Mara nyingi jambo hili limewafanya wahusika wakuu wa kazi za fasihi

wawe "midomo" ua wasanii. Wawe vipaza sauti vya Watungaji. Wahusika Wakuu hasa wa riwaya na tamthiliya huchorwa na Wasanii kwa mapana na marefu ya maisha na tabia zao ili kuukamilisha unafsi wao.

**(ii) Wahusika wadogo/wasaidizi**

*Hawa hujitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi ili kuukamilisha ulimwengu wa kazi hizo*. Hawa husaidia kujenga dhamira flani katika kazi ya fasihi, lakini mradi dhamira hiyo ni ndogo, basi hata wahusika hao tutawaita kama ni wadogo. Wakati mwingine husaidia kuijenga dhamira kuu ya kazi ya kazi ya fasihi, lakini, kwa sababu nafasi yao ni ndogo sana katika kuutoa msaada huo, basi hawa tunawaita wahusika wadogo.

**(iii) Wahusika wajenzi**

*Hawa ni wahusika ambao wamewekwe ili kuikamilisha dhamira na maudhui fulani*, kuwajenga na kuwakamilisha. Wahusika hawa wawili; yaani wahusika wakuu na wahusika wasaidizi.

Wahusika wakuu na wadodo tunaweza kuwaweka katika makundi makuu matatu:

**(i) Wahusika Bapa**

*Hawa ni wale wasiobadilika kitabia au kimawazo kulingana na mazingira au matumio ya wakati wanayokutana nayo*. Wahusika bapa tunaweza kuwagawanya kwenye makundi mawili:

Wahusika Bapa – Sugu – hawa wanakuwa sugu katika hali zote, kiasi amacho hata tunapowaona mahali pengine hali zao ni zilezile, hawahukumiwa bali wao huhukumu tu, hawashauriwi bali wao hushauri tu, madikteta, mfano Bwana Msa katika riwaya za M.S. Abdalla ni mmoja wa wahusika hawa.

*Wahusika Bapa – Vielelzo – Ni wale ambao pamoja na kutobadilika kwao,* wamepewa majina ambayo humfanya msomaji aielewe tabia na matendo yao. Shaaban Robert alikuwa fundi sana katika kuwaumba wahusika wa aina hii, akina Majivuno, Adili, Utubusara n.k. Hapa msanii anatilia mkazo tabia moja inayotawala, kiasi ambacho anaondoa sehemu nyingine zote za sifa za mhusika huyo.

**(ii) Wahusika Duara/Mviringo**

*Hawa ni wahusika ambao wana desturi ya kubadilika kitabia,* mawazo au kisaikolojia. Maisha yao yanatawaliwa na hali halisi za maisha. Hivyo wanavutia zaidi kisanii, kwani wanasogeza hadithi ielekee kwenye hali ya kutendeka au kukubalika na jamii. Mfano ni: Rose (Rosa Mistika), Josina (Pepo ya Mabwege).

**(iii) Wahusika Shinda/Wafoili**

*Hawa wako katikati ya Wahusika bapa na wahusika duara*. Hawakuja kama wahusika duara, lakini ni hai zaidi kuliko wahusika bapa. Tofauti kubwa kati ya wao na wahusika wengine ni kwamba wahusika shinda wanawategemea wahusika duara au wahusika bapa zaidi ili waweze kujengeka. Wanaendeshwa na mawazo ya wahusika wengine. Kwa mfano, katika riwaya za M.S. Abdalla, Najum ni mhusika shinda.

## Zoezi

1. Taja na eleza aina za wahusika.
2. Fani na maudhui ni pande mbili za shilingi. Jadili.

## Marejeo


1. Nkwera, Fr. F. V. (2003), *Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo*. Creative Prints Ltd: Dar es Salaam.
2. Senkoro, F.E.M.K (1987), *Fasihi na Jamii.* Press and Publicity Centre.
3. Wamitila, K.W (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.Vide ~Muwa Publishers*

# MUHADHARA 19

# Uhakiki wa Kazi za Fasihi

## 19.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu tunakusudia kuelezea maana ya mhakiki, sifa anazopaswa kuwa nazo mhakiki, dhima za mhakiki na uhakiki wa fasihi.

## Malengo ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu unatarajiwa kuweza:

- Kueleza kwa usahihi maana ya mkakiki
- Kutaja sifa za mhakiki
- Kufafanua dhima za mhakiki

## 19.2 Mhakiki Ni Nani?

Mhakiki ni mchambuzi na mfafanuzi wa maandishi ya sanaa hasa yale ya kifasihi. Ni jicho la jamii kwa vile katika kazi za fasihi anagundua mazuri pamoja na hatari iliyomo. Huyu ni bingwa wa kusoma na kuchambua maudhui, maadili na ujumbe uliomo katika maandishi ya fasihi.

## 19.3 Sifa za Mhakiki

Mhakiki anatakiwa ajue historian ya mazingira yaliyomkuza mwandishi. Mhakiki ili aweze kuifanya kazi yake anapaswa aelewe vema historia ya mwandishi na jamii yake inayohusika. Aelewe asili ya mwandishi, historia yake na utamaduni wake kwa ujumla. Kutokana na hali hii, mhakiki anaweza kuelewa kama mwandishi amefanikiwa kueleza ukweli wa maisha ya watu yaani jamii inayohusika.

Mhakiki anatakiwa kuelewa histori na siasa ya jamii inayohusika. Hii itamwezesha kuyaelewa matatizo ya jamii hiyo. Mhakiki lazima aifahamu barabara jumuiya ambayo mwandishi aliandika juu yake ili aweze kuandika uhakiki imara, ama sivyo atakwama na kuandika uhakiki dhaifu. Mhakiki anapaswa kuelewa historia ya watu ambao maandishi yao hayo yanawahusu, bila kuifahamu historia yao, itakuwa vigumu kwake kueleza bayana baadhi ya mambo ambayo mwandishi aliandika na kwa nini aliandika hivyo. Uhakiki wake ukisomwa na watu wanaoishi katika jamii hiyo si ajabu kusema yeye si mhakiki. Mhakiki, huangalia jinsi gani mwandishi ameiwakilisha hali halisi ya jumuiya na historia ya watu hao.

*Mhakiki ni muhimu awe amesoma kazi mbalimbali za fasihi na siyo ile tu anayoifanyia uhakiki.* Hii itamsaidia kuwa na ujuzi zaidi katika uwanja wa uhakiki.

*Mhakiki anatakiwa asome tahakiki za wahakiki wengine katika uwanja wa fasihi na hata nje ya jamii yake ili kupata upanuzi zaidi katika kazi ya uhakiki.* Hii itamsaidia kutoa tahakiki bora zaidi kwani atakuwa amejifunza yale yaliyo mazuri na kuepuka makosa waliyofanya wengine.

Mhakiki lazima awe na akili pevu sana ili aweze kung'amua mambo na akishayang'amua ayaandike kwa lugha rahisi ili mawazo yake yasomeke na kila mtu kwa urahisi, yaani atumie lugha ambayo itawatumika wasomaji wake.

*Mhakiki lazima ajiendeleze katika taaluma mbalimbali ili aweze kuwa na mawazo mengi ambayo yatamsaidia kuhakiki maandishi mbalimbali.*Mhakiki hodari huichonga jamii yake kimawazo. Huiimarisha isitetereshwe au kupofushwa na waandishi wapotoshi.

*Mhakiki anapaswa kuwa na uwezo wa kuchambua mambo kisayansi bila kutonesha hisia za wasomaji*. Asiwe na majivuno na awaheshimu anaowahakiki na anaotaka wasome uhakiki wake, asichukie au kusifia tu kazi za waandishi kwa sababu zake binafsi bila kueleza ukweli wa kazi hiyo. Mhakiki ni rafiki wa mwandishi na wasomaji. Kwa hiyo, mhakiki lazima awe fudi katika kutoa hoja zake na lazima ziwe zinagonga, zenye kuibua udadisi na kuathiri.

*Mhakiki anapaswa asiwe mtu wa kuyumbishwa na maandishi au maeneo ya wahakiki au watu wengine*. Tunategemea asme kweli kuhusu kazi hiyo. Mahusiano baina ya mhakiki na mwandishi yasiathiri uhakiki wake.

Mhakiki anapaswa awe na uwezo wa kutumia mkabala sahihi kulingana na kazi anayoifanyia uhakiki. Mikabala humwongoza mhakiki kuchambua vema kazi za fasihi.

## 19.4 Dhima za Mhakiki

*Kuchambua na kuweka wazi funzo linalotolewa na kazi ya fasihi*. Hapa mhakiki anatoa ufafanuzi wa kimaudhui wa kazi ya fasihi. Mhakiki husoma kwa uangalifu kazi ya fasihi, baada ya kusoma kwa makini, hutafakari na kuchunguza maudhui, Maadili , na ujumbe ambao mwandishi amekusudia kuwafikishia wasomaji wake na jamii inayohusika.

*Kuchambua na kufafanua picha za kisanii zilizotumika katika kazi ya fasihi*. Mhakiki huwasaidia wasomaji ili wasishindwe kuyaelewa maudhui barabara kutokana na kukakanganywa na usanii, matumizi, mathalani ya Ishara na baadhi ya mbinu ambazo zinaweza kumkanganya msomaji ambaye hajapata utaalamu mkubwa wa kuchambua. Mhakiki kwa kufichua ishara Fulani ina maana kuwa amemsaida msomaji kupata ujumbe kikamilifu.

*Kuhusu matumizi ya picha, kwa kawaida, lugha ya picha ina mguso sana na huibua hisia aina na hata kuchekesha au kuwafanya watu walie machozi*. Mhakiki sharti awambie kwamba, matumizi ya picha ni mbunu mojawapo inayosaidia maudhui kuwaganda wasomaji. Picha inayochekesha, kufurahisha, kukejeli n.k. haikomei pale tu kwani baada ya kucheka n.k. msomaji huathiriwa sana kinafsia na aghalabu huachiwa funzo fulani. Hivyo mhakiki lazima achambue na kuiweka wazi funzo ambalo linatolewa na picha hiyo.

*Mhakiki ana dhima ya kumshauri mwandishi ili afanye kazi bora zaidi*. Mhakiki anamfundisha mwandishi juu ya yale anayoyasema yanavyoweza kupokelewa na jamii. Humwonesha msanii uzuri na udhaifu wa kazi aliyosaini kitendo hiki humfanya anavyoelekezwa na mhakiki, na hivyo humfanya awe na nafasi nzuri ya kuirekebisha kazi hiyo atakapoishulikia kazi nyingine. Kwa msingi huo mhakiki anaweza kulaumu au kusifu/ kumpongeza mwandishi wa kazi yoyoe ya kisanaa.

*Mhakiki ana dhima ya kumwelekeza msomaji ili apate faida zaidi kuliko yale ambayo angeweza kuyapata bila dira ya mhakiki*. Mhakiki huifunza jamii (wasomaji) namna ya kupokea na kuifurahia kazi ya sanaa. Vilevile mhakiki huwasaidia wasomaji kuyabaini maandishi yaliyo sumu kwa jamii. Mhakiki lazima ayafichue maandishi hayo ili yasieneze sumu kwa jamii inayohusika.

*Mhakiki ni kiungo muhimu kati ya jamii na msanii.* Mhakiki ndiye anayeitambulisha na kuelezea kazi ya msanii kwa hadhira. Vile vile mhakiki huchukua mawazo ya wasomaji na kuyapeleka kwa mwandishi. Humtahadharisha msanii kuhusu makosa aliyoyafanya katika kuikabili kazi yake na wakati huo huo anaionesha jamii udhaifu uliomo katika kazi hiyo ya fasihi.

*Mhakiki ana dhima ya kukuza kiwango cha utunzi na usomaji wa kazi ya fasihi*. Kutokana na ushauri anaoupata mwandishi kutoka kwa mhakiki, humfanya awe makini zaidi wakati wa kushughulikia kazi nyingine. Vile vile wasomaji wanakuza kiwango chao cha usomaji kwa kufuata mawaida ya mhakiki.

*Mhakiki ana dhima ya kusema wazi kuhusu kiwango cha maandishi anayoyahakiki*.Akisema wazi kwamba maandishi hayo yako katika kiwango cha chini, mara mwandishi huyo asilia atakapoamua kutunga tena, atashawishika kuandika maandishi yaliyo kwenye kiwango cha juu zaidi. Na waandishi wengine watapatiwa msukumo wa kuandika maandishi yaliyo kwenye kiwango cha juu pia. Na hivi ndivyo mhakiki anavyosaidia kukuza na kuendeleza maandishi ya taifa lake.

*Mhakiki ana dhima ya kumsaidia msomaji kuyabaini maandishi yaliyosumu kwa jamii*. Mhakiki sharti aseme wazi ayafichue maandishi ya namna hiyo. Kuna maandishi ambayo huwachekesha na kuwaburudisha wasomaji sababu yameandikwa kwa namna hiyo, na kumbe yaneneza sumu, na maandishi haya yanazorotesha maendeleo ya jamii, hivyo mhakiki huyafichua maandishi kama haya.

*Mwisho, mhakiki anatakiwa kuheshimu na kuthamini kazi za waandishi na kuzifanyia haki*. Jambo la msingi (lazima) kuzingatia ni kwa mhakiki afayapo kazi yake huwa vitani. Mhakiki anapaswa kujua namna ya kuwanasa wasomaji bila wao kujitambua na kuwa na uwezo au kuchambua kisayansi mambo bila kutonesha hisia za wasomaji. Anatakiwa asiwe na majivuno na aheshimu anaowahakiki na anaowataka wasome uhakiki wake, awachukue hatu kwa hatua kifalsafa hata waone vigumu, na haiwezekani kupingana naye.

*Kwa kuhitimisha, mhakiki ni mtu muhimu sana katika kazi za fasihi*. Kazi ya sanaa ya uandishi ni kama chakula kilichokwishapikwa na kuungwa vizuri. Uhakiki ni sehemu mbalimbali za ulimi zenye kuifanya jamii ikubali utamu wa chakula hicho; uchungu au ukali wa chakula hicho na igundue uchungu wa chakula hicho au ukali wake.

## 19.5 Uhakiki wa Fasihi

Nkwera (2003) amechunguza na kuona kwamba mara nyingine mhakiki hulazimika kulinganisha kazi za kifasihi. Kazi hizo zinaweza kuwa zinafanana au zinatofautiana. Ulinganisho huo utazingatia vipengele vyote vya fani na maudhui. Mhakiki anatazamiwa aone ubora au upungufu katika kazi na jinsi zinavyozidiana.

Vigezo vinavyotumiwa katika kulinganisha kazi za fasihi ni vile vile vya ukweli, uhalisi na umuhimu. Vigezo hivyo vitapima dhamira, ujumbe, falsafa, wahusika na matumizi ya lugha.

Uhakiki wa kazi za fasihi unajumuisha kuzingatia kazi hiyo kwa kuisikiliza au kuisoma; kuchambua vipengele vya fani na maudhui vinavyoijenga kazi hiyo. Hatimaye mhakiki atatoa maoni kuhusu ubora au ubaya wa kazi hiyo na hukumu ya kazi ipi bora kuliko nyingine.

**Vipengele Vya Uhakiki**

1. Maudhui
2. Fani

### 19.5.1 Uhakiki wa Maudhui

Katika kuyahakiki maudhui ya fasihi, zingatia yafuatayo:

i Soma na uielewe habari nzima, kisha uieleze kwa muhtasari.

ii Itambulishe hadhira au wazo kuu la mchezo husika kwa sentensi mbili au tatu.

iii Onesha mapendekezo au mawaidha ya mwandishi, msimamo na mtizamo wake wa mambo kutokana na mchezo huo.

iv Chunguza falsafa ya maisha ambayo mwandishi anaielezea: k.m. Je, mwandishi anaelezea hali halisi ya maisha au ni nadharia tu za uchawi au ni maisha ya njozi yasiyo na ukweli ndani yake?, nk.

v **A**inisha matatizo na migogoro inayojitokeza katika mchezo huo na sababu zake.

vi Mtambulishe mhusika mkuu katika mchezo mzima.

vii Onesha njia/mbinu zilizotumika ili kumuinua au kumuangusha mhusika mkuu.

viii Onesha njia/mbinu zilizotumika ili kuyakabili na kuyatatua matatizo hayo na migogoro iliyojitokeza katika mchezo huo.

ix Onesha majibu/matokeo ya juhudi zote alizotumia mwandishi ili kulikabili suala au tatizo linalozungumziwa katika mchezo huo.

x Fanya tathmini ya kupima kama mwandishi amefanikiwa, katika maelezo yake, kulifikisha lengo alilokusudia kwa hadhira lengwa.

xi Na kama hakufanikiwa kulifikisha lengo lake kwa hadhira husika, eleza kwa nini kashindwa.

### 19.5.2 Uhakiki wa Fani: Wahusika

Uhakiki wa Fani Wahusika unatakiwa ushughulikiwe kwa kuzingatia na kuchunguza mambo mawili makubwa:

(i) ***Wahusika***

Yuko mhusika mkuu au wako wahusika wakuu.

Mhusika mkuu au wahusika wakuu hutambulishwa kwa maswali matatu:

(a) Hadithi imejengwa juu ya nini?

(b) Je, mhusika huyo hutokea mara nyingi akitenda mambo, kuongea au kuzungumziwa na wahusika wenzake?

(c) Je, mhusika anatoa uamuzi unaofikisha mchezo kwenye kilele au upeo wa weledi wa hadhira yake?

Wahusika wadogo nao huunda makundi matatu:

(a) Wahusika wadogo walio maarufu au muhimu.

(b) Wahusika wadogo walio maarufu kidogo.

(c) Wahusika-Wadogo wanaofanya mazingira katika mchezo ambayo yanamsukuma Mhusika-Mkuu aamue au asiamue jambo kama alivyokusudia hapo awali.

Jinsi wahusika walivyoundwa na kulelewa mambo muhimu ya kuchunguza katika kipengele hiki ni:

(a) Sura, tabia, kazi zao maishani katika jamii, na katika mchezo.

(b) Uhusiano wao katika Jamii:

- Je, wanaendelezana kimaisha, au kila mmoja kivyake?
- Je, wanagongana kitabaka, kifikra, kiuchumi, kielimu, nk?
- Je, wanasadikika na kupokeleka na jamii yao, au na hadhira kwa jumla?

### 19.5.3 Uhakiki wa Fani: Muundo

Kipengele hiki kinachunguza jinsi mchezo wenyewe ulivyotengenezwa. Maswali ya kujiuliza ni haya:

(a) Mwanzo wa mchezo ni wapi na unakomea wapi?

(b) Kilele cha mchezo ki wapi; kimeanzia na kuishia wapi?

(c) Sehemu za mchezo ni zipi? Yaani mchezo una vitendo vingapi (sehemu ngapi) na maonesho mangapi?

(d) Ni mandhari gani yaani sura ya mahali na mzingira ya wakati yanasawiriwa katika mchezo?

### 19.5.4 Uhakiki wa Sanaa: Kufaulu Kwa Mtunzi

Uamuzi wa kwamba mtunzi amefaulu ama hakufaulu katika utunzi wa mchezo wake, hatuna budi kuchunguza au kujiuliza mambo yafuatayo kuhusu sanaa aliyoitumia katika mchezo wake.

(a) Je, lugha aliyoitumia mwandishi ni fasaha, (yaani ni lugha sahihi kisarufi, na ni rahisi kueleweka kwa watu wengi waliokusudiwa wauelewe mchezo wake?

(b) Je, viashiria au ishara na mifano iliyotumika ili kulijenga wazo kuu; kuunda visa, mazingira ya wakati na mahali; kubainisha ukale dhidi ya usasa (mapinduzi); nk. yamechangia kufanikisha azma ya mchezo?

(c) Je, ukubwa wa hadhira au jamii inayoweza kufikiwa na ujumbe wa mchezo na ikauelewa fika na kuathirika nao vibaya au vizuri, unaridhisha?

(d) Je, maudhui yatokanayo na mchezo huu yanatoa jawabu au suluhisho la kufaa kuhusu migogoro inayojitokeza katika jamii hiyo? Je, yanachochea zaidi vurugu akilini kuhusu mgogoro uliopo?

(e) Je, semi zimetumiwa katika mchezo ili kusisitiza au kukejeli mambo yanayosadikiwa na kufuatwa kama kanuni au desturi katika jamii?

(f) Je, suala linalojadiliwa linawagusa watu wa kiwango gani kielimu katika jamii hiyo?

(g) Je, suala la wachache katika jamii, yaani ni tabaka dogo tu la watu?

(h) Je, suala la watu wengi katika jamii, yaani ni tabaka kubwa la watu?

(i) Je, suala la watu wote katika jamii?

(j) Je, suala linalojadiliwa lina umuhimu gani kwa jamii kwa wakati huu?

(k) Je, mwandishi amewatumia wahusika wake ipasavyo katika kuliweka bayana wazo kuu kwa hadhira husika, na uwe mfano bora kwa hadhira kuwaiga au kutowaiga kwa vile alivyowamulikia kwa undani maisha yao kwa vitendo na maneno yasemwayo mchezoni?

### 19.5.5 Uhakiki wa Kichwa cha Mchezo

Kichwa cha mchezo ni kama nembo. Kwa hiyo, nacho pia inafaa kihakikiwe. Maswali ya kujiuliza kuihusu ni kama ifuatavyo:

(a) Je, kichwa kilichowekwa kweli kinawakilisha wazo kuu, au kiini cha habari?

(b) Je, ni wazo mojawapo tu linalojitokeza katika mchezo huu katika jumla ya mawazo? au

(c) Ni neno tu la kuamsha udadisi wa msomaji na labda la kuwavutia wanunuzi wa kitabu chake?

| | Zoezi |
|---|---|
| 1. | Elezea mambo yanayotakiwa kuzingatia unapohakiki;<br>(a) Maudhui,<br>(b) Wahusika,<br>(c) Fani muundo,<br>(d) Sanaa ya kufaulu au kutofaulu kwa mtunzi,<br>(e) Kichwa cha mchezo. |
| 2. | Hakiki matumizi ya maneno katika shairi la<br>**'Dunia ina hadaa shetani mtu kwa mtu'**<br>Utulize moyo wako, ulimwengu ni hadaa,<br>Usiache kifo chako, vizuri vingi vijaa, |

| | |
|---|---|
| | Ibilisi kaja kwako, dhamiri ni kukuvaa,<br>Dunia ina hadaa, shetani mtu kwa mtu.<br><br>Waweza ukawa kwako, na nyumba ikakujaa,<br>Kwa furaha na vicheko, na mapambo ya kuvaa,<br>Ukazusha sokomoko, watu wakaja shangaa,<br>Dunia ina hadaa, shetani mtu kwa mtu.<br><br>Sasa wapata umbuko, uendapo hutokaa,<br>Lako liwe hangaiko, mashitaka kwa jamaa,<br>Shoga uwape vicheko, kwa kujitia fadhaa,<br>Dunia ina hadaa, shetani mtu kwa mtu.<br><br>Duniani kuna miiko, kubali ukikataa,<br>Usijitie sumbuko, kwa kuongeza tamaa,<br>Shukuru kwa Mola wako, upatacho kinafaa,<br>Dunia ina hadaa, shetani mtu kwa mtu.<br>Sengo (1992). |
| **3.** | Eleza maana ya (a) muundo, (b) matumizi ya lugha, (c) wahusika, katika fasihi. |
| **4.** | Chagua kazi mbili za fasihi na kwa kutumia mifano hiyo, hakiki mandhari na wahusika. |
| **5.** | Hakiki shairi lifuatalo:<br>Tulia nyumbani mwako, akichafuka upepo<br>Mpenzi wangu shwahiba, sikia langu tamko,<br>Upatacho ni kushiba, sitaki muhangaiko,<br>Ongeza yako mahaba, na kupamba nyumba yako,<br>Tulia nyumbani mwako, ukichafuka upepo.<br><br>Kimbunga si kitu chema, utatupa roho yako,<br>Ukianza kulalama, utaeneza vicheko,<br>Utapata na lawana, wambulie sikitiko,<br>Tulia nyumbani, mwako, ukichafuka upepo. |

Hizo ni pepo dharuba, maradi na tetemeko,
Zisikutie msiba, ukahama nyumba yako,
Tundu bovu ni kuziba, juwa shukrani yako
Tulia nyumbani mwako, ukichafuka upepo.

Siri ifane kikuba, kwani ni aibu yako,
Tia ndani ya mokoba, sitowelako tamko,
Utawezesha ujuba, watarudi watokako,
Tulia nyumbani mwako, ukichafuka upepo.

Wameyasema mababa, pavumapo pema mwiko,
Yalokupa sihaba, aya juwa mola wako,
Kila shida ina tiba, subiri ndio tambiko,
Tulia nyumbani mwako, ukichafuka upepo.

Mpenzi wangu wa huba, nakuaga ni mwenzako,
Penye hasha ni kuziba, tuliza sukari yako,
Usiache pakushiba kwa kuhofia vituko,
Tulia nyumbani mwako, ukichafuka upepo.

Sengo (1992).

# Marejeo

1. Nkwera, Fr. F. V. (2003), *Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo.* Creative Prints Ltd: Dar es Salaam.

2. Senkoro, F.E.M.K (1987), *Fasihi na Jamii.* Press and Publicity Centre.

3. Wamitila, K.W (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.Vide ~Muwa Publishers*

# MUHADHARA 20

# Utungaji

## 20.1 Utangulizi

Katika muhadhara huu tunatarajia kuelezea maana ya utungaji, aina za insha. Pia tutaeleza uandishi wa insha na uandishi wa barua za kirafiki na za kikazi.

## Malengo ya Muhadhara

Baada ya kusoma muhadhara huu, unatarajiwa uweze:

- Kueleza maana ya utungaji
- Kutaja aina za insha.
- Kutofautisha insha za wasifu na insha za hoja.
- Kuandika barua za kirafiki na barua za kikazi

## 20.2 Insha/Utungaji

Insha au Utungaji ni maandishi yanayoeleza habari juu ya kitu, mtu au jambo fulani. zipo aina mbili kuu za insha: insha za maelezo, na insha za mazungumzo.

## 20.3 Aina za Insha

***(i) Insha za Maelezo***

Aina hii ya insha inajumuisha:

(a) Masimulizi ya mambo yaliyotokea (visa).

(b) Hadithi za kubuni

(c) Maelezo kuhusu au kutokana na msemo au methali fulani.

***(ii) Insha za Mazungumzo***

Aina hii inajumuisha:

(a) Mijadala

Katika insha ya kujadili, huwa kuna mambo mawili au zaidi;

Mwandishi anaweza kuzungumzia pande zote mbili, halafu atoe uamuzi wake. Lakini pia mwandishi ana uhuru wa kuchagua upande mmoja, ama wa kuunga mkono au kuipinga anwani aliyopewa, na kuzungumzia upande huo huo hadi mwisho.

(b) Mazungumzo/Tamthiliya

Insha za aina hii huwa na mzungumzaji zaidi ya mmoja. Insha hizi pia zinajulikana kama insha za kujibizana. Mmoja akizungumza, naye mwenzake humjibu apo hapo.

## 20.4 Sehemu za Insha

Insha yo yote huwa na sehemu **tatu** muhimu:

***(i) Mwanzo***

Mwanzo wa Insha unakuwa kama salamu. Inafaa uwe wa kuvutia ili msomaji awe na hamu ya kuendelea kuisoma insha hiyo. Katika hatua hii, mwandishi hueleza *maana* ya mada/anwani/kichwa alichopewa. Endapo *methali* ni kichwa cha Insha, mwandishi ataeleza:

(i) maana ya juu,

(ii) maana ya ndani,

(iii) matumizi ya methali aliyopewa katika jamii husika.

Endapo ni Insha ya mjadala, baada ya kueleza maana ya mada, mwandishi ataeleza kama anaunga mkono au ataupinga mjadala. Lakini pia anaweza kuamua kutoa maelezo ya pande zote mbili na halafu atoe uamuzi wake.

***(ii) Maudhui***

Hii ni sehemu muhimu sana katika zoezi nzima la kuiandika Insha; ni kiini cha Insha. Ni sehemu ambayo ina aya kadhaa, na kila aya hujitosheleza kwa kila kitu katika kulielezea jambo moja tu au hoja moja tu.

Wingi wa aya hutegemea wingi wa maudhui aliyonayo mwandishi wa kichwa cha Insha. Urefu wa aya hutegemea uwezo wa mwandishi wa kufafanua wazo linalozungumziwa. Kwa mfano, endapo ni Insha juu ya Maumbile ya Ng'ombe, aya moja inaweza kuwa juu ya kichwa cha ng'ombe. Ayah inaweza kuwa ndefu kuliko aya kuhusu shingo au mkia wa ng'ombe.

***(iii) Hitimisho***

Hitimisho ni aya ya mwisho ya Insha ambayo inaelezea muhtasari wa maudhui yote yaliyoelezwa katika Insha nzima.

(a) Endapo ni Insha ya Mjadala, mwandishi anatoa uamuzi wake baada ya kutoa maoni kuhusu pande zote mbili.

(b) Endapo ni Insha ya Methali, mwandishi anaweza kusisitiza maana na matumizi ya methali, huku akitoa methali nyingine zenye maana sawa au maana kinyume na maana ya methali ya Insha.

## 20.5 Jinsi ya Kuandika Insha

(a) Soma kwa makini mada/kichwa/anwani uliyopewa zaidi ya mara moja, ili uielewe vizuri.

(b) Ifikirie mada/kichwa/anwani kwa muda.

(c) Yaandike mambo muhimu yatakayokuongoza katika kuiandika nsha

Yapitie mambo hayo muhimu ili uhakikishe kwamba yanaenda sawa na anwani: endapo kuna mambo ambayo hayafai, yaondoe; endapo kuna nyongeza, iandike.

(d) Andika methali, misemo na nahau ambazo unadhania zinaweza kukufaa katika uandishi wa Insha yako.

(e) Iandike Insha yako huku ikizingatia kwamba:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Aya ya Kwanza | = | Mwanzo |
| (ii) | Aya ya Pili | = | Kidokezo cha kwanza. |
| (iii) | Aya ya Tatu | = | Kidokezo cha pili. |
| (iv) | Aya ya nne | = | Kidokezo cha tatu. nk. |
| (v) | Aya ya Mwisho | = | Hitimisho. |

(f) Isome Insha yako huku ukirekebisha makosa ya:

(i) Tahajia

(ii) Sarufi

## 20.6 Miundo Mbali Mbali ya Insha

***(i) Kujibu Maswali ili Kuandika Insha***

Katika muundo wa aina hii ya kuandika Insha, maswali yanayoulizwa lazima yatoemajibu ambayo yatasaidia kueleza habari kamili ya mtu, kitu, au jambo fulani. Kwa mfano:

(a) Shughuli za Mwanafunzi/Mtu kunzia asubuhi anapoamka hadi usiku anapokwenda kulala.

(b) Mifugo

(c) Mmomonyoko wa Udongo

(d) Nchi yetu, nk.

***(ii) Kujaza Nafasi ili Kuandika Insha***

Insha yote huwa imesha kuandikwa isipokuwa tu kwenye sentesi fulani fulani za aya kumeachwa nafasi ya kujaza neno, kirai au kishazi kizima ambacho mwanafunzi anatakiwa akijaze ili kuleta maana kamili inayokubalika katika mtirirko mzima wa insha yenyewe.

(a) Kukamilisha insha ambayo umepewa mwanzo wake

(b) Kukamilisha insha ambayo umepewa mwisho wake

(c) Insha za methali

Muundo wa Insha za aina hii ni kama ifuatavyo

(a) Andika maana ya nje na ya ndani inayohusu methali uliyopewa:

(b) Eleza mfano wa kisa (visa) vinavyothibitisha ukweli wa maelezo ya methali.

***(vi) Insha za Kawaida***

Zipo aina mbili za insha za kawaida:

(a) Insha-Hadharishi – ni zile ambazo inafaa mwandishi awe mwangalifu katika kueleza yanayohusu vitu au mambo anayoyaelezea kwa sababu hivi ni vitu au mambo ambayo maudhui yake yanajulikana kwa watu wengi. Kwa mantiki hiyo, insha hizi hazimpi mwandishi fursa ya kubuni maelezo yake binafsi.

(b) Insha-Huru – ni insha ambazo masharti yake ni kinyume na yale ya Insha- Hadharishi. Katika uandishi wa insha-huru, mwandishi ana fursa yote ya kujieleza apendavyo. Anaweza hata kuandika mambo ya kubuni (uwongo); lakini ingemfaa mwandishi, kama angechopeza chembechembe za ukweli katika maelezo yake yaliyokithiri urongo ili insha yake angalau iwavutie wasomaji wake walio wengi wenye kuishi katika imani inayotawaliwa na kweli.

***(vii) Insha Zinazotokana na Picha***

Katika insha za aina hii, mwandishi anapewa picha kadhaa zinaelezea kisa kwa ukamilifu wake. Kutokana na picha hizo, unatakiwa kuziandika sentesi kadhaa ambazo zitakuongoza katika kuikamilisha insha yako, kwa mfano:



***Kielelezo 6.1:*** **Ajali Barabarani**

## 20.7 Malengo ya Insha/Utungaji

Somo la Insha/utungaji linalenga kumpa mwanafunzi mazoezi ya kutunga habari yeye mwenyewe, na jinsi ya kuziwasilisha habari zake kwa watu wengine kwa njia ya mazungumzo au maandishi. Somo hili linashughulikia vipengele vitatu: mazungumzo, kuandika, kusoma, kufahamu na ufupisho (muhtasari).

Jinsi ya kuyaendesha ni ile ile katika vidato vyote, tofauti ni katika viwango vya mifano itakayochaguliwa kushughulikiwa.

### *(i) Mazungumzo*

Shabaha ya somo hili ni kumfunza mwanafunzi kuzungumza na wenzake, aidha kuhutubia hadharani, kujadili hoja, nk. kwa lugha fasaha, bila woga, akaeleweka.

### *(a) Hotuba*

Kuzungumza ni kipawa cha mtu kuweza kuwasiliana na wenzake. Kuna mazungumzo ya ishara, hasa baina ya watu bubu na mazungumzo ya mdomo. Hotuba ni mazungumzo yaliyotayarishwa kwa muda mrefu au mara ile ile ili kutolewa mbele ya watu. Hotuba safi haina budi kuwa na mambo yafuatayo:

- Ukweli wa habari na taarifa.
- Ufasaha wa lugha ipate kupendeza na kueleweka vizuri.
- Nidhamu, yaani adabu njema ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele za watu .
- Mantiki nzuri, yani mfuatano mzuri wa mawazo na fikra.
- Sauti ya kusikika wazi pamoja na ishara zinazoeleweka iwapo hotuba inatolewa mbele ya watu. Ishara siyo za lazima iwapo hotuba inatolewa kwa njia ya redio.

Hotuba zaweza kugawanywa kwa misingi mbalimbali. Baadhi ya misingi hiyo ni:

- Urefu wa Muda wa Matayarisho: Kulingana na uzito wa mada za hotuba zenyewe matayarisho huwa ni ya muda mrefu kwa mada nzito, lakini huwa ni ya muda mfupi kwa hotuba zenye mada nyepesi. Aghalabu, hotuba za dharura huwa na mada nyepesi nyepesi, yaani zinazotolewa papo kwa papo bila ya kupata muda mrefu wa kuziandaa.

- Aina za Hotuba: Ziko aina nyingi za hotuba. Baadhi yake ni:

  (i) Hotuba na Mafundisho ya Kidini; aghalabu, hizi hutolewa miskikitini, makanisani, kwa njia ya redio; lakini pia popote penye mkusanyiko wa waumini husika.

  (ii) Hotuba za Kisiasa na Kiserikali: Kwa mfano; matangazo ya taarifa za kiserikali na chama, fafanuzi za maazimio au sheria, n.k.

(iii) Mihadhara au Masomo ya Darasani: Hizi ni hotuba au mafundisho ya Mwalinu shuleni hasa anapofundisha kundi kubwa la wanafunzi, na hasa wanachuo wa vyuo vikuu.

- Nia ya mzungumzaji katika kuzitayarisha hotuba:

Mzungumzaji au mhutubiaji hujiwekea lengo la hotuba yake:

(i) Kuna hotuba za kuhimiza na kualika watu kutenda jambo fulani;

(ii) Kuna hotuba za kupasha habari ya furaha au ya simanzi;

(iii) Kuna hotuba za kushukuru, kukaribisha wageni, kupongeza na kutoa hongera, kumliwaza na kumfariji mwenye huzuni na masikitiko, (iv) Aidha, kuna hotuba za kushutumu na kukaripia.

- **Risala**

  Risala ni *hotuba* na *barua* wakati huo huo. Mwenye kuzungumziwa husomewa hotuba iliyoandaliwa rasmi kuhusu suala fulani la jamii. Baada ya kusomewa hotuba nzima, mzungumziwa hupewa taarifa hiyo hiyo kwa maandishi kama kumbukumbu ya kudumu.

## Zoezi

1. Andaa hotuba au risala kuhusu

(i) Ufunguzi wa Zahanati na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Uchaguzi wa balozi mpya na kumwaga wa zamani.

(iii) Mgombea ubunge ajitangaza kuomba kura.

(iv) Kumkaribisha kiongozi wa chama au Serikali.

(v) Kuhimiza kilimo cha kufa na kuoana au jambo lingine.

(vi) Kushutumu ulevi, uzururaji na wapika majungu; au wanafunzi wasio na nidhamu shuleni, au kumsuta mwalinu asiyetimiza vema wajibu wake

(vii) Kueleza maana na umuhimu wa utu na uungwana.

(viii) Balozi wa nyumba kumi anawaagiza wanamgambo wake wasake majambazi walioingia tarafani.

(ix) Kiongozi wa serikali akemea utegaji wa kazi.

(x) Kiongozi wa Chama/ vijana ahimiza umma kuhudhuria vikao vya Chama.

(xi) Kuwakaribisha wanaharusi kwenye tafrija.

(xii) Kuagana na kuwatakia fanaka ya maisha wanafunzi wanaomaliza masomo ya kidato cha IV/VI

(xiii) Shukrani toka kwa mtalii (mgeni) wa kiserikali au ya Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya au Mkoa kwa wanafunzi kwa vile wameshiriki vizuri katika ujenzi wa Taifa.

***(b) Mazungumzo kwa Simu***

Simu ni chombo cha kupelekea habari kwa haraka sana, tena ni chombo cha watu wengi duniani; na hali halisi ilivyokuwa leo kuhusu mazungumzo kwa simu ni kama ifuatavyo:

Mazungumzo kwa simu hayana siri. Ni mazungumzo kwa sauti kubwa ili mwenzako aliye mbali aweze kusikia sawasawa usemayo wewe; tena yapitia vituo vya wapokeaji kadhaa. Kwa hiyo zungumza mambo ya lazima, kwa lugha nzuri na kwa adabu za Kitanzania, ikiwa pamoja na kwamba tumeingiliwa sana na usasa.

Simu ni chombo kinachodai kulipiwa, ni ghali. Kwa hiyo, zungumza kwa kifupi, uwape nafasi pia wengine wakitumie kuzungumza na wenzao. Usicheze nayo, vinginevyo, itaharibika haraka na kukuingiza katika hasara kubwa.

Upigapo au upokeapo simu, yafaa kutaja jina lako, pia nambari ya simu yako. Hayo ni kumwezesha mwenzako anayezungumza nawe afahamu kama anazungumza na mtu sahihi, aliyepo kwenye kituo sahihi.

***(c) Mazunguzo-Kimjadala***

Mijadala hujitokeza katika sura mbili kama ifuatavyo:ni ya aina mbili:

Majadiliano ya kuhojiana baina ya pande mbili zenye misimamo tofauti, yaani zinazopingana. Upande mmoja huwa wa watetezi na upande wa pili wa wapinzani.

Majadiliano ya kuendelezana na ya kutafuta pamoja hoja za kupinga au za kuyakinisha kauli fulani.

Nidhamu bora ni kitu muhimu wakati wa majadiliano. Na ili pawe na nidhamu bora wajadilianaji sharti:

- Wawe na shabaha maalumu ya majadiliano yao, watafute kujua nini?
- Mada (kichwa) ya majadiliano ipewe mipaka, yaani ieleweke wazi vipengele vya majadiliano yao. Wasijadili juu ya suala ambalo kila upande umeshikilia kipingele chake tofauti.
- Wapeane nafasi ya kuzungumza kwa uhuru, bila ya kukatizana.
- Washike adabu njema na heshima katika lugha zao. Jambo muhimu ni kwamba wajadiliane wala siyo kubishana na kudadisi jambo kwa nia ya kudadisi tu na kukashifiana. Zuia hasira.
- Pawe na matayarisho yanayopasika ili kutafuta ukweli wa mambo kwa kinaganaga, hasa mambo ya msingi yanayotugusa binadamu: Elimu-Dunia na Elimu-Akhera., Uchumi, Afya, na Uhusiano Mwema.

*Waendeshaji wa mijadala:* Uaendeshaji wa mjadala wowote wa kielimu sharti uchukuliwe kama ni *kikao cha utafiti*. Kwa hivyo, vikao kama hivyo havina budi kuwa na:

- Mwenyekiti ambaye hufungua, huendesha na kufunga kikao.
- Katibu wa kuchukua mawazo makubwa na kuyaandika vema kama kumbukumbu.
- Wazungumzaji wakuu au wadokezi wa suala.
- Washiriki wote.

### *(ii) Kuandika*

Zoezi la kuandika ni kumfunza mwanafunzi kufikiri, kusikiliza, kuchunguza mambo, na baadaye kuandika ibara hata taarifa ndefu pamoja na kujieleza kwa njia ya maandishi.

### *(a) Kuandika Barua*

Waswahili husema barua au waraka ni:

- *Nusu ya kuonana*: Inawakutanisha kwa namna fulani watu wawili. Kwa njia ya barua mwandikaji humshirikisha mwandikiwa mawazo yake pengine na hisia zake. Wanaonana kwa mbali.
- *Mjumbe au Risala*: Barua inatumwa iende kwa fulani ikamwambie mambo kadha wa kadha. Kwa hiyo uiandike barua yako vema ipate kusema utakalo, ieleweke na ikuletee mapato yale unayotamani, wala isiwe kinyume chake.
- *Kumbukumbu ya kudumu:* Barua inadokeza tabia, elimu na nidhamu ya mwandikaji wake. Tena kinyume cha maneno yanayosemwa tu kwa mdomo na kupotea hewani, barua huhifadhika. Huweza ikawekwa katika jalada (faili) na pale ikadumu kuwa kumbukumbu ya daima.
- *Barua ni shahidi wa nafsi*: Maneno yaliyoandikwa katika barua na kuambatanishwa na saini unayoinandika kwa mkono wako chini yake ni shahidi mkubwa. Yaweza kukuokoa barazani au kukuponza moja kwa moja.

Kwa hiyo uandikapo barua yoyote:

- Iandike kwa makini, tahadhari na bila hasira.
- Iandike kwa upendo na mpango safi, kwa mwandiko safi unaosomeka bila shida.
- Uzito wa barua unategemea tarehe na saini yako ya mwisho; kwa hiyo usisahau kuandika kwa mkono jina lako.
- Na kamwe usiandike barua kwa mtu mwenye madaraka wakati umekasirika, kwa kuhofia usije ukaandika mambo ambayo katika utulivu wa akili na moyo hungethubutu lau kuyataja tu kwa kinywa.

***(b) Aina za Barua***

Zifuatazo ni aina kuu za barua zinazoandikwa mara kwa mara:

**1. *Barua za Kirafiki:***

- Hizi ni barua wanazoandikiwa wazazi, marafiki, watani na wajuani. Hizi zina uhuru mkubwa katika kuziandika. Hazidai utaratibu wa pekee sana. Mtu huwa huru kuandika upendalo ilimradi halimvunjii mtu heshima yake.

- Barua ya aina hii huandikiwa marafiki, na jamii. Huwa mwandishi anajuli kama kwa wale anaowaandikia kwa hivyo si lazima iwe na sahihi yake au majina (yake yote) kamili. Kwa kawaida barua hii inaanza kwa salamu. Huwa ina anwani ya mwandishi peeke. Mwishoni mwandishi huweza hata kuwatumia salamu watu wengineo anaowajua na wanaomjua.

***(i) Muundo wa Barua ya Kirafiki***

Shule ya Msingi Mtakanini,
S. l. p 115,
Namtumbo.
Agosti 3, 2005

Kwa Baba mpendwa,

Ni matumaini yangu kwamba hujambo, tangu tulipoachana. Je, majirani zetu huko nyumbani huwajambo? Mimi ni mzima, sina neno.

Madhumuni ya kukuandikia barua hii ni kukuarifu Maonyesho ya Kilimo ya Wilaya ya Namtumbo. Kila mwanafunzi anahitajika kulipa shilingi mia moja za kugharamia nauli, chakula na kiingilio. Nakuomba unitumie pesa hizi tafadhali Baba, ili niweze kuandamana na wenzangu.

Nisalimie Mama, ndugu zangu na wote wanaonifahamu. Kwa heri kwa sasa.

Ni mimi Kitinda-mimba wako,
Mariamu.

## Zoezi

1. Wewe u mwanafunzi katika shule ya bweni. Mwandikie mama yako barua ya kumjulisha siku ya kufungwa kwa shule, huku ukimuomba aje kukuchukua kwenda nyambani.

2. Umefuzu katika mtihani wako. Ndugu yako anayefanya kazi Nairobi, alikuwa amekuahidi zawadi ,maalum, ukishapita mtihani huo. Sasa mwandikie barua, umuombe akuletee zawadi.

3. Umepata habari kwamba rafiki yako alipatwa na ajali ya barabara. Kwa sasa amelazwa katika hospital kuu ya Mkoa wa Mashariki. Mwandikie barua ya kumpa pole na kumtakia apone haraka.

4. Likizo ya mwisho wa mwaka imekaribia. Mwandikie Baba yako anafanya kazi katika nchi za mbali. Mwambie akuletee nguo mpya na aje kushiriki nanyi wakati wa Sikukuu.

5. U mwanariadha mashuhuri sana. Umechaguliwa kuiwakilisha shule yako katika mashindano ya Wilaya. Mwandikie barua rafiki yako, umweleze vile ulivyoshiriki na kupata ushindi katika mashindano ya Kata.

**2. *Barua za Mwaliko:***

Unapoalikwa kwenye michezo, tafrija, mikutano ya vyama au kwenye midahalo, unaandikiwa barua za mwaliko yenye sifa kama ifuatavyo:

1. Barua hizi sharti ziwe fupi na wazi.
2. Zitaje tarehe, saa na mahali pa kukutania;
3. Jina la mwalikaji na anwani yake kamili lazima itajwe;
4. Aidha, jina la mwalikwa na kusudi la mwaliko na pengine vitu anavyopaswa kwenda navyo inapaswa vitajwe.

3. ***Barua za kazi na shughuli*:**

Barua zinazohusika hapa ni zile za kuomba kazi, kutoa ripoti ya kikazi, shughuli za kiserikali, kichama na kidini.

Katika barua hizi kumbuka:

1. Kutaja nambari au/ na tarehe ya barua zinazopaswa kurejewa; (ii) Kichwa cha barua na aina ya shughuli unayotaka izingatiwe.

***4. Barua ya Kiofisi (Rasmi)***

Barua ya aina hii huandikiwa Maafisa wa Serikali au Makampuni ya watu binafsi. Kwa kawaida, maafisa hawa si lazima wamjue mwandishi. Barua rasmi, basi huwa na anwani ya mwandishi (upande wa juu, mkono wa kulia) na anwani ya anayeandikiwa, upande wa kushoto. Anwani hufuatiwa na mtajo – (kichwa cha habari). Barua hii huanza moja kwa moja, bila salamu. Ujumbe pekee ndio unaoandikwa. Mwishoni, mwandishi huandika majina yake kamili (rasmi) na sahihi yake.

(iii) ***Mfano/Muundo wa Barua Rasmi:***

Shule ya Msingi Mtakanini,

S. L.P 115,

**Namtumbo.**

Agosti 3, 2005

**Mkurugenzi,**
Chama cha Wakuza Mboga,
Sanduku la Posta 225,
NAMTUMBO

**KUH: UUZAJI WA MBOGA**

Ningependa kukujulisha ya kwamba Wanafunzi wangu wa **Chama cha K4M** wamekuza kabichi na karoti nyingi.

Nakuomba utusaidie katika uuzaji wa mboga hizi ambazo kwa sasa tayari zimekomaa.

Natumai utatusaidia uwezavyo.

Ahsante.

Wako mwaminifu,
(Sahihi)

Nasoro Kasimu Njarambaya
MWALIMU MKUU

- Anwani

Kama mwandishi na mwandikiwa wote wanapatikana katika *nchi moja* (Tanzania, Kenya, Uganda, Zimbabwe, Zambia, Malawi, nk.), basi anwani huandikwa ndani ya barua kama ifuatavyo:

Shule ya Msingi Mtakanini,
S.L.P 115,
Namtumbo.
Agosti 3, 2005

Lakini juu ya bahasha, yaani kule inakopelekwa barua, huandikwa kama ifuatavyo:

Mkurugenzi,
Chama cha Wakuza Mboga,
S.L.P 225,
NAMTUMBO.

Kama mwandishi na mwandikiwa wote wanapatikana katika *nchi tafauti* (anayeandika yuko Tanzania, na anayeandikiwa yuko Kenya , Uganda , Zimbabwe , Zambia au Malawi, nk.), basi anwani huandikwa ndani ya barua kama ifuatavyo:

Shule ya Msingi Mtakanini,
S. l. p 115,
Namtumbo.
TANZANIA
Agosti 3, 2005

na juu ya bahasha, yaani kule inakopelekwa barua, huandikwa kama ifuatavyo:

Bwana Paul Kipruto,

Chama cha Wakulima Langas,

S.l.p  146,

Eldoret,

**KENYA**

***(iii) Mfano wa Bahasha***

Bwana Paul Ngao Simala,

Chama cha Wakulima Mumias,

S.L.P  146,

Eldoret,

**KENYA**

Barua za Biashara na Matangazo: Matangazo ya biashara magazetini ni ghali. Kwa hivyo, barua ziwe fupi na wazi ili zisimpotezee mfanyabiashara muda wake.

- Simu: Kuna simu ya mdomo  na barua ya simu. Barua za simu ni fupi sana. Mtu huna fursa ya kueleza mengi au kuzungumza moja kwa moja na yule unayempelekea taarifa. Isitoshe barua za simu zatarajiwa kwenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida.

Gharama ya kuilipia hukadirwa kwa idadi ya maneno yaliyoandikwa:
maneno mengi, gharama kubwa, maneno machache, gharama ndogo.

Kwa ufupi, kuna barua ya *kirafiki (kindugu)* na *barua ya kiofisi (rasmi)*.

## Hatua za Kuangalia katika Barua

Hatua zinazotakiwa kuchukuliwa wakati wa kuandika barua ni kama ifuatavyo: (a) *Hatua ya Jumla*:

(i) Anwani ya mwandikaji, *ndani ya barua,*

(ii) Anwani ya mwandikiwa iandikwe vema, *juu ya bahasha* na pengine *ndani ya barua pia*;

(iii) Tarehe,

(iv) Salamu (maamkio), (v) Barua yenyewe,

(vi) mwisho wa barua.

(vi) Tumia karatasi na bahasha safi.

(vii) Juu ya bahasha ya mtumiwa barua, iwekwe stempu inayostahiki;

(viii) Kama ni kifurushi, funga kamba kwa umbo la kukatana;

(ix) Iwapo ni rejesta, chora mistari ya kukatana: moja wa wima na mwingine wa kulala katikati ya bahasha nyuma na mbele.

(b) *Hatua za Pekee:*

(i) Katika Barua za Kazi na Shughuli za Kiserikali:

Licha ya hayo yaliyotajwa katika (a) hapo juu,

- Andika kichwa cha barua kinachotaja nia ya barua kwa sentensi moja fupi kabla ya maelezo ya barua yenyewe.

- Barua nzima iwe fupi na wazi.

(ii) Katika Barua za Biashara:

Pamoja na hayo yaliyotajwa katika (a) hapo juu,

- Ongeza orodha ya vitu unavyoagizia.
- Eleza jinsi ya kulipia iwapo ni kwa *fedha taslimu*, au *malipo mara upokeapo vitu unavyoangiza* yaani, (c.o.d }ikiwa na maana ya: (‘cash on delivery’} au iwapo ni kwa *hundi*.

(iii) Barua za Simu

Mambo muhimu yanayotakiwa katika barua za simu ni:

- Anwani kamili ya mtu yule unayempelekea simu.
- Toa taarifa kwa kifupi na wazi kwa maneno yasiyozidi kumi.
- Kumbuka maneno yote yanaozidi kumi ya kwanza utatozwa zaidi.

- Andika anwani ya mtuma simu.
- Malipo taslimu ya nayotolewa palepale posta.

(iv) Kutuma Fedha kwa Simu:

Ili kutuma fedha kwa simu zingatia mambo haya:

- Lipa fedha taslimu kwa postamasta ofisini pamoja na ada ya kupelekea hizo fedha.
- Dai risti ya kupelekea hizo fedha, nayo uitunze ili uweze kuitumia kudai pesa zako hizo ikiwa zitapotea.
- Mwandikie nduguyo unayempelekea hizo fedha ukimwarifu kwamba umemtumia fedha kiasi kadhaa, ili atakapoitwa posta na kuulizwa nani amemtumia fedha hizo, aweze kutaja jina lako na kupewa fedha zake.

(v) Kutuma Fedha kwa Barua ya Rejesta:

Pamoja na kutumiwa fedha kwa njia ya simu, kupo pia kupelekewa fedha kwa *barua ya fedha* au *rejesta*. Hapa yafaa kukumbusha tu kwamba uchukuapo fedha zilizofika kwa rejesta, ifungue bahasha mbele ya postamasta na kuhesabu kwa uangalifu pesa zilizomo mbele yake, ili zikipungua au zisipokuwamo uweze kuanza madai mbele yake yeye akiwa shahidi.

(vi) Kutuma taarifa kwa njia ya Faksi

Pamoja na simu leo kuna teknolojia za kisasa zaidi za kupashana habari.
Nazo ni: *Teleprinta, Teleksi, Faksi* na *Intaneti*.

Kwa mfano, ukitaka kutumia taarifa kwa faksi, njia ambayo bado inayohifadhi siri kwa kiasi kikubwa, na inayochukua muda mfupi na gharama ndogo ni *faksi*.

Unachotakiwa kukifanya ni

- Kuandika taarifa yako kikamilifu kwenye karatasi nyeupe.

- Kisha ipitishe hiyo karatasi yenye taarifa yako kwenywe *mashine ya faksi* ambayo itaituma taarifa yako huko unakotaka iende.

Huko iendako itapokelewa na faksi-mashine nyingine ambayo itatoa kwa maandishi *nakala halisi* (kopi) ya taarifa yako ambayo ataipokea uliyemtumia.

1. Tarehe zinaweza kuandikwa kama ifuatavyo:

   (a) 3, Agosti, 2005

   (b) 3 – 8 – 2005

   (c) 3/8/2005

2. Anwani inaweza kuandikwa kama ifuatavyo:

   (a) Shule la Msingi Mtakanini,
   S.L.P. 115,
   <u>NAMTUMBO.</u>

   au

   (b) Shule ya Msingi Mtakanini,
   S.L.P 115,
   <u>NAMTUMBO.</u>

**Zoezi**

1. Wewe u mwanafunzi katika shule ya bweni. Mwandikie mama yako barua ya kumjulisha siku ya kufungwa kwa shule, huku ukimuomba aje kukuchukua kurudi nyumbani.
2. Umefuzu katika mtihani wako. Ndugu yako anayefanya kaziDar es Salaam, alikuwa amekuahidi zawadi maalum endapo ungepita mtihani huo. Sasa umepita. Mwandikie barua ukimuombea akuletee zawadi aliyokuahidi
3. Umepata habari kwamba rafiki yako alipatwa na ajali ya barabarani. Kwa sasa amelazwa katika hospital kuu ya Mkoa wa Ruvuma. Mwandikie barua ya kumpa pole na kumtakia apone haraka.
4. Likizo ya mwisho wa mwaka imekaribia. Mwandikie baba yako anayefanya kazi katika nchi za mbali. Mwombe aje na nguo mpya kushiriki pamoja nanyi wakati wa sikukuu.
5. U mwanariadha mashuhuri sana. Umechaguliwa kuiwakilisha shule yako katika mashindano ya Wilaya. Mwandikie barua rafiki yako, umweleze vile ulivyoshiriki na kupata ushindi katika mashindano ya Kata
6. Mama yako amelazwa hospital baada ya kujifungua. Wewe ni mwanafunzi katika shule ya msingi. Mwandikie barua mwalimu wako mkuu umwombe ruhusa ya kutohudhuria shule siku moja ili umtembelee mama yako hospitalini.
7. Umefuzu mtihani wako wa Darasa la Saba lakini hujachukuliwa kujiunga na shule yoyote ya sekondari. Andika barua ya maombi ya nafasi ya kusoma katika shule yoyote ile ya sekondari hapa nchini Tanzania.
8. Umeshindwa kuendelea na masomo yako kwa sababu ya ukosefu wa karo. Mwandikie barua mjumbe wenu umwombe akuchangishie pesa za karo kwa njia ya Michango ya Wahisani, yaani Harambee.
9. Mwandikie barua mhariri wa gazeti la Taifa Leo umwarifu kwamba ungetaka kumtumia mashairi ambayo umeyatunga ili ayachapishe katika gazeti lake.
10. Wewe ni katibu wa Chama cha Uhifadhi wa Mazingira. Umwandikie barua Mkuu wa Mkoa wenu umwalike katika sherehe za upandaji wa miti zitakazokuwa shuleni mwenu.

## Marejeo


1. Akwisombe, A. (1976), *Welewa na Muhtasari.* Tanzania Publishing House: Dar es Salaam.
2. KCPE, (KCPE, (2001), *Gold Medal Kiswahili*. Macmillan: Nairobi.
3. Mhina, G.A. *Vifungu vya Ufahamu.* Oxford: Nairobi.